

# DZUWA

JUNI 2021 TOLEO LA II

KUHESHIMU URITHI WA UDHABITI, UPONYAJI NA UPINZANI

# NENO KUTOKA KWA JUKWAA LA THE FEMINIST REPUBLIK

Ilizinduliwa mnamo Julai 2020, Dzuwa jarida la mkondoni linalochapishwa na Feminist Republik linalenga kuangazia mazoea ya kibinafsi na ya pamoja ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu wa Kiafrika na kwa wakati huo huo kuunda jukwaa la ushiriki na utunzaji wa maarifa. The Feminist Republik ingependa kujibu hitaji linalozidi kuongezeka la WHRD wa Kiafrika kupata vifaa, maoni na rasilimali ambazo zinaweza kukuza utunzaji wao wa kibinafsi na wa pamoja tunapokabiliana na janga la COVID - 19, na jarida la Dzuwa ni zana mojawapo ya vifaa kama hivyo. Toleo hili linaangazia miongoni mwa juzuu zingine, hadithi za uthabiti na maoni kuhusu haki ya uponyaji kutoka kwa watetezi wa Haki ya Ulemavu na wanaharakati. Hadithi hizi zinafunua fursa za kuungana na kila mmoja na jamii zetu licha ya kuwa tuko katika maeneo mbali mbali tunapopatikana wakati huu wa shida.

Dzuwa Toleo la II linalenga haswa Haki ya Ulemavu, tamko ambalo halieleweki na wengi. Haki ya Ulemavu kama utakavyosoma katika baadhi ya juzuu humu ndani inachunguza kwa kina ulemavu na kasumba ya kujiweza na jinsi ambavyo inahusiana na aina nyingine za ukandamizaji. Dzuwa Toleo la II linazingatia jinsi ambavyo Haki ya Ulemavu inaweza kutumika kama kifaa chenye nguvu cha kupambana ili kupata mabadiliko ya kijamiina pia namna tunavyotazama na kuelewa ulemavu ambayo haijajumuisha tu upatikanaji lakini pia jinsi tunavyoendesha mashirika katika jamii. Katika Dzuwa Toleo la II sisituna **"heshimu urithi wa uthabiti, uponyaji, na upinzani"** wakati wa shida na hata baadaye zaidi.

Katika toleo hili, tunasherehekea uzoefu wa wanaharakati katika kipindi cha COVID – 19, kuangazia simulizi kuhusu jinsi ambavyo WWU wameweza kupona na kutunzana miongoni mwao licha ya hatari nyingi wanazokabiliana nazo.
Katika kipindi cha COVID-19 tumeshuhudia Wanawake Wenye Ulemavu (WWU) kwa namna zisizo zenye usawa wakipata athari na vizuizi vya kimazingira ambavyo vimepunguza uwezo wao wa kusonga kimwili, vizuizi vya kifedha ambavyo vimewafanya watu wenye uwezo wa kifedha tu kupata kile wanachohitaji na vizuizi vya kitaasisi na vya kimfumo ambavyo vimewanyima nafasi ya kupata kwa mahitaji ya msingi na fadhila.

Tunapofanya kazi ili kutunza na kushiriki maarifa, tunakusanya kutoka kutoka Wanawake Mbalimbali wa Kiafrika ambao ni Watetezi wa Haki za Binadamu na maeneo mbalimbali, wito wetu kupitia jarida hili ni kwamba sasa tuweze kusonga kutoka kwa Sheria za Haki ya Ulemavu na kuelekea Utekelezwaji wa Haki ya Ulemavu, kufikia juhudi zaidi za pamoja na kutafakari upya ulimwengu wa harakati zenye muingiliano zisizoegemea kasumba ya kujiweza, ambayo inafafanua vipaumbele na kuanzia ardhini ikienda juu.

Kupitia mashairi, kazi ya sanaa na mahojiano, tunatarajia kuwa WHRD wa Kiafrika (Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu wa Kiafrika) na washirika vile vile wataweza kupata uelewa mzuri zaidi juu ya jinsi kasumba ya kujiweza inavyoungana na harakati zote tofauti na mifumo mingine ya ukandamizaji. Toleo hili limeundwa kwa msaada kutoka kwa wanaharakati, watetezi na walindaji wa utekelezweaji wa Haki ya Ulemavu na kutayarishwa na msaada kutoka kwa **Ndapwa Alweendo** mwanaharakati wa kifeministi kutoka Namibia, **Faith Njahira** Bingwa wa Utekelezwaji wa Haki ya Ulemavu kutoka Kenya na **Ekaete Umoh** mtetezi wa utekelezwaji wa Haki ya Ulemavu kutoka Nigeria ambaye hivi karibuni alijiunga na Bodi ya Urgent Action Fund - Afrika. Wameweza kutoa maarifa muhimu yasiyopimika thamani kwa Dzuwa Toleo la II.
Tunatumai ya kwamba utaweza kufurahia Dzuwa Toleo la II na ujisikie huru kuwasiliana na sisi ukishiriki maoni, mapendekezo yako na dhana zako kupitia **feministrepublik@uaf-africa.org.**

**Shinaz ALI -**
**Feminist Republik Mtunza Utamaduni,**
**Mhariri Dzuwa II,**
**Juni 2021**

# HAKI YA WALEMAVU: ZAIDI YA KUBADILISHA JINA TU

NA FAITH NJAHIRA

Salamu kwa ndugu zangu, wapenzi, wazee wenye ulemavu, na hata washirika wentu wengine wasiokuwa na ulemavu!

Ni furaha yangu kuu kukukaribisha kwenye toleo hili la Dzuwa ambapo tunafanya jaribio la kuwainua na kuwaweka katika nafasi ya kipaumbele wale wenye ulemavu na maswala ambayo yanatuhusu kama hatua za kuelekea kufikia haki ya walemavu. Natambua kuwa neno "haki ya walemavu" na dhana inayowakilishwa huenda ikawa ni jambo jipya kwa wengine wetu kwa hivyo nitajaribu kulifafanua kama utangulizi.

Haki ya Walemavu ni neno lililobuniwa na kundi la watu wenye rangi za ngozi nyeusi na kahawia, wenye jinsia kinzani, wabadili jinsia, na wale wasiotambua baina ya jinsia, na ambao pia walikuwa na ulemavu waliokuwa wanaishi katika eneo la Kisiwa cha Turtle, Marekani ya Kaskazini. Walitaka kuangazia umuhimu wa vile ambavyo rangi ya ngozi ya mtu, jinsia, uraia, matumizi ya huduma za matibabu ya magonjwa ya kiakili, ulemavu ulio dhahiri na hata ule usioonekana, na hata hali ya kukosa makao ni mambo muhimu ambayo huumba upatikanaji wa haki kwa watu wenye ulemavu mbali na sera za serikali.

Haki ya walemavu kama tafakari katika jamii kwa mujibu wa Sins Invalid (mradi wa kisanii unaoendeleza haki ya walemavu na wenye lengo la kukuza vipaji vya wasanii wenye ulemavu) inaongozwa na maadili kumi (10) yafuatayo: muingiliano, uongozi wa wenye athari kubwa zaidi, siasa zisizo za kibepari, kujitolea kwa utenda kazi unaozingatia harakati, kutambua ukamilifu, uendelevu, kujitolea kuendeleza mshikamano kwenye aina mbalimbali za ulemavu, kutegemeana, ufikiaji wa pamoja na ukombozi wa pamoja.

Kwenye mshikamano wa watu wenye ulemavu, ningependa kutumia maneno ya Patty Berne kuhusu haki ya walemavu "Hii ni haki ya walemavu, kutolewa kwa heshima kwa urithi wa muda mrefu wa uthabiti na upinzani ambao ni urithi wetu sisi sote ambao miili au akili hazitawiana. Haki ya Walemavu ni maono na mazowea ya hali ambayo bado haijatokea, ramani ambayo tunaiunda kwa pamoja na mababu zetu na hadi kufikia vitukuu wetu na hata kuendelea, katika mapana na vina vya uzidishaji na historia, harakati ambayao inaelekezea ulimwengu ambamo kila mtu atatambulika kama mzuri na kila akili itatambulika kama nzuri."

Iwapo unashangaa ni jinsi gani ambavyo dhana hii ambayo iliundwa nje ya bara la Afrika inaweza kututumikia sisi, hizi ndizo fikira zangu kuhusu jinsi ambavyo tunaweza kujihusisha na kutwaa haki ya ulemavu kwa njia yenye manufaa kwetu.

Kwa sehemu kubwa sana, kazi ya huduma kwa walemavu imekuwa ikifadhiliwa na kuongozwa na mashirika yasiyo ya kiserakali ya kimataifa ambayo yalianzishwa katika maeneo yaliyo mbali na Bara la Afrika. Haya mashirika yenye nia njema huwa kwa mara nyingi hayana uzoefu wa moja kwa moja wa kupambana na maswala ya ubaguzi wa rangi ya ndani kwa ndani au kushiriki uelewa wa karibu wa kukabiliana na kukumbana na kasumba ya kuyaona mashirika kama haya ya wakombozi wenye asili za kizungu. Hawajashirikiana kwa uaminifu na mifumo inayofanya kazi zao kuendelea kama vile vita vinavyofadhiliwa na serikali zao au miundo yao ya utawala inayodumisha hali yenye madaraja ya vyeo na ambamo mara nyingi huwa na watu wazungu wa jinsia ya kiume wanaounda idadi yao ya watu walemavu katika nafasi za juu za usimamizi. Wakati wowote ambapo kuna mahitaji anuwai (hata iwapo yanapingwa) na serikali za Kiafrika yamekuwa na matokeo ya mashirika haya kuwaajiri Waafrika wenye rangi nyeusi kwa nafasi za juu za uongozi barani, watu hawa mara chache ni watu wenye ulemavu.

Toleo hili linakujia kama kazi ya upendo, matokeo ya uhusiano wa miaka mingi kwenye majukwaa ya vyombo vya habari kwenye mitandao ya kijamii ambapo nimeona ndugu zangu wenye ulemavu wakidai nafasi bila kusubiri ruhusa kutoka kwa ulimwengu ambao haujaundwa kwa miili na akili zetu ambazo zina ulemavu, iwe imethibitishwa au haijathibitishwa na mfumo uliopo wa matibabu.

Michango katika toleo hili imetolewa kwa ukarimu wakati wa vipindi vya unyogovu, wakati wa kufanya kazi, hata wakati wa uchovu mkubwa, utambuzi mpya wa maradhi, vipindi vya kufanya maamuzi ya kubadilisha maisha wakati wa janga bila uhakikisho wa kupata ajira, au kupitia vipindi vya maumivu sugu.

Toleo linaunda nafasi ya masimulizi yote ya kubuni na yasiyo ya kubuni ya uzoefu wa moja kwa moja kwa wenzetu waliochangia na watu ambao wanahisi kuonekana na kushikiliwa katika maandiko haya. Utapata maandishi kutoka bara zima yanayozungumza juu ya miradi ya walemavu wa aina mbalimbali katika anuai, hali halisia za ulemavu ambazo zinaweza tu kunaswa kwa maandishi ya kubuni, na kufadhaika kwa wanariadha walemavu na womn viziwi wanaofanya kazi katika miradi ya kupunguza uchafuzi wa mazingira katika ulimwengu ambamo ulemavu fulani ni matokeo ya moja kwa moja ya udhalimu wa kimazingira.

Maandishi yameshirikiwa kwa uaminifu mkubwa kwamba toleo hili linayashika kwa upendo na moyo wa kujali. Kwa wachangiaji ambao wameniamini mimi na wengine kwenye timu yetu na maandishi yao, nawashukuru kila mmoja na natumai kuwa mnajisikia kuthaminiwa kwa kweli. Kwa msomaji aliye na ulemavu ambaye analisoma toleo hili, ni matumaini yangu kwamba utaifungua roho yako ili uweze kutabasamu, kucheka, kulia, na kuchukua wakati wa kupumzika wakati unaposoma au kusikiliza wasilisho hizi ambazo natumaini yanaturuhusu kufikiria juu ya ukombozi wa pamoja.

Inaendelea...

Kama watu wenye ulemavu, mara nyingi tunalazimishwa kuchagua ni maandishi yapi ambayo sisi tunaingia nayo kwenye baadhi ya nafasi na, tabaka zilizoongezwa za tambulisho za wabadili jinsia wetu, wenye jinsia kinzani, au wasiojiambatanisha na jinsia yoyote, au uraia wetu unaotiliwa shaka, hali ambayo mara nyingi hufanya iwe vigumu sana kwa ukamilifu wetu kutambuliwa. Ni matumaini yangu kwamba unajisikia kuonekana kupitia toleo hili.

Kwa washirika wetu wapendwa, ni matumaini yangu kwamba unakubali kuwa na usumbufu wa kutokuelewa kile tunachozungumzia katika baadhi ya maandiko kadhaa, ya kutoelewa “ni nini cha maana sana hapo” kuhusu baadhi ya maandishi yetu ambayo tunashiriki hapa, kutambua kwamba kazi nyingi zaidi zinahitajika kufanywa ndani kwa ndani ili kuhakikisha kuwa madhara kwa watu wenye ulemavu hayatoki tena kutoka mahali pa fadhila za wasioelewa kikamilifu, na kwamba unaisoma kwa upendo.







# Jamii ya Mkusanyiko Ndani ya Harakati

NA SHINAZ ALI-ZAIDS

Ninapokaa chini kuandika juzuu hili, siwezi kujizuwia ila kutafakari juu ya changamoto tulizopata katika kupata mawasilisho juu ya Haki ya Ulemavu. Mipango ya awali ya Dzuwa ilikuwa kulengwa tu haswa Haki ya Ulemavu Kusini mwa bara Afrika; uamuzi ambao ulifahamishwa na taarifa zilizopatikana kutoka kwa mpango wetu wa kutoa ruzuku katika shirika la UAF-Afrika. Ni mara chache sana tunapokea maombi kutoka kwa nchi hizi juu ya Haki ya Ulemavu na nilidhani kuwa huu ni wakati mwafaka wa kuangazia kazi ya wanaharakati na watetezi wa Haki za Ulemavu wa Kifeministi – Feminist Disability Justice - katika nchi hizi. Kwa kutarajia toleo hili, nilikuwa kama mtoto anayesubiri zawadi, nikifurahia kile tutakachoishia kuunda, kuwa na mhemko kwa kusikia kuhusu kazi ya wanaharakati wa Haki za Ulemavu nchini Lesotho, kugundua taarifa kuhusu njia za uponyaji nchini Botswana, na kuongeza mtandao wangu na wanaharakati kutoka Namibia. Walakini, msisimko wangu ulikuwa wa muda mfupi; matumaini yalianza kufifia nilipoanza ufikiaji mkondoni. Asilimia kubwa ya vikundi na mashirika vilijikita zaidi juu ya Haki za Ulemavu kwa ujumla. Wanaharakati wa kifeministi walikuwa wapi ambao wangezingatia haswa Haki ya Ulemavu? Wanaharakati wa haki za wanawake walikuwa wapi? Zilikuwa wapi sauti za wanawake ambao kwa miaka mingi wamekuwa wametengwa? Nani anazungumza na maswala ya ulemavu? Kwa niaba ya nani? Ni nani anayejali Wanawake wemye Ulemavu, almaarufu Womn With Disabilities (WWD)?

Kwamba hatukuweza kupata mashirika ya kifeministi yanayoshughulikia Haki ya Ulemavu ilinifanya nitafakari juu ya jinsi harakati imekuwa; eneo hili la kazi limeachwa kwa watetezi wa Sheria za Walemavu. Ukweli huu haukuonyesha mapambano ya Haki ya Ulemavu dhidi ya "uhuru" ambapo harakati zipo peke yao na hujitegemea wao wenyewe. Wakati wa uundaji wa Haki ya Ulemavu, Harakati ya Walemavu inapaswa kuwa na watu / vikundi ambao huiunga mkono kama tu vile ambavyo inavyopaswa nayo kuziunga mkono harakati zingine. Hatupaswi kutenganisha ulemavu na maswala ya rangi ya ngozi, harakati za kifeministi, Haki za Afya ya Kijinsia na Uzazi - SRHR, matabaka n.k. Ulemavu Haki, kwa yenyewe, inaangalia jinsi mifumo tofauti ya ukandamizaji inavyozidi kuongezea mingine. Kwa hivyo, tunapopambana na aina zingine za ukandamizaji, tunapaswa pia kuwa tunapambana dhidi ya kasumba ya uwezo na sehemu ambalo kasumba hii inachangia katika kulipaka mafuta gurudumu la mfumo dume. Maisha ya Wanawake Wenye Ulemavu - WWU hayapaswi kufanywa yasionekane wakati ambapo tunazingatia aina zingine za ukandamizaji kwa sababu zote zinaingiliana.

Kama watetezi wa haki na wanaharakati, tunahitaji kuangalia maswala yote na jinsi yanaingiliana. Hatuwezi kutatua suala moja na kuwaacha mengine yakingoja. Hili ndilo Haki za Ulemavu zimekuwa zikihusu; kuangalia dalili za kukosekana kwa usawa ndani ya Harakati ya Walemavu na sio kuzingatia sababu za msingi, kushughulikia maswala kwa njia ya moja moja ambayo huwatenga WWU kwa kuyatenga bila kuzingatia aina zingine za ukiukaji ambazo wanakabiliwa nazo kama wanawake ambao hawafuati ujinsia, wanawake ambao huabudu kwenye dini zingine, wanawake ambao ni miongoni mwa wasio na ardhi, na wale ambao ni kutoka jamii zingine ukizingatia rangi ya ngozi. Orodha inaendelea ...

UAF-Afrika na jukwaa la The Feminist Republik linajaribu kuziba mapengo wakati kuna ukosefu wa sauti katika nafasi ambapo zinapaswa kuwepo na mapungufu ambayo yanatokana na ufadhili ambao sio wa kutosha kwa kazi ya Haki ya Ulemavu barani Afrika na vile vile ukosefu wa umoja katika harakati. Karibu 4% tu ya fedha ambazo UAF-Afrika inapokea kusaidia wanaharakati wa kifeministi ni kutoka kwa wafadhili ambao wamejikita katika kazi ya ulemavu. Hii inazuia ufikiaji wa eneo hili la ulemavu lakini pia inapunguza juhudi za Feminist Republik za kueneza utunzaji wa pamoja na uponyaji haki kwani rasilimali fedha ni muhimu kuhakikisha kuwa utunzaji ni kiini cha Haki ya Ulemavu haswa wakati wa janga. COVID-19 imefanya wanawake wenye ulemavu waweze kuingia kwenye hatari ya kukabiliwa na shida ya akili na maswala mengine ya akili na afya, mengine ambayo yamesababishwa na kutengwa. WWU wanaendelea kukabiliwa na changamoto katika kushiriki katika hafla mbalimbali tofauti na kuwaacha watafute njia mbadala za kujitunza wao wenyewe. Katika kutafuta mabadiliko,

***Hatuhitaji kusahau kwamba watu ambao wameathiriwa zaidi wanapaswa kuwa kwenye kiini cha mazungumzo hayo juu ya mabadiliko.***

# Jamii ya Mkusanyiko Ndani ya Harakati

NA SHINAZ ALI-ZAIDS

Ulemavu Haki unategemea ushirikiano (ufikiaji wa pamoja na utunzaji wa pamoja) kinyume na utunzaji wa kibinafsi. Bila kufanya mabadiliko haya kutoka kwa utunzaji kama jukumu la kila mmoja peke yake na kufikia utunzaji kama ilivyoainishwa katika Haki ya Ulemavu, hatuwezi kutarajia uponyaji wa WWU. Hii imekuwa dhahiri hata zaidi na ujio wa COVID-19. Tuliona jinsi ambavyo utunzaji wa WWU ulivyoachwa kwenye majalala, na kuwepo tu jukumu la kila mtu binafsi badala ya jukumu la pamoja.

Kuhama kutoka hali hii kuelekea umoja zaidi katika kibinafsi na jamii, lazima tuunde mtandao wa utunzaji wa pamoja ambapo wanaharakati wanaweza kushiriki uzoefu wao, kujifunza kutoka kwa wenzao, na baada ya muda wapate kupona. Kupona kama tunavyojua siyo tukio la kufuata mkondo halisi mara moja; kunachukua mitindo mbalimbali tofauti, kunachukua muda, na kunahitaji jamii, ikishikilia nafasi yetu sisi wenyewe na za jamii zetu. Je! Tunaundaje jamii ya utunzaji ambayo inatambua utimilifu wa watu binafsi na inathamini chochote wanacholeta mezani kulingana na uzoefu wa maisha na mafunzo muhimu? Hapa ndipo mahali ambapo mshikamano wa harakati unaokutanisha vitengo mbalimbali katika anuai unahitajika kutamba. Haki ya Ulemavu inahitaji mtazamo wa umoja.

Tuna nguvu ndani yetu kuunda tandu ya utunzaji ambayo inajumuisha kila mwanamke ambaye ameathiriwa na aina mbalimbali za mfumo dume, muundo ambao unaangalia WWU sio kama wanawake ambao wanahitaji misaada ya hisani lakini kama washirika katika mshikamano ambao hauna madaraja kiasili.

Kwa mshikamano tunahitaji kutambua rasilimali endelevu kwa utunzaji wa pamoja ndani ya harakati tofauti za walemavu na kote. Utunzaji wa pamoja haupaswi kuwa mahali pa kubatilisha au kupuzilia uzoefu wa wengine. Kuzingatia utunzaji wa pamoja haimaanishi kujitunza mwenyewe kibinafsi sio muhimu sana. Inatutaka kwamba sisi tufikirie hali inayowezekana ambapo WWU anashauriwa kutafakari au kuchukuwa muda wa faraja ili kupumzika katika ulimwengu ambao tayari umemtenga, kama moja ambayo inaweza kumfanya ajihisi ametengwa kama ilivyo tofauti na kutekeleza uponyaji, kutafakari, au kuchukua muda wa mapumziko katika jamii ambayo inaweza kuwa uzoefu mdogo zaidi wa kutengwa. Kwa kumalizia, kuna haja ya dharura ya kupata rasilimali, zote za kifedha na kiufundi, kwa kiwango ambacho kinajali umuhimu wa umoja na kina uhusiano na Haki ya Ulemavu. Zaidi ya hapo, uelewa ambao unawaruhusu wanawake wenye ulemavu kuweza kufafanua ni vipi ustawi unavyoonekana kwao kinyume na kujaribu kurekebisha kile tunachodhani kimeharibika, ni hatua muhimu sana ya kuendelea mbele. Miili yote huelezewa na ujinsia, dini, uwezo miongoni mwa vitambulisho vingine. Ni matumaini yangu kwamba harakati nyingi zaidi na zaidi zitaanza kuthamini jinsi zinavyounganishwa na kuingiliana na yasite kuwagawanya wanawake kwenye maghala mbalimbali haswa kutokana na mafunzo muhimu ambayo tumejifunza kutoka kwa janga hili.

**Bila jamii hakuna ukombozi - Audre Lorde**



# Kuhusu Modeli Aliye Kwenye Jalada La Jarida

PICHA NA SIMULIZI NA N A M A F U A M U T S E

Agnes Hausiku ambaye amefanya kazi na mashirika kama vile Chama cha Namibia cha wanawake ambao wana Uwezo Tofauti almaarufu Namibian Association for Diffrently Abled Womn kwa sasa anapata masomo ya kazi ya kijamii na ameajiriwa katika Wizara ya Madini na Nishati huko Windhoek kama afisa wa utawala katika idara ya ununuzi. Yeye ni mtetezi thabiti wa haki za walemavu na uwezeshwaji wa wanawake. Kujitolea kwake ni dhahiri katika kazi anayofanya na Kamati ya Kitaifa ya Olimpiki za Walemavu (National Paralympic Committee) juu ya mipango inayozingatia wanawake katika uongozi wa michezo na pia kilabu cha michezo cha Uwezo wa Magurudumu – Wheel Ability Club - huko Windhoek, ambapo, miongoni mwa shughuli zingine, yeye hucheza mpira wa kikapu. Hausiku pia ni mmoja wa wanachama wa Chama cha Watumiaji wa Viti vya Magurudumu cha Namibia – Namibian Association of Wheelchair Users - kilicho Windhoek, shirika linalotetea haki za watumiaji wa viti vya magurudumu, na vile vile Wanawake Wenye Ulemavu – almaarufu Womn With Disabilities (WWDs).

'' Ikiwa baadhi ya maeneo hayafikiki, hatuwezi kutarajia watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za kila siku — kuabiri shule, vituo vya ununuzi au jamii zao,"Agnes Hausiku anabainisha.



Wazo hili linachochea utetezi wake wa ufikiaji kwa kila mtu ulimwenguni, ambao anaamini kuwa utawezaleta fursa kwa watu wenye ulemavu na kuendeleza haki zao za binadamu. Kwa maoni yake, ulimwengu ambao ufikiaji wa kila mtu ulimwenguni kote unafikiriwa na kutekelezwa, silo swala la kujadiliwa. Anataka kuona watu wenye ulemavu "wakistawi katika mazingira ambapo wanaonekana na kutambuliwa." Anasisitiza kwamba tunaboresha jamii kwa kukuza uwakala na uongozi wa watu wenye ulemavu, kwani wanachangia uchumi wa nchi kwa njia ile ile ambayo wasio na ulemavu hufanya.

Uanaharakati wa haki za ulemavu ni suala kuu linalokutanisha masuala mengi, Hausiku anatafakari.

'' Kama mwanamke wewe tayari umepata hasara. Sasa fikiria kuwa wanawake aliye na ulemavu. Hiyo ni hasara mara mbili.

Ukosefu huu wa haki ndio unaomsukuma Agnes Hausiku kuwapa motisha wanawake wengine wenye ulemavu kwa kuishi maisha yake kwa uwezo wake wote, akijitahidi kuwafikia wengine na kujenga madaraja au kuchukua nafasi na fursa. Shauku inayomchochea kuwahamasisha wanawake wengine wanaoishi na ulemavu pia humfanya ahisi hali ya uwajibikaji kuongezea kwenye kazi yake, uanaharakati wake, na kila kitu anachokipenda juhudi zake bora zote bila kupuuza kujiburudisha na kujitunza.

'' Mtu wa kwanza aliyenipa uwezo na nguvu alikuwa ni bibi yangu, "anasema," Alikuwa mtu wa kwanza kuniona na kuwekeza kwangu. "Hausiku ana nia ya kusudi kuchukua nafasi na kuonekana katika jamii kwa sababu hii inadhihirisha uwakala na uongozi wa Wanawake Wenye Ulemavu (WWD) na huwapa motisha wanawake wengine wengi.

*'Kama mwanamke wewe tayari uko katika nafasi iliyo hasi. Sasa tafakari kuwa mwanamke aliye na ulemavu. Hiyo ni hasara mara mbili.''*



# Je, Ulimwengu Ulioumbwa kwa Sababu Yetu Unataka nini kutoka Kwetu?

Na Liz Ombati

"Jinsi ninavyotembea nikiwa hapa na nyinyi wote, wanaharakati wenzangu wenye ulemavu, najisikia mwenye furaha. Sijihisi mwenye kuhukumiwa. " Simphiwe, womn aliye na ulemavu anashiriki uzoefu wake wa kuyaendesha maisha ya kila siku na chumba kilichojaa wanaharakati wenzake. Anahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kuonyesha raha na faraja kwa wenzie, akiongeza, "Nje ya chumba hiki, barabarani, mahali pangu pa kazi, kanisani... lazima nivumilie kukodolewa macho."

Si wazi kila wakati kwa Simphiwe na marafiki zake ikiwa huku kukaziwa macho ni kwa sababu ya udadisi, au ni macho ya huruma au mchanganyiko wa zote mbili. Lakini huu ni uzoefu ambao watu waliopo chumbani wanalazimika kukabiliana nao katika maisha yao ya kila siku. Kama womn wenye ulemavu; watu wasiowiana na ujinsia wao na ambao wana ulemavu, watu wa LGBTI wenye ulemavu, wanamuelewa. Hapa, ndani ya usalama wa jamii waliyoiunda, ambapo wanajua kuwa kuzunguka ulimwenguni kama watu wenye ulemavu hakuwafanyi kuwa na raha iliyopunguka, wenye ushindani wa chini, wenye kutotamanika, kupunguza ugumu, wanaweza kucheka kuhusu masuala haya. Sio kwa sababu kuwa katika hali ya kupokea uchunguzi usioutafuta hakufikii viwango vya juu vya kuingiliwa usiri au kupunguziwa utu, il ani kwa sababu, katika chumba hiki, wanakuwa na uhuru kuwa vile walivyo wao wenyewe na maumbile yao.

Simphiwe na wanaharakati wenzake hawaogopi kuwa tofauti. Wana idadi za utofauti kama vile utofauti unaweza kupatikana, na hujitokeza kuonekana katika uzuri, nguvu, matumaini na ndoto zao, wasiwasi na hofu. Lakini, wakiendesha Maisha katika jamii ambazo kila siku wanalazimika kukabili jamii ambayo haielewi hili au haijapangiliwa kuwajumuisha, wanajifunza kujipa nguvu kila siku za kustahimili udadisi, kwa majengo ya umma na huduma za usafirishaji ambazo haziwajumuishi, kwa uchokozi mdogo unaokuja kwa njia ya maswali na maoni yanayotolewa pembezoni, au mbaya zaidi, kwa ubaguzi ulio wazi wakati wanaponyimwa nafasi za ajira na ushari wakati ambapo uhuru wao, hadhi na haki yao ya kuchagua inapuuzwa au kuchukuliwa kuwa kama si muhimu.

Jinsi ninavyotembea, nikiwa hapa na nyinyi wote, wanaharakati wenzangu wenye ulemavu, najisikia mwenye furaha. Sijihisi mwenye kuhukumiwa.

Kuna maneno ambayo yanaelezea uzoefu walioupitia. Haya ni kasumba ya uwezo. Kwa maneno ya kimsingi, kasumba ya uwezo inaelezea kuwa kuna watu ambao wanawaona watu wenye ulemavu kuwa ni duni - wasio na thamani wala karama. Mtu mwenye kasumba ya uwezo humwangalia mtu aliye na ulemavu na kufikiria: "Asante Mungu mimi sio wao." Kwa njia hii, kasumba ya uwezo huondoa uelewa zaidi, na kwa hiyo, dhana ya utu na haki sawa kwa kila mtu. Inawezesha chuki na ubaguzi. Katika jamii yenye kasumba ya uwezo, mwajiri huuliza, "Kwa nini nikuajiri wewe? Je, utakuwa na tija kama mtu mwingine ambaye si kama wewe?" Na katika wakati huo, yule aliye na ulemavu ameondolewa utu. Uingiliano huu haupo tu kwa mahali pa kazi. Inatokea katika taasisi za elimu ambapo watu wenye ulemavu wanajua vizuri sana hali ya kuwa tu takwimu; mmoja wa watoto wengi wenye ulemavu ambao wamewakilishwa zaidi kati ya watoto wanaokwenda shule ambao hawawezi kupata elimu bora. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni *, kuwa na ulemavu huongeza mara mbili uwezekano wa mtoto kama huyo kukosa kuhudhuria shule. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa sehemu kubwa ya bara, chini ya asilimia 10 ya watoto wenye ulemavu wako katika shule za msingi na ni asilimia 13 tu ndio hupata aina yoyote ya elimu. Wakati mwingine, nafasi pekee zinazopatikana kwa watoto wenye ulemavu ni shule zilizo mbali sana na nyumba zilizoitwa "maalum".

Ingawa watu wenye ulemavu hawaogopi kuwa tofauti, lebo "maalum" mara nyingi inaweza kuwa kisingizio kwa jamii ambayo inataka njia rahisi ya kujiondoa kwenye swala nyeti. Badala ya kufanya shule kupatikana kwa wanafunzi wenye ulemavu, jamii huchagua shule "maalum" ambazo huwatenga wanafunzi kutoka kwa mifumo yao ya msaada na kuwatoa nyumbani kwao. Watoto wenye ulemavu hawapaswi kulazimika kuchagua kati ya kupata elimu na kutengwa na familia zao, marafiki, na jamii. Walezi na watunzaji wenye ulemavu hawapaswi kulazimika kupitia mifumo ya elimu ambayo haitarajii mahitaji yao.

Jinsi ninavyotembea, nikiwa hapa na nyinyi wote, wanaharakati wenzangu wenye ulemavu, najisikia mwenye furaha. Sijihisi mwenye kuhukumiwa.

Katika chumba hiki, ambapo Simphiwe anashiriki uzoefu wake, wandugu wanaelewa wazi kuhusu ile kazi ambayo inahitaji kufanywa na wote wana umoja katika kujitolea kwao kutetea kuwepo kwa ulimwengu unaowahusisha zaidi womn wenye ulemavu, watu wasiofuata jinsia yoyote, na womn ambão ni transijenda wanaweza kuendelea kuwepo katika utofauti wao wa kijinsia na kiulemavu. Wao ni jamii. Wanakumbatiana wenyewe kwa wenyewe. Wanapata sauti zao wakati wanapozungumza juu ya matumaini yao na wasiwasi wao. Edna, mmoja wa womn anaambia kikundi kwamba kasumba ya uwezo imemuamulia kuhusu maisha yake ya kazi. Kasumba ya uwezo ndiyo sababu kubwa iliyomfanya asiombe kazi aliyokuwa ameitaka sana. Kasumba ya uwezo ilimuamulia uzoefu wake kama mwanafunzi anayeendesha mfumo wa shule katika jamii yake.

"Unauliza kwa nini ninahisi kuwa nilikuwa nikibaguliwa?" Anauliza. "Unakumbuka wakati tulizungumza kuhusu kasumba ya uwezo? Je! Unakumbuka wakati tulisema kwamba 'wao' hawakutengeneza jamii yao kwa ajili yetu? Walijiundia wenyewe. Walijiita 'wenye mili iliyo na uwezo'. Je! Ninaweza kucheka kidogo? Wao hawakujali. Kumbuka hawakujali kufanya elimu ipatikane kwetu. Kile ambacho hilo lilinifanyia mimi, lilitufnyia sisi, liliondoa fursa zetu za kuweza kupata kazi. Kisha pia, kwa namna fulani, tena, nikageuka kuwa takwimu. Tukawa sehemu ya utafiti. ['Watu wenye ulemavu wanawakilishwa zaidi kati ya wasio na kazi. Na wanapoajiriwa, asilimia kubwa wanalazimika kufanya kazi za kada za chini ']… je, unakumbuka jinsi elimu ilifanywa kuwa isiyoweza kufikiwa na sisi? Kazi na ajira pia?" Wakati Njoki anasimamisha hotuba yake iliyojaa mhemko, ukimya ndani ya chumba unaonekana.


**Ulimwengu. Ambao umetengenezwa kwa ajili yetu. Ulimwengu. Ambao hauna kasumba ya uwezo. Ulimwengu, ambapo tunaweza kutembea kwa ujasiri na raha, nje ya chumba ambacho kina wanaharakati wenye ulemavu, na bado tuhisi kutokuhukumiwa. Ulimwengu. Ambao umetengenezwa kwa ajili yetu sisi.**

Nje ya jamii zao salama, ulimwengu ambao Simphiwe, Njoki, na wenzao wanaufikiria una taswira gani? Ni ulimwengu ambao huwaona wao. Huwasikia wao. Huwajumuisha wao. Ni ulimwengu ambao hauwaangalii wao kwa huruma. Ni ulimwengu ambao unauliza, "Ofisi yetu iko kwenye gorofa sakafu ya nne juu na haina kambarau, hakuna barabara panda, kwani hii ofisi tulimuundia nani?" Ulimwengu uliyoundwa kwa wote unauliza, "Je! Ni nani mtoto ambaye hayuko shuleni, ni nani mwenye ulemavu - mwanamume, mwanamke, LGBTI, asiyewiana na jinsia yoyote – asiyefikia meza hii ya maamuzi? Nani ameachwa nje? "Ulimwengu uliyoundwa kwa manufaa ya wote huyauliza maswali haya yote na mengine zaidi. Ulimwengu ambao unafikiria ya kwamba utofauti huanza kushughulikia ukosefu wa haki wa mifumo yake yenye kasumba ya uwezo.

**Ulimwengu huu unasema, Tuangamize kasumba ya uwezo. Na inaanza sasa!**

Jinsi ninavyotembea, nikiwa hapa na nyinyi wote, wanaharakati wenzangu wenye ulemavu, najisikia nikiwa na furaha. Sijihisi kuhukumiwa.

*Chanzo: Ulimwengu Wao (Their World)




**UZERUZERU**

Rangi ni uwakilishi wa kujengwa wa kijamii lakini urembo wangu unazuia nguvu zangu katika ulimwengu ambao hauoni uzuri wangu.
Niko hapa na nitaonekana na kusikilizwa, ualbino wangu sio laana kama ilivyoonyeshwa hata kupitia historia, naweza kuonekana kuwa sina rangi lakini uso wangu ni turubai nyeupe kwa urembo wote ulimwenguni.

Miseda_Art



# Wanawake wenye Ulemavu na Harakati za Ufeministi – Ufikiwaji kwa Wote

NA EKAETE UMOH

Kwa miaka mingi, vyombo tawala vya harakati za kifeministi na Asasi za Kijamii (almaarufu CSO) havikuwa vinajumuisha Wanawake wenye Ulemavu (WWU) katika mipango yao, katika hatua za mipango na utendaji. Masuala yanayohusiana na WWU yalikuwa yana chukuliwa ni masuala ya walemavu na yalikuwa yanasukumwa katika harakati za walemavu.

Hakuna ubishi kwamba harakati za ufeministi zimebadilika sana na zina ufahari. Hata hivyo, ni nia yetu kuunganisha utofauti wetu. Hiyo itaonesha jinsi gani harakati za kifeministi zitakavyoshikamana na kuwa na nguvu. Uzuri wa harakati za kifeministi unategemea kuundwa kwa nafasi salama zenye uhuru wa kujieleza, wakati huo huo tukiunganisha pamoja nguvu zetu kupambana na changamoto za kutokuwepo kwa usawa na athari zake zozote zile.

Hata hivyo, inaelekea kuwa kazi ngumu sana kwenye harakati za kifeministi ili kuweza kufikia mpango jumuishi wa urithi wetu, kama kutakuwa na upungufu au baadhi ya walengwa kuachwa kwa makusudi au kwa kutokusudia. Wafeministi WWU wanapitia changamoto kubwa na vikwazo vya ushiriki wanapojaribu kujichanganya ama kujihusisha na harakati za kifeministi ama mahali kwingine kwa sababu ya ulemavu walio nao. Hata hivyo ulemavu siyo sababu inayojitosheleza kuweka vikwazo kwa wanawake yeyote kuwa na ushiriki kwa usawa katika harakati hizi.

Katika kujitoa kwenye uwajibikaji na kujenga harakati yenye uwiano, ni muhimu kujiuliza swali la marekebisho. Kwa mfano vikwazo hivi viko wapi? Vikwazo hivi vinaweza kudhihirika kwenye mitazamo hasi /ubaguzi ndani ya harakati ya kifeministi dhidi ya dada wenzetu wenye ulemavu. Inawezekana pia inachangiwa na hali ya kutojali kwenye mazingiria ya ujenzi liyowekwa ambayo inaweza kuwazuia dada wenzetu ambao wanatumia viti vya magurudumu kuweza kuhudhuria mikutano. Pia inaweza kuwa vikwazo vya kimawasiliano kwa dada wenzetu wenye ulemavu wa kusikia na kuona. Ama, kama ilivyo wakati mwingine, ni miundo na utekelezaji wa kisera na kisheria ambao unashughulikia ajenda za kifeministi ila bila kuyazingatia mahitaji ya walemavu, na ambazo zinaweza kuwaondoa WWU katika kushiriki kikamilifu, kwa sababu mara nyingi wanakuwa kama dhana ya baadaye au wale dada waliosahaulika.

*" ulemavu siyo sababu inayojitosheleza kuweka vikwazo kwa wanawake yeyote kuwa na ushiriki kwa usawa katika harakati hizi. "*

Mapambano yanayoendelea bila kusita ya WWU ili kupata nafasi na kutambulika katika vyombo vikubwa vya wanawake au vya kifeministi, na kundelea kusukumwa nyuma walikopitia kutoka kwenye harakati za kifeministi kumesababisha dada zetu wenye ulemavu kupata madhara makubwa ya kisaikolojia ambayo pia yamepelekea kuathirika pakubwa kwa afya yao ya akili na ustawi wao. Dada zetu wenye ulemavu wanaathirika sana kila mara wanapofurushwa kutoka katika nafasi ambazo kisheria ni zao, kutokana na kutokuwa na mazingira yanayoruhusu ufikiaji, mapengo katika uundaji wa sera ambayo yangekuza uwezeshaji wa wanawake au hata mtazamo wa kijumla kwamba "Wewe hufai kuwa hapa", ukosefu wa watafsiri wa lugha ya ishara ambayo ingewezesha kushiriki kikamilifu kwa dada zetu wenye ulemavu wa kusikia, upungufu wa taarifa muhimu /upatikanaji wa maandishi ya kifeministi katika nakala za nukta nundu kwa dada zetu wenye ulemavu wa kuona, na kiujumla kutokuwa na uelewa kuhusu umuhimu wa "uhusishwaji wa kuridhisha" na "ushiriki kikamilifu"

Baadhi ya dada zetu wenye ulemavu wamefikia kiwango ambapo hawana imani tena na harakati hizi kutokana na kutojumuishwa walikopitia kwa muda mrefu, ila pia baadhi ya wengine wamefikia hali ya kutokujithamini wakiwa katika mikutano ya kifeministi, ambalo ni jambo baya sana kwenye harakati za kifeministi. Ili kuangazia zaidi viwango vya madhara ambavyo baadhi ya dada zetu wanakumbana navyo, wanawake na wasichana wenye ulemavu wanaathirika na kutokuonekana siyo tu kwenye harakati za kifeministi bali pia hata kwenye harakati za haki kwa walemavu. Wanakumbana na mazowea ya mitindo ya mfumo dume katika harakati za wenye ulemavu na pia hawawezi kupata nafasi katika harakati za kifeministi; ni hatari mara mbili!

Mwaka wa 2014, nilichaguliwa kama rais wa kwanza mwanamke wa Sirika la Pamoja la Kitaifa la Watu Wenye Ulemavu – almaarufu Joint National Association of Persons With Disabilities nchini Nigeria, na kwa zaidi ya miaka 20 ya kuwepo kwa shirika hili, halikuwahi kuongozwa na rais mwanamke. Shirika hili limekuwa ni nafasi inayotawaliwa na wanaume na hakukuwa na fursa yoyote ya kuonekana kwa WWU aitha katika mipango yao au uongozi. Nilipotangaza nia yangu ya kuwa mwanamke wa kwanza kabisa kugombea kiti cha urais katika shirika hili nilikumbana na upinzani mkubwa sana kutoka kwa wagombea wenzangu wa kiume; wagombea wengine nane wote walikuwa wanaume. Kampeni zilikuwa na hali ya udhalilishaji mkubwa kwenye vyombo vya habari na kasumba za ubaguzi wa kijinsia yote hayo yakinuiwa kunikatisha tamaa ya kugombea. Nilipokea vitisho ili nijiondoe kwenye dimba hilo, lakini nilipambana na hatimaye nikachaguliwa. Kwa upande wangu nilikuwa na uelewa mkubwa wa maswala ya ulemavu na maendeleo, na nilikuwa na ushupavu wa kusukumiza upatikanaji wa haki kwa wenye ulemavu. Mwishowe, ijapokuwa waliuchukia uongozi wa mwanamke, hawakuweza kuuchukia uelewa na uzoefu wangu. Hali iliendelea kuwa ngumu zaidi kwa wale waliokuwa wakipinga uongozi wa mwanamke. Na pia nilikuwa na ushirikiano wa karibu kutoka kwa mashirika ya kutoa ufadhili na washirika wengine mbali mbali. Niliweza kushinda changamoto mbalimbali na kutekeleza miradi na mabadiliko yaliyohitajika kwa Watu Wenye Ulemavu. Lakini hata hivyo hii siyo taswira panan iliyoko kwa sasa kwa wengi wa womn wanaoishi na ulemavu. Harakati hii inastahili kubadili mwelekeo ili kuunga mkono waziwazi na kimakusudi uongozi wa wanawake. Wanawake wenye ulemavu wanakumbana na changamoto nyingi zaidi, na mshikamano na mifumo imara inahitajika.

Ulimwenguni kote utafiti umeonyesha ya kwamba vyombo tawala vya harakati za wanawake havija kuwa na kuzingatiwa kwa maswala ya wanawake wenye ulemavu, na hili limepelekea kuachwa nyuma kwa kwa kiwango kisichopungua asilimia 20 ya idadi ya watu ulimwenguni kote ambao ni wanawake na wasichana wenye ulemavu, almaarufu Womn and Girls with Disabilities (WGWD). Hii ni kwasababu WGWD ni asilimia 20 – 22 ya idadi yoyote ile ya watu popote. Hili linammanisha ya kwamba, katika nchi yoyote ile, ukizingatia idadi ya yoyote ya womn iliyomo, asilimia 20 ya idadi hiyo wanatarajiwa kuwa ni WGWD. Hebu tafakari viwango vya hasara wakati ambapo harakati ya kifeministi inapopoteza kwa kutozihusisha sauti ambazo ni asilimia 20 ya idadi yake yote na hebu fikiria hasara kubwa zaidi ya kupoteza watu wengi sana katika uhamasishaji kwenye dunia nzima kwenye maswala ya kifeministi. Asilimia 20 ni idadi kubwa tu sana ya kuweza kupuuziliwa katika ajenda zozote za maendeleo zinazolenga maswala ya kifeministi. Ingekuwa vizuri sana kama harakati za kifeministi zingefanya pupa kurudisha haraka sana idadi ya watu iliyopotezwa wa WGWD.

Kama harakati za wanawake, lengo letu kuu ni kupambana na ubaguzi unaotugawa ndani kwa ndani. Kama tutakuwa na ukweli katika utetezi wetu, inabidi tusiangalie ulemavu wanaoishi nao WWU ila tuzingatie vikwazo wanavyopitia na vinavyowafanya kuwa na uzoefu mgumu na kufanya watengwe.

Mfano wa kujumuisha WWU katika harakati za vyombo vikuu vya harakati za kifeministi ni jinsi ambavyo shirika la Urgent Action Fund-Afrika limehakikiisha kwamba limewajumuisha WWU katika mipango ya miradi yao. Mnamo mwaka wa 2019, nilipoalikwa kwenye uzinduzi wa jukwaa la Feminist Republik, nilieeleza kwamba ningehitaji kiti cha magurudumu na UAF-Afrika walinipatia gari jipya la walemavu. Hilo lilikuwa ni hitaji la kimsingi la kujumuishwa kwa walemavu, na liliondoa kikwazo ambacho kingenizuia nisishiriki vya kutosha.

Pia, nimealikwa kujiunga na bodi ya UAF-Afrika ili kuwakilisha maslahi ya WWU, kwa hiyo kwa sasa mimi ni mmoja wa wanachama wa halmashauri hiyo kutoa miongozo ya kimkakati ya kujumuisha masuala ya walemavu katika kazi zao. Hii ni hatua ambayo harakati zingine za wanawake wanaweza kuiga. Sisi wote ni wanawake, kwanza kabla ya ulemavu wetu, kwa hivyo, inabidi tujumuishwe katika shughuli na mipango iliyoundwa na vyombo vikuu vya harakati za wanawake.

Mshauriane na kuwaalika WWU kukaa mezani na nyinyi ili kushiriki mawazo, wakati wa kuunda, kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya miradi. Tafuteni ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya kuwajumuisha walemavu katika programu zenu zote, muunde na kutumia orodha ya ukaguzi wa masuala ya ulemavu katika katika miradi /shughuli zenu, na mwishowe huku tukiwa tumevalia kofia ya kifeministi, ni muhimu sana kuhakikisha ya kwamba pia tumevalia "lensi ya ulemavu", ili kuhakikisha hakuna dada mwenzetu yeyote anayeachwa nyuma.

Kwa kuendelea, ningependa kusisitiza ya kwamba upatikanaji wa hiyo nafasi ya kifeministi kwa Wanawake Wenye Ulemavu ni zaidi ya dhana ya nafasi dhahiri ya ufikiaji. Tunataka tushirikishwe katika kila mijadala ya kifeministi katika anuai yote ya mada za kifeministi; tunataka tuchangie na kuvuruga hali ya kutokuwepo na usawa na pia kubadilisha fikra. Dada zetu wawe wana ulemavu au hawana sote tunahitajiana. Tunahitaji kupata nguvu kutoka kwa uimara wetu katika mshikamano ili kuweza kusukumiza kuundwa kwa arakati jumuishi ya kifeministi ambayo ni salama kwa wote.

Hebu sasa tufurahie mtazamo wa kifeministi kuhusu ulemavu ambao uma ari ya kuangamiza kabisa vikwazo na kuunda nafasi za usawa ambazo zitajumuisha kila aina ya utofauti.



# UPONYAJI WA KIMAGEUZI NA UTUNZAJI WA KIBINAFSI KAMA VYOMBO VYA KUSAMBARATISHA MILA ZA KASUMBA ZA KUTOKUWA NA ULEMAVU

NA THATO MPHUTHI

Katika wakati wa mabadiliko makubwa, Mabadiliko yaliyotokea ambayo hayakutarajiwa, maisha yamekuwa magumu. Zaidi hasa kama ni mtu mwenye ulemavu. Ukiukaji wa haki za kibinadamu umetokea sana Afrika ya Kusini katika nyumba zetu, Shuleni, na katika maeneo mengine ya kijamii. Jamii zinazotuzunguka zinasauti za watu wachache wanaotambulika kuongelea watu wanaoishi na ulemavu. Upungufu mkubwa unaonekana pale unapolinganisha namba hiyo na ile ya wanayoengelea watu wasio na ulemavu.

Uhitaji wa wanaharakati na watetezi wanaowakilisha jamii ya watu wenye ulemavu haujawahi kuwa mkubwa. Kwa kulitambua hili na kujumlisha changamoto nilizokutana nazo katika nyakati ambazo niliamua kuamka, ilipelekea kuanzishwa kwa Enabled Enlightenment.

Sababu iliyopelekea jina hilo. Sikuwahi lipenda jina 'wenye ulemavu' niliona ni kama jina lililoweka ili kuweka mtazamo wa kuwanyima nguvu kundi Fulani la watu katika jamii. Kwa kuangalia jamii yangu ya Chiawelo, Soweto jijini Johannesburg, Neno hilo lilitumika na watu kuelezea hali yangu. Nilipatikana na maradhi ya kifua kikuu kwenye nyonga yangu ya upande wa kulia nilipokuwa mtoto na baadaye nikalazwa hospitalini ili niweze kufanyiwa upasuaji wa kutoa sampuli ya kupimwa maradhi. Kwa miaka mingi nimekuwa nikihamasisha na kwa wakati ule, nilishuhudia ubaguzi na udhalimu unaowapata watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Nilijifunza kuyashinda yote. Uzoena wangu ulinifundisha kuwa thabiti na kuyashinda magumu yote. Huu ndio ujasiri ambao Enabled Enlightenment unajumuisha ili kuvunja mila ambazo zinaendeleza ukandamizaji.

Kupitia taasisi yetu, maono yangu ni kuonesha wanaoishi na ulemavu ni Zaidi ya kitu kimoja wanachoshindwa kufanya. Mamlaka ya Enabled Enlightenment ni kuamsha wengine na kuonesha uwezo kwa hao wanaoitwa 'Walemavu' kuonesha dunia uwezo mkubwa walionao katika mambo mbalimbali. Tunatakiwa kutoa sauti zetu na kupinga uvunjwaji wa haki na ubaguzi ambao watu wenye ulemavu wanapitia. Sehemu kubwa ya kazi yangu na Enabled Enlightenment inalenga watoto. Naamini kufundisha watoto kuhusu haki zao na haki za wengine, kunaweza toa huu ubaguzi katika maisha ya mbeleni kama hii elimu itaanza mapema. Hii ndio inafanya mimi nivutiwe Zaidi. Nadhani ni muhimu tuelimishe watoto wetu kuhusu majukumu yao katika dunia ambayo wanajumuika na wengine. Kuwafundisha kuwa na mawazo chanya kuhusu miomgozo ya ukuaji ya miili na mawazo ya kidunia, bila kujali walipotokea na uzoefu wao.

Katika mpango wa Enabled Enlightenment watoto wanafundishwa kujieleza na kutoa sauti zao. Watoto wanapewa nafasi ambapo ya kujieleza hata kama itawafanya baadhi ya watu wazima kutokuwa na wasiwasi. Wanapewa nafasi kuonesha wanajali na kupewa elimu kuhusu maamuzi yao na athari ambazo zinaweza jitokeza katka mahusiano yao na watu wanaokutana nao katika dunia ambayo watu wanamawazo fofauti na kujiweza kitofauti. Kama watu watatambulishwa katika mafunzo haya wakiwa na umri mdogo, watakuwa wakielewa lazima kuweka kipaumbele kujali wenzao kiujumla na kama njia ya kuwa katika ustawi mzuri.

Watoto wenye ulemavu wanahaki katika mpamgo huu, kujua kwamba wanahaki zote kupewa nafasi ya kupewa faraja, furaha na kujaliwa. Kwa bahati mbaya hakuna majalada na nyaraka yanayoonesha njia za uponyaji na kujijalli binafsi, hasa njia zile zilizotumiwa na vizazi vya kiafrika. Hii imesababisha mara zote kutegemea haswa njia za watu wa magharibi lakini naamini kijijali binafsi ni kitu kinachoanzia na mama zetu, na mabibi zetu hata kama hakikuitwa kujijali binafsi.

Jambo la muhimu ni jinsi ya kuzitafuta hizi njia za mababu zetu na kuziandika katika nyaraka. Kufundisha kujiponya wenyewe na wengine katika njia ambazo zinatumia muktadha wetu. Na katika hiyohiyo, maandiko ya kutetea haki, uwezo na mahitaji ya watu wenye ulemavu yanatakiwa yaelezwe hadharani. Wakati ni sasa kuanza kufuta mila zinazoturudisha nyuma.




*"Kama jamii, na kama mashirika na wadau ambao wanaunga mkono harakati za haki za wanawake na uwezeshaji, kuna haja ya haraka kupata suluhisho tofauti za muda mrefu juu ya utunzaji wa pamoja kwa wanawake wetu na wasichana katika ngazi za mashinani .*

## AFYA YA KIAKILI KWA WANAWAKE KATIKA NGAZI ZA MASHINANI

AMISA RASHID.

Bado kuna kazi nyingi inayostahili kufanywa katika kuleta uelewa wa afya ya akili, zaidi ya hayo, kuna kazi inayostahili kufanywa kuhakikisha faida zake ni endelevu ikija kwa wanawake wenye umri mdogo, wasichana, na afya yao ya akili. Kazi yangu kama mwanasaikolijia wa ushauri nasaha katika Wakfu wa Nivishe, almaarufu Nivishe Foundation shirika ambalo linalenga kujenga ustahimilivu wa jamii kupitia programu zinazoshawishiwa na masuala ya afya ya kiakili na maoptio ya kiwewe ili kuendeleza mshikamano wa kijamii kwa jamii zilizotengwa na walio kwenye makaazi yasiyo rasmi, imeweza kuweka wazi jambo hili.

Kama sehemu ya juhudi zetu kuhakikisha kuwa tunajenga halaiki na jamii zinazotoa kipaumbele kwa uwepo mzuri wa ustawi wa kiakili wa watu binafsi katika jamii hizi ni kuandaa mazungumzo ya kila wiki kwenye redio kuhusu maswala ya afya ya kiakili na maswala mengine kuhusu jamii. Tunaifanya kazi hii kupitia radio za jamii, kwa kutumia lugha asili ya jamii husika, ili kuhakikisha kuwa ujumbe huu unasambazwa vyema na ya kwamba kuna uwepo wa ushiriki na uhusishaji rahisi wa wasikilizaji.

Katika mojawapo wa vipindi vyetu mapema mwaka huu, tulijadili swala la utunzaji wa kibinafsi kupitia upeo wa afya ya kiakili, na kule kuweza kurahisisha uelewa wa suala hili la utunzaji wa kibinafsi. Kwa muda mrefu, utunzaji wa kibinafsi umefahamika kuwa wa watu katika viwango fulani na kuhusishwa na watu wa matabaka maalum katika jamii kwani inadhaniwa kuwa ghali sana kwa wanawake wanaotoka katika maeneo ya kipato cha chini na hawawezi kumudu. Mmoja wa wasikilizaji wetu alipiga simu na kuuliza swali lililoibua tafakari ya kina sana. Alitaka kujua jinsi mtu angeweza kukidhi mahitaji yake ya kujitunza mwenyewe na wakati huo amekuwa akipambana na uzoefu wa hali moja ya kiwewe baada ya nyingine. Pia alitaja kuwa anajua kuhusu wanawake ambao wamepitia ukatili wa kijinsia, unyanyasaji wa kijinsia, kuvunjika kwa familia, na aina nyingine za madhara na dhuluma, na ambão wanashangaa ni vipi vitendo vya utunzaji wa kibinafsi vinaweza kufuta miaka hiyo mingi ya majeraha ambayo wamevumilia.

Huu ulikuwa ni wakati wangu wa kutafakari, na nilipokuwa nikimsikilia hisani na kumpa maoni na mitazamo yangu kulingana na uzoefu na maarifa yangu, nilikuwa napiga ubongo jinsi tunavyoweza kuunda harakati za utunzaji wa pamoja kwa jamii zetu katika ngazi za mashinani ambazo zinaweza kuleta uwezeshaji na hivi kwamba wanawake katika jamii hizi wangechukua hatua za kuzimiliki harakati hizo na kujiendeleza nazo. Pia, ni vipi kunaweza kuwa na uhamasishaji wa raslimali za kutosha kutoka kwa mashirika mbalimbali ya haki za wanawake ili kuhakikisha ya kwamba mipango kama hii ni endelevu na haitasitishwa kwa sababu ya ukosefu wa ufadhili na rasilimali?

Kwa kupitia kazi yangu katika mtaa wa Kibra nilipokuwa nikiwashirikisha wanawake na wasichana kutoka makaazi mengine yasiyokuwa rasmi na maeneo ya vijijini, nimechunguza na kuona mtindo ambapo vipindi vya buraha kama njia moja ya utunzaji wa kibinafsi hupangiwa wanawake ambao wanafanya kazi katika jamii hizo. Ni imani yangu kuwa vikao vingi kama hivyo vya buraha vinatakikana kuandaliwa kwani hawa wanawake wanastahili vikao hivyo na hata mengine mengi. Wasiwasi wangu tu ni kuwa hakuna mgao wenye usawa wa nafasi kama hizi. Mwaka nenda mwaka rudi, ni idadi ndogo tu ya wanawake wenye uwezo wa kufikia ambão watahudhuria vikao kama hivyo vya buraha, hali ambayo inaleta ugumu kukosa kufikiria kuhusu wanawake na wasichana ambao wana mahitaji makubwa sana ya msaada wa afya ya kiakili, ambão wanapambana na uchovu wa kimwili na kiakili, au ambão wamefika kwenye kingo za kuzama kwenye dhiki za afya ya kiakili na lakini hawko kwenye nafasi za kupata huduma hizi kwa sababu ya mgao usiokuwa sawa wa raslimali na nafasi.

Wasiwasi wangu mwingine tukija kwa upande wa utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa pamoja katika ngazi za mashinani ni kwamba inaonekana kama kuna njia moja pekee ambayo imebuniwa ya utunzaji wa kibinafsi, na ambayo ni buraha. Kama jamii, na kama mashirika na washikadau wanaounga mkono harakati za haki za wanawake na uwezeshaji wao, kuna haja kuu ya ya haraka ya kuzindua suluhisho mbalimbali za kudumu za utunzaji wa pamoja kwa wanawake na wasichana wetu katika ngazi za mashinani. Njia moja ya kufanya hivyo ni kwa kuunga mkono asasi za ya kijamii na mashirika yanayofanya kazi kushughulikia lengo hili, ambayo yataelekezea upatikanaji wa uponyaji wa pamoja hatimaye. Kwa kuongezea, wanawake wenye ulemavu sanasana husahaulika katika mipango kama hii, pamoja wa walezi wao. Mtu hawezi akapeana kutoka kwenye kikombe ambacho ni tupu.

Je, itakuwa vipi kama harakati za utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa pamoja zimeundwa ili kusaidia pia walezi wa wanawake wenye ulemavu? wanawake wengi watasaidiana wao wenyewe kwa wenyewe kwani vikombe vyao vitakuwa vimejaa na kufurika, jambo ambalo litapelekea kupambana na ukosefu wa haki za walemavu na pia kuleta udada unaotamaniwa sana na ambao sote tunajitahidi kufanya kazi ili kuufikia.

Kwa mujibu wa nyaraka zilizoko, kuna uhusiano kati ya magonjwa ya kiakili na hali ya wanawake kupitia matatizo ya kisaikolijia kama vile shida za kiuchumi, kupoteza na kufariki kwa wapendwa, kufariki kwa Watoto wachanga, kunyimwa mapenzi, kufanya kazi nyingi kuzidi kiasi, kupewa mshahara kiduchu, dhuluma za kijinsia na za kiuzazi. Wito wangu kwa washikadau wote wa haki za wanawake ni kuwa, ni jukumu gani tutakalochukua kuhakikisha kuwa hata kwa kadiri ambavyo tunashughulikia haki za wanawake na uwezeshaji, pia tunahakikisha ya kwamba ustawi wao wa kiakili nao unashughulikiwa kikamilifu.



## MWANAMKE MWENYE 'ULEMAVU'
## NA ELIZABETH NAMWANDI

Sasa ndiyo wakati
wa mwanamke mwenye ulemavu.
Sasa ndo wakati wetu kung'aa.

Tulidhulumiwa, tukasahaulika,
Na hakuna aliyetujali hata!
Tulibaguliwa,
Na kuachwa nyuma.

Mwanamke Kiziwi huna sauti ya kupiga kelele,
Walio na osari ya macho hawawezi kuona
mwenye ulemavu wa kimwili anakumbwa na mapungufu,
watu wanaoishi na uzeruzeru wanafanywa kama
wasiojulikana.

Ukatili wa kijinsia ulinuia kutuweka chini kwa mzigo,
Haki za binadamu zilitolewa kwetu sisi,
uhuru wetu wa kunena ukadhukumiwa

Ukosefu wa nafasi za ajira ni mzuka kwetu siku baada ya
siku,
na sisi tumekuwa waasiriwa wa umaskini.
Majina mabaya yamekuwa mkate wetu wa kila siku.
Hakuna anayeweza kukubali ulemavu wetu,
ndo kwa sababu tumedhalilishwa leo.

Dzuwa II, Juni 2021

# Jinsi Ambavyo Ubaguzi Dhidi Ya Wanawake Wenye Ulemavu Katika Michezo Unatuumiza Sote

NA PALESA MANALENG

"Kuna nini na kofia yako ya chuma?" Ninatazama juu na kupata mzee ambaye lazima alikuwa akiendesha baiskeli juu ya kilima nyuma yangu.

"Aargh, ninahitaji mpya tu," ninasema ninapogusa kofia ya chuma iliyounganishwa-unganishwa pamoja na mkanda wa gundi. Ninahitaji pia basikeli mpya ya kuendeshwa kwa mikono na ufadhili ili kwenda kuwakilisha Afrika Kusini kwenye Mashindano yajayo ya Dunia, lakini simtajii hili.

Kuwa mwanariadha mlemavu wa nchi ya Afrika Kusini ni kama kuwa katika uhusiano uliojaa dhuluma. Wewe huendelea kurudi tu kwa huyo mpenzi bila kujali ni mara ngapi anakugonga na kukuangusha. Na tunafanya hivyo kwa sababu michezo ni uhuru wetu, shauku yetu, na tunanawiri katika michezo hiyo.

Nimechaguliwa kuwakilisha nchi kwenye mashindano matatu ya kimataifa, moja ambayo ni Mashindano ya Dunia lakini ni ya kujigharamia mwenyewe. Ninaamka kila asubuhi na kupanga ratiba yangu ya mafunzo nikitumaini mtu atajibu barua pepe zangu kuhusu ufadhili. "Imara, thabiti, jizatiti msichana, usikate tamaa juu yangu," nilimnong'oneza Bi Billie Holiday, baisikeli yangu ya kuendeshwa kwa mikono, wakati wa vipindi vya mazoezi.

Yeye ni mzee na amepitwa na wakati lakini hatutengenezi vifaa vya baiskeli za spoti ya walemavu nchini Afrika Kusini, jambo ambalo pia linamaanisha kuwa hatuwezi kuendeleza mchezo huo katika vitongoji vya miji midogo au maeneo ya vijijini. Baisikeli mpya kabisa ya kuendeshwa kwa mikono ikinunuliwa bila vipuri hugharimu takriban R86 000 (kama dola 6,000), ambayo inamaanisha watoto wengi wametengwa kwenye mchezo huo.

Ikiwa familia inapaswa kuchagua kati ya chakula, malazi, kutunza mahitaji ya matibabu, na kununua baiskikeli ya kuendeshwa kwa mikono ili mtoto aweze kushiriki katika michezo, chaguo bila shaka ni dhahiri.

Nimekuwa na Bi Billie Holliday tangu 2015 shukrani kwa mdhamini na tumeshiriki mashindano mengi sana ikiwa ni pamoja na kuendesha baiskeli kutoka Pretoria hadi Cape Town kwa kipindi cha siku kumi.

Kwa miaka kadhaa iliyopita, kiwango changu cha kimataifa kimetoka nambari 8 duniani, hadi sasa, 22, kwa sababu ninatatizika kumudu kushiriki kwa mashindano ya kimataifa. Mtu angefikiria kuwa utendaji ungekuwa sawa na thamani ya kibiashara kwa mdhamini, lakini inaonekana kwamba hali siyo hivyo kwa wanariadha wenye ulemavu.
Bingwa wa tenisi ya magurudumu wa Afrika Kusini aliyeiwakilisha nchi hiyo kwa miaka kwa kiwango cha kimataifa bila udhamini lakini kwa msaada wa shirikisho la kitaifa, Tennis South Africa. Wakati shirikisho la tenisi halikuweza kumsaidia tena kwenda kwenye

mashindano, Montjane ilibidi atafute jinsi ya kufika kwenye mashindano peke yake mwenyewe. Na hakuweza kumlipa kocha wake tena, lakini aliendelea kumfundisha. Ilikuwa mnamo 2018, wakati alipewa nafasi ya kubahatisha kushiriki katika mashindano makubwa ya Wimbledon, alichukua pesa kidogo aliyokuwa nayo na kwenda kushindana peke yake kwenye mashindano n ani baada yah apo ndipo nchi ya Afrika Kusini ilianza kutambua kuwepo kwake.

Alikuwa Wimbledon bila kocha kwa sababu hakuwa na uwezo wa kumlipia ili kuandamana naye. Montjane alikuwa mwanamke wa kwanza wa Kiafrika, asiye na ulemavu au mlemavu kushindana, huko Wimbledon, na hakuwa na msaada wowote.

Kwa kweli, alikuwa tayari yuko njiani anarudi kutoka kwenye mashindano kabla ya watu kuanza kumzingatia na vyomba vya Habari vilianza kumuangazia kila mara. Rais Cyril Ramaphosa aliandika kumhusu kupitia mtandao wa Tweeter hata ingawa hakuwa amepata msaada wowote wa kifedha kutoka kwa Wizara ya Michezo, licha ya kuwa mwanariadha bora.

Kelele kufuatia kurudi kwake na mfululizo wa ziara za waandishi wa habari zilisababisha Mkurugenzi Mtendaji wa wakala wa uuzaji wa Afrika Kusini, Optimize, kumchukua Montjane chini ya mabawa yake. Kwa hivyo, kusaidia kupata udhamini kutoka kwa kampuni kumi ikiwa ni pamoja na Nike, Discovery, na udhamini wa vifaa kutoka Macsteel.

"Daima nimeweka juhudi 100% katika mchezo wangu. Ninafanya mafunzo kwa bidii na kufanya mazoezi kwa bidii, sababu pekee ya kutofautisha imekuwa kiti changu cha magurudumu. Wapinzani wangu siku zote wameweza kugeuka kwa upesi na kuzunguka hap ana pale kwenye uwanja haraka zaidi," alisema mwanariadha huyo wakati akipokea kiti chake cha magurudumu kipya kabisa cha tenisi.


Je! Wanariadha walemavu wenye vipaji vya juu wanapaswa kusubiri hadi waandike historia kabla ya kupata kutambuliwa wanavyostahili? Je! Wanapaswa kulazimika kutegemea wakati huo mmoja wa kufanya historia ili kuepukana na ubaguzi katika michezo?

Wanariadha wenye ulemavu huweka juhudi sawa katika michezo yao na hufaulu na msaada mdogo au hata bila msaada kabisa. Walakini, inaonekana kuwa hiyo haitoshi kwa wao kufanikiwa kupata begi na kujikimu kutokana na talanta zao.



# Kutambua Kuweweseka ambako Vizazi Vinapitia Na Kusherehekea Uthabiti wa Vizazi na Nguvu za Uponyaji ulio kwenye Maarifa Asili

NA BEAUTY BOOIS



Kufuta historia, utamaduni na desturi na hata lugha ya Watu Waafrika Wenye Ngozi Nyeusi wenye milengo ya kikuchu na wale wanovutiwa na jinsia nyingine, almaarufu Queer and Heterosexual Black African People (QHBAP) imetupora urithi wetu na zaidi kutunyima haki kama binadamu. Mifumo ya kikoloni, ubaguzi na mifumo dume iliundwa katika namna ambayo mpaka sasa urithi wake unaathiri zaidi jamii iliyotengwa. Kunyimwa haki huku kunatokea katika njia tofauti tofauti: Baadhi zinanyanyasa zaidi na kubagua na zingine zimewekwa kimfumo kupitia sheria na sera. Huku kunyimwa haki kunaleta udhaifu wa kiakili, kihisia, kimwili na kiroho katika maisha ya watu. Ukoloni huu wa kiakili unaonekana kupitia maswala ya kijinsia, ubaguzi wa rangi, kiuwezo na unyanyasaji. Ni dhahiri kuwa watu wanaotengwa ndivyo wanavyohisi ama kuamini kuhusu wenyewe, kulingana na ufundishaji wetu katika mifumo kandamizi ambayo tunayo. Ukoloni wa kiakili unatawala akili zetu, mawazo yetu na thamani na kujiamini na watu wengine ambao wananyimwa haki kama sisi. Hii inajionesha katika mahusiano na haki za kibinadamu. Hatujumuishwi katika haki zetu na usawa kama wanawake, jinsia kinzani, transijenda wanawake, na kama watu wenye ulemavu. Kama hatuelewi tunaishi na mifumo kandamizi na isiyotenda haki hii inatufanya tukubali baadhi ya watu wana haki zaidi na wanatakiwa watendewe ubinadamu zaidi.



Nyenzo za ukoloni wa kiakili zinapatikana kila mahali – katika mitaala yetu ya elimu, katika vitabu vyetu vya historia, vyombo vya habari na fasihi. Nyenzo hizi zinatulisha na mawazo fulani ambayo yanalenga kutufanya kuwa watumwa wa kimawazo. Mfano, tukiangalia vyombo vya habari huwa vinazingatia kwa kimfumko mazoea ya makuchu kama kiwewe – uenezaji wa mambo ya kimapenzi machafu huku kukiwa na picha zisizohesabika na masimulizi mengi kuhusu mazoefu ya kiwewe ambayo yamepitiwa na Watu Waafrika Wenye Ngozi Nyeusi wenye milengo ya kikuchu na wale wanovutiwa na jinsia nyingine. Hayo, pamoja na kasumba za kimfumo zilizokithiri kuhusu QHBAP ambazo huongezea maradufu taswira hasi walizo nazo kujihusu, kujiona kama hawana thamani, kukosa ujasiri au kujiamini, na hata pia kuna uwezekano wa kujichukia wenyewe

Ni Muhimu kukubali matukio ya kusikitisha ambayo QHBAP wanapitia katika mifumo yenye ukadhamizaji. Kuweka vipaumbele sawa katika kuangazia uthabiti, ujasiri, uwezo wa kushamiri, kuinuana kifalsafa na kujijali na njia za kujiponya ambazo QHBAP wanatumia. Jinsi gani njia hizi zinatuhamasisha sisi sote kukuza uzoefu wetu. Kuna mengi ya kujifunza kutoka katika uzoefu wa QHBAP na kuuiga katika jamii zetu. Fikiri kuwa upo katika ulimwengu ambapo wanabadilishana picha, jumbe, historia na taarifa kuhusu uzuri na ushindi wa QHBAP.

Steve Biko katika kitabu chake mashuhuri, Nitaandika Kinahonivutia, anaandika kuhusu nguvu ya ufahamu wa watu weusi na kuweka maelezo kama "Silaha kubwa aliyoko nayo mkandamizaji ni akili ya anayemkandamiza." Watu ambao wamepitia ukandamizaji wakibadili mawazo yao katika vitu vyenye ubora kwao, uwezo wao wa kuhimili na kustawi hata katika magumu wanayopitia, kutambua ubinadamu wao, huruma yao, na uwezo wa kuishi kwa usawa kupitia nguvu za mababu zao, huwa wanapata ujasiri wa kuyakomboa mawazo yao na maisha yao kupitia kujitambua na kuwezeshwa kibinafsi. Kuna uponyaji mkubwa katika kukumbuka wale wote wale waliokuwepo kabla yetu na wale amabo tunaishi nao sasa. Tunapoeleza hadithi zao, tunaongelea matumaini yao, jitihada zao, na kufurahia mafanikio yao na hatua za kupata haki katika jamii, tunaanza na hatua ya kutambua ubora wetu, ushujaa, uthabiti na uimara ulioko ndani yetu..

Uelewa kuhusu mambo ya kiasili au kama ambavyo mchambuzi wa masuala ya kijamii anavyosema katika kitabu chake, cha Ujuzi wa Kihisia ''Ujuzi ambao unaipa akili na mwili uhai, unaacha matokeo kama vile harufu ya marashi mazuri.'' Ni kuzaliwa upya. Mfumo wa kutenga umewekewa misingi katika tamaduni na mila za jamii yetu. Ni kupitia uelewa wa wa mambo ya asili ndipo watu wa Afrika watafahamu uponyaji kupitia nguvu ya kucheza ngoma, umuhimu wa historia kupitia kusimuliwa kama hadithi, nguvu ya matambiko, umuhimu wa sanaa na ubunifu wa kujieleza, na nafasi ya ulazima ambayo asili imechukua katika maisha yetu. Uelewa wa asili unachochea kujitegemea kwetu, uthabiti wetu, uimara wetu na umihimu wetu. Ni uponyaji, unaleta urejesho, unaleta uwezo, unaleta usawa, na unatia nguvu kiakili, kihisia, na kiroho. Unatuunganisha na mizimu ya mababu zetu na kutupa kujiamini sisi ni kina nani na tumetokea wapi. Inakubali kuwa mababu zetu walitupatia mwongozo wa njia ya uhuru na uponyaji kwetu na vizazi vyetu vijavyo.






# KUFIKIA KAULI YA PAMOJA YA UPONYAJI

NA MELISSA WAINAINA

Jukwaa la Feminist Republik

Tumeingia 2021, zaidi ya mwaka mmoja tangu kuzuka kwa janga, tukishughulikia COVID-19 na shida ambazo imeleta katika maisha yetu. Ni ngumu kukosa kuona matabaka mbalimbali ya ukandamizaji na jinsi jamii ilivyowashughulikia wale miongoni mwake walio hatarini zaidi.

Ubaguzi katika makutano kati ya jinsia na ulemavu haujawahi kudhihirika zaidi, lakini maswala ambayo yanaathiri maisha ya watu ambao ni wanawake, wabadilijinsia, na watu wasioambatana na jinsia yoyote wenye ulemavu ulitangulia janga hilo ambalo limezidisha tu ubaguzi huo. Matatizo ya kiuchumi, kutengwa kijamii, kujitenga kimwili kwa umbali wa kijamii, na maagizo mengine ya kukaa nyumbani yanayosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona yameongezea tu mapungufu ambayo tayari yapo. Watu wengi zaidi wenye ulemavu wanakabiliwa na umasikini, kukosa makao kabisa au kuishi kwenye nyumba duni, upungufu wa kazi, na kuharamishwa.

Watetezi wa haki za watu wenye ulemavu wamekuwa wakishiriki jinsi ambavyo unyanyapaa wa walemavu, kasumba ya wanaojiweza, ukosefu wa usawa, na ubaguzi ulivyo kithiri kwa miaka. Imekita mizizi ndani ya taasisi na miundo yetu. Kusikitisha zaidi, inajitokeza na inaingiliana na mifumo mingine ya kutovumiliwa, ya ujinsia, na ya unyonyaji.


Tunahitaji kushughulikia urithi usiofaa usio wa haki wa ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu. Hii ni fursa muhimu ya kufanya mtazamo wetu uwe wa kutoa kipaumbele kwa ubinadamu na kupinga sera za kibaguzi, mazoea, na ukiukaji wa kimfumo wa haki za watu wenye ulemavu.

Jukwaa la Feminist Republik lilianza shughuli zake katika kilele cha janga hilo mnamo 2020. Tulijitahidi kufanya maboresho ili kuhakikisha ujumuishaji zaidi, ufikiaji zaidi, na ushiriki zaidi katika hatua zetu zote. Ulimwengu ulipoelekea kusimama, tulipata njia mpya bunifu za kuunganisha kimkondo kupitia Mikutano ya Uponyaji ya Ubuntu, almaarufu Ubuntu Healing Gatherings. Mikusanyiko hii ilianzisha hali ya unyumbufu na ubunifu ambao ulituwezesha kuwa katika jamii na kila mmoja. Vipindi vyetu viliundwa ili kuwezesha kuwepo na chaguzi mbalimbali tofauti za kutafsiri, ikiwa ni pamoja na Lugha ya Ishara na maelezo mafupi yaliyofungwa pale ilipowezekana. Tunazidi kukuza ujuzi wetu na rasilimali zetu ili kupanua mikutano na njia za mawasiliano ambazo zinajumuisha mahitaji yetu yote.

Huku likidhibitiwa na uongozi na ufahamu wa wanawake wanachama wa harakati wa haki za walemavu, Jukwaa hili linaendelea kwenye njia ya kazi yake ya ubunifu ili kuchunguza jinsi ya kukita mizizi ya utunzaji wa kimageuzi wa watu wenyewe binafsi na wa pamoja katika maisha yetu ya kibinafsi na harakati zetu. Michango na ubunifu kutoka kwa mitungo ya ngonjera, nakala za blogi, na sanaa ya kuona kutoka kwa wanaharakati wa haki za walemavu, wafeministi, wasanii, wawezeshaji, walimu, na wabunifu katika hafla zetu zote na machapisho yamekuwa ya nguvu na yenye utajiri. Wamefanya iwezekane kuleta pamoja uzoefu kamili na wa pande nyingi miongoni mwa wafeministi na wanaharakati kufikiria, kujifunza, na kushiriki zaidi juu ya mitazamo ya kujumuisha bara zima la Afrika kuhusu uponyaji haki. Tunapoendelea na uwezekano mpya unaojitokeza, tunaongeza msaada wetu kuelekea juhudi zinazopigania haki ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi, haswa kwa vikundi vya haki za binadamu vya wanawake ambavyo mara nyingi hutengwa. Hii ni njia moja ambapo tunalea tamaduni za utunzaji ndani kwa ndani na kwa upana wa harakati zetu zote.

Sio tofauti na Mfuko wa UAF-Afrika katika wito wa maombi yake yote ya ruzuku. Tunatoa mshikamano na msaada kwa wanawake, watu wanaobadilisha jinsia, na watu wasio tambua jinsia wenye ulemavu. Tunafanya kazi na wanaharakati wa haki za ulemavu kusaidia hatua na hali za dharura huku tukishughulikia mahitaji yao ya afya, ustawi, usalama, na uponyaji.
Mnamo mwaka wa 2020 katika kilele cha mkurupuko wa COVID-19, UAF-Afrika iliunga mkono zaidi vikundi 25 vya haki ya wanawake wenye ulemavu katika nchi za Kamerun, Burundi, Zimbabwe, Kenya, Nigeria, Tanzania, Sierra Leone, Uganda, Senegal, na Rwanda kwa majibu rahisi, ya haraka kufikia ufadhili wa jumla ya $ 154,000.

Kazi nyingi muhimu ziliunga mkono juhudi za kuwapa wanawake wenye ulemavu habari muhimu juu ya ulinzi na kujibu COVID-19. Kiwango fulani cha ufadhili huo kilitoa habari za kutosha kwa wanawake wenye ulemavu wa kusikia ambao wameachwa nje kabisa katika utoaji wa ujumbe wa afya ya umma na kuwawezesha kupata habari muhimu na mapendekezo ili kuepusha hatari na kupunguza kuenea. Rasilimali zingine ziliweza kusaidia kikundi kinachozalisha jumbe zinazohusiana na COVID kwenye vifaa vya kuchapisha herufi za braille na vifaa vya kuona ili kupanua ufikiaji wa wanawake wengine zaidi ili kuwwawezesha kufanya maamuzi sahihi wanapopambana na janga hilo.



Kando na janga hilo, fedha pia ziliwasaidia wanawake wa umri mdogo wenye ulemavu wanaotaka kuingia katika siasa na kugombea ofisi. Wanawake katika michakato ya kuchagua na kufanya maamuzi bado ni nadra kuliko kuwa kawaida, hata zaidi kwa wanawake wenye ulemavu. Ili kuhakikisha ya kwamba hakuna mtu atakayeachwa nyuma, ni muhimu kubadilisha hali ilivyo - ambayo inawafanya wanawake wenye ulemavu wakiwa na uwakilishi wa chini sana katika ngazi zote za maamuzi. Ni kutoa michango ya aina hii ndiko ambako kunaongezea hali ya mabadiliko ya kimageuzi.

Kuna njia nyingi sana watetezi wa Kiafrika wenye ulemavu wanapambana na kutokuwepo kwa usawa katika miundo na mifumo ya uwezo. Urgent Action Fund – Afrika bado imejitolea kuunga mkono juhudi za haraka za kuendeleza usawa na ujumuishaji.
Kuhakikisha kwamba ahadi hii inatimizwa, mnamo 2021, UAF-Afrika ilizindua wito wa maombi ya ruzuku inayozingatia haki ya ulemavu kwa wanawake wa Kiafrika katika janga la ulimwengu.
Unaweza kupata kiunga cha maombi ya ruzuku hapa.

(https://www.uaf-africa.org/wp-content/uploads/2021/03/2021_COVID-19-disability-Justice.docx)

Inatoa njia za kushughulikia maswala ya haki za kiuchumi kama kazi ya huduma isiyolipiwa, kupungua au kupoteza kwa vitega uchumi, kudai kwa mpango wa kufufua uchumi wa baada ya COVID-19 ambao unajumuisha masuala ambayo wanawake wenye ulemavu wanakumbana nayo, na kadhalika. Pia inakaribisha mapendekezo ya kutaka kukuza afya ya ngono na uzazi na haki na uhuru wa kimwili kwa wanawake wenye ulemavu, iwe ni kampeni za utetezi au shughuli za kukuza uelewa ili kutoa huduma kamili na za kutosha. Maarifa ni zana yenye nguvu ya kisiasa kusaidia kushiriki uzoefu halisia na kujumuisha ushahidi ili kushinikiza mabadiliko. Utoaji huu wa ufadhili pia unasaidia mapendekezo yanayonuia kuundwa kwa nyaraka za kuorodheshwa kwa athari za COVID-19 kwa wanawake wenye ulemavu ili kuongezea Zaidi juhudi za utetezi na kujulikana.

Mwishowe, wito huu wa ruzuku ni wa makusudi katika kuhakikisha inasaidia juhudi za kukuza utunzaji wa kibinafsi na wa pamoja haswa kwa wale walio katika maeneo hatarishi na yenye migogoro barani Afrika.

***Tunahitaji kushughulikia urithi usi wa haki wa ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu.***

**"Kujijengea kuelekea mfumo wa kisheria, sera na mifumo ya taasisi inayojumuisha walemavu na kuzingatia ujinsia ambayo inatoa haki kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu nchini Zimbabwe –**

Safari Ilipofikia Kwa Sasa"- na ICODZIM

Kuhakikisha ujumuishaji wa walemavu ni kazi kubwa ambayo inahitaji ushirikiano na kujitolea kwa wadau wote ikiwa tutafikia lengo la ushiriki mzuri wenye maana na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika nyanja zote za kijamii, kiraia, kiuchumi, kisiasa, na kitamaduni kama inavyotarajiwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu, almaarufu United Nations Convention on the Rights of Persons with Disabilities (UNCRPD).

Ni jambo la kusikitisha sana ya kwamba katika nchi ya Zimbabwe ujanibishaji kamili wa UNCRPD unaendelea kuanguka kupitia nyufa za hatua za kimaendeleo. Taasisi ya Maendeleo ya Jamii nchini Zimbabwe Institute for Community Development in Zimbabwe (ICODZIM), ni shirika linaloongozwa na wanawake, ambalo linaendeleza haki za wanawake wenye ulemavu bila kuzingatia migawanyiko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Tangu ianzishwe mnamo mwaka wa 2015, ICODZIM inaendelea kuchukua jukumu la kushughulikia kutengwa kwa Wanawake Wenye Ulemavu (WWU) na kwa wakati huo huo likiendelea na juhudi za kudumisha kutambuliwa kwa haki za walemavu na washika majukumu na amii kwa ujumla.

Sehemu ya ahadi hii ni kunuia kuendeleza mfumo wezeshi wa kisheria, kisera, na kitaasisi kwa utekelezwaji na kufurahiya kwa haki na watu wenye ulemavu nchini Zimbabwe. ICODZIM inaamini kuwa wakati huu ni mwafaka kwa Zimbabwe kukubali kikamilifu njia inayotegemea haki za binadamu kwa ulemavu. Kama ICODZIM, tunaisherehekea UNCRPD kama kigingi muhimu kikubwa katika safari ya mapambano ya kurekebisha mahitaji na wasiwasi wa Watu Wenye Ulemavu (WWU) kuhusu haki zao. Inajumuisha mabadiliko ya dhana kutoka kwa mwitikio wa kihisani kwa ustawi wa jamii kwenye mipango wa watu wenye ulemavu hadi kufikia mwelekeo unaotegemea haki za binadamu. Kwa hivyo, ni muhimu sana bila kusita kwa Zimbabwe kutekeleza kikamilifu UNCRPD kulingana na Ajenda ya 2030 ya kutokuacha mtu yeyote nyuma.

## “Kujijengea kuelekea mfumo wa kisheria, sera na mifumo ya taasisi inayojumuisha walemavu na kuzingatia ujinsia ambayo inatoa haki kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu nchini Zimbabwe – Safari Ilipofikia Kwa Sasa”- na ICODZIM

Katika makala haya, ICODZIM inashiriki hatua muhimu zilizopatikana kufikia sasa katika kuendeleza sheria za ujumuishaji wa walemavu na uzingatiaji wa ujinsia kwenye mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi hali ambayo inatoa haki kwa WWU. Mnamo mwaka wa 2019, ICODZIM ililalamikia Bunge la Zimbabwe, ikidai kujanibishwa kwa UNCRPD. Hii ilikuwa baada ya kugundua ukosefu wa mfumo wezeshi wa kisheria na wa taasisi kufanikisha vifungu vilivyowekwa katika UNCRPD. Kwa matokeo, kamati ya bunge ya mada juu ya haki za binadamu imepitisha mapendekezo yaliyotolewa na kutaka ujanibishaji wa haraka wa UNCRPD nchini Zimbabwe. Ilipendekezwa pia kwamba nchi inapaswa kuunda sera mpya ya kitaifa juu ya ulemavu ambayo inachukua mtazamo wa haki za binadamu. Kitendo hiki kimeisababisha ICODZIM kuhitimu kuwa mwanachama wa kikundi cha mada kinachofanyia kazi mchakato wa ujanibishaji UNCRPD; fursa ya kuendelea kushawishi na kutetea ujanibishaji kamilifu wa UNCRPD. Moja ya sababu kuu za mtazamo wa ulemavu kukosekana katika mageuzi ya katiba ambayo yaligunduliwa na ICODZIM ni ukosefu wa ushiriki kamili na ushirikishwaji wa maana wa WWU katika mchakato wa kutengeneza katiba kwa sababu ya ukosefu wa taarifa katika fomati zinazoweza kutumiwa na walemavu na vile vile uelewa mdogo wa michakato ya katiba.

Hii imekuwa ikichangia kutengwa kwa WWU katika michakato anuwai ya mabadiliko ya katiba iliyofanywa nchini Zimbabwe. Kwa msaada kutoka kwa UAF-Afrika, ICODZIM iko tayari kuishughulikia na kuondoa changamoto hii wakati wa mchakato wa Muswada wa Marekebisho ya Katiba ya awamu ya 2 kupitia usambazaji wa habari inayopatikana ya walemavu juu ya Muswada wa 2 na uhamasishaji wa WWU kushiriki kikamilifu na kuzipaza sauti zao wakati wa mchakato huo. Hii haikuleta tu ushiriki ulioboreshwa wa WWU katika mchakato wa urekebishaji wa katiba katika ngazi zote lakini pia ilihakikisha kuongezeka kwa uthamini na uelewa wa masuala ya ulemavu na jinsia na watunga sera na washikaji wa majukumu haswa wabunge. Ufuatiliaji wa nakala za mijadala ya bunge almaarufu hansard na ICODZIM imethibitisha kuongezeka kwa hamu ya kushinikiza maswala ya ulemavu na wabunge ambao wamefikiwa.

Upatikanaji wa haki unahusisha gharama, na kufanya kazi ya shirika kuunganishwa kwa karibu na michakato ya bajeti ya kitaifa. Mnamo mwaka wa 2020, ICODZIM iliunda Wasilisho la Vipengee Kumi la Vipaumbele vya Mpango wa Ulemavu wa kwa bajeti ya kitaifa ya 2021 ambayo imesababisha mabadiliko ya juu ya 4.9% katika mgao wa fedha kwa afya na kuletwa kwa laini mpya ya bajeti inayojisimamia ya kusaidia WWU. Ili kuhakikisha kuwa bajeti ya 2021 inatekelezwa kwa utoaji wa huduma, shirika limeanzisha Mfano wa Roboti ya Fedha; mfumo unaotumika kwa sasa kufuatilia utekelezaji wa vipaumbele vya walemavu vinavyozingatiwa katika bajeti ya kitaifa ya 2021. WWU wameathiriwa pakubwa sana kuliko wengine wote wakati wa COVID-19 kwa hivyo hitaji la kuwapa kipaumbele katika mgawanyo wa rasilimali kwa urejesho endelevu baada ya COVID-19. Ulimwenguni kote, upatikanaji wa haki kwa WWU, haswa waathirika wa Ukatili wa Kijinsia (GBV), umekuwa ndiyo hali ya mipango ya kawaida; viwango vya kuigwa na mazoezi bora ya ujumuishaji wa walemavu. Kwa sababu ya ukweli huu, ICODZIM imeendesha mashindano ya kwanza kabisa ya kitaifa mahakama ya kuigiza juu ya haki za walemavu kwa kushirikiana na shule za sheria za vyuo vikuu nchini Zimbabwe. Mashindano haya yalilenga kuendeleza ufikiaji wa haki ya Afya ya Kijinsia na Uzazi (SRH) kwa WWU na kuunda mazingira wezeshi ambayo yanahakikisha utekelezwaji wa haki na WWU. Kwa maoni yetu, mpango huu unachangia kurekebisha ukosefu wa usawa uliopo katika jamii yetu. Hii pia inatoa wito kwa hatua za pamoja kati ya serikali, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia, na jamii kwa jumla kugeuza hali hii ilivyo. Kama ICODZIM tunasema ulemavu ni uzoefu wa ulimwengu kwa wanadamu. Inapaswa kujumuishwa katika michakato yote ya maendeleo ya kisiasa na kijamii na kiuchumi.

## Kupanda Mbegu ya Ufahamu wa Jamii, Uponyaji na Mabadiliko: Shamba la Uponyaji la jukwaa la Feminist Republik

### Na shirika la Feminist Republik – Usasishaji kutoka kwa kamati ya Waajiriwa

Jukwaa la Feminist Republik limekuwa likichunguza ni mifumo gani ya msaada ya Wanawake ambao ni Watetezi wa Haki za Binadamu wa Afrika almaarufu African Womn Human Rights Defenders (AWHRD) wanahitaji kukuza kikamilifu usalama, usalama, ustawi, na utunzaji wa pamoja katika ya maisha yao, mashirika, harakati, na miundo mbalimbali.

Kwa kuzingatia hili, tumefanya juhudi kuanzisha Shamba la Uponyaji kama mradi wa urithi. Maono yetu ni kuwa na usemi thabiti wa ndoto ya Jukwaa kutoa kwa wanachama wa AWHRD nafasi ya kujiponya, kuungana na miili yetu katika anuai zao zote za miundo na hali halisia, na kila mmoja, na kuweza kuzifufua nguvu zetu zinazoendelea kupungua.

Tunayo furaha kuwajulisheni ya kwamba hamu hii ilianza kujitokeza wakati tulimalizia ununuzi wa sehemu ya ardhi ili kuandaa maono yetu katika eneo la Mashariki mwa Kenya mnamo Januari 2021! Safari ambayo ilituongoza kufikia hapa ilikuwa ndefu lakini yenye manufaa, ikijumuisha ushiriki na usimamizi wa wataalam huru wasio waajiriwa na AWHRD. Walitekeleza jukumu muhimu katika kuchagua kipande cha ardhi kinachofaa zaidi kwa mradi huu wa fahari. Sisi kwenye Jukwaa tunashikilia kanuni ya uongozi wa pamoja. Hili linadhihirika katika kazi yetu ya kushirikiana na AWHRD na vile vile mbinu tunazotumia katika kazi zote tunazozifanya. Sisi kila wakati tunatafuta njia za kuhakikisha kuwa AWHRD wako mstari wa mbele katika kuunda na kuelezea aina ya msaada wanaouhitaji katika kuweka kipaumbele kwa uponyaji wa kibinafsi na ule wa pamoja katika kujenga asasi na harakati.

Ardhi yenyewe ambayo ni jumla ya ekari 13.6 iko katika eneo la Muselele, kaunti ya Kitui nchini Kenya. Mwanzoni mwa Machi 2021, wawakilishi wa Kamati ya Wafanyakazi ya Shamba la Uponyaji na wajumbe wa Bodi ya UAF-Afrika walipata fursa ya kutembelea ardhi hiyo liyonunuliwa. Walikuwa na bahati sana ya kukutana na kuungana na wamiliki wa zamani wa ardhi hiyo, ambao walielezea timu hiyo kuhusu historia ya ardhi hiyo. Masimulizi haya ni kumbukumbu za historia tunatarajia kuweka pamoja tunaposhiriki safari yetu pamoja.

Tunaamini kwamba Shamba la Uponyaji linatoa njia kwa AWHRDs kupata uwiano na dunia. Shamba hili la uponyaji la aina ya kipekee litakuwa nafasi ambapo tutawasiliana na anga, maji, na ardhi, tukilijumuisha hili na miili yetu, akili, na roho zetu kama jamii. Tunalichukulia Shamba la Uponyaji kama kiumbe kilicho na hai na kinachopumua na ambacho kinapanda mbegu ikipandikiza tena ufahamu wetu na midundo ya maumbile ambayo hutufanya upya na kutulea.



**“Tunaamini kwamba Shamba la Uponyaji linatoa njia kwa AWHRDs kupata uwiano na dunia. Shamba hili la uponyaji la aina ya kipekee litakuwa nafasi ambapo tutawasiliana na anga, maji, na ardhi, tukilijumuisha hili na miili yetu, akili, na roho zetu kama jamii. “**

Mradi huu wa urithi una lengo mahsusi la kuchochea moto wa utamaduni wa utunzaji na unatoa uwezekano wa kukumbana na uzoefu asilia wa Kiafrika wenye chimbuko la utunzaji wa kimageuzi na jibu la kifeministi kwa changamoto zetu za kijamii na kiuchumi, kisiasa, na kiikolojia za wakati wetu.

Kwa hivyo, tunapojaribu kutafakari jinsi ulimwengu utaweza kuonekana baada ya janga la COVID, tunaota hali halisia mpya ya kustawi ambapo miili yetu yote, maeneo yetu yote, akili, roho zinathaminiwa na kusherehekewa katika utofauti wetu. Tunatia kipaumbele mahitaji yetu ya afya na ustawi kama watetezi wa haki.

Adui wetu wa Pamoja mkubwa sana ni kujitenga, kwani kunatuzuia kutoka kwa kuwa pamoja ili kupata haki, uhuru, raha, na furaha. Tunatumai tunaweza kupata msingi wa pamoja unaohitajika kutuwezesha kuweka umuhimu mkubwa katika utunzaji wa kimabadiliko, uponyaji, afya, na ustawi kwa kila mmoja na wote. Matumaini yetu ni kwamba Shamba la Uponyaji litaweza kutimiza hili na mengine mengi zaidi.

Udhihirisho wa mafanikio wa kazi hii unaweza kuonekana tu ikiwa kazi hii imeundwa kwa pamoja. Tungependa kusikia kutoka kwako kuhusu ndoto yako na maono yako kuhusu ni nini nafasi hii inaweza kufanya ili kuwasaidia AWHRD katika safari zao za utunzaji wa kibinafsi na wa pamoja. Tafadhali shiriki mapendekezo na maoni yako. Tunayathamini yote!
Dondosha barua pepe kwa feministrepublik@uaf-africa.org na uandike kichwa hiki katika mstari wa mada: Maono Yetu ya Shamba la Uponyaji la Feminist Republik!

# Picha zilizopigwa katika shamba la uponyaji





# Uthabiti wa Afya ya Kiakili katika kipindi cha COVID-19

NA TARIRO TANDI


Ugonjwa wa COVID -19 umebadili kiasili utaratibu wa ulimwengu na maisha yetu. Kwa jinsi janga hili limeathiri moja kwa moja na kwa namna zisizo wazi maisha ya watu, wengi wanateseka kwa upweke, wasiwasi na misukumo wa mawazo wakati huu tusiouelewa. Hata hivyo jambo moja ni la hakika, COVID-19 imetulazimu kwa namna moja ama nyingine kutilia maanani maswala ya afya ya kiakili.

Janga hili limeathiri sana afya ya kiakili ya watu wengi ambao walidhani waliishi maisha kamili, yenye afya na maisha yenye fanaka. Wengi wamepata pingamizi katika fikra zao za awali na jinsi ambavyo hapo mbeleni walitupilia mbali dhana ya kuzorota kwa afya ya kiakili kama ada ya maisha kwa watu wa ughaibuni pekee. Sasa wameanza kuona kuwa mtu yeyote yule aweza kuathiriwa na ukosefu wa amani ya akili kabisa maishani au kwa kipindi, wakati wowote. Hakuna mtu yeyote aliye na kinga. Afya ya kiakili ni swala muhimu ambalo sasa limekuzwa na kuwa jambo muhimu la kusisitizwa na ambao limepewa kipaumbele.

Kabla ya janga hili, wengi waliokuwa wameadhiriwa na shida za afya ya akili hawakupewa msaada waliouhitaji wala kushughulikiwa ilivyostahili. Ilikuwa tu ni ulemavu ambão haukueleweka na likaishia kwa wengi kusahaulika na kutengwa waendelee na kuteseka kwao.

Bila shaka watu wengi sana wakati huu wanaendelea kuathirika na ugonjwa wa COVID - 19 kwa njia ambazo hazijatokea hapo awali, lakini kwa watu ambao tayari pamoja na janga hili, wanapambana na mtafaruku wa mawazo, wasiwasi na aina nyingine za shida za ulemavu wa afya ya kiakili wanapitia mkasa mara mbili. Janga hili limekuwa na athari kubwa sana hasi kwa afya yao ya akili, na bado hakuna hakuna miundo inayotumiwa kutambua ni jinsi gani ambavyo watu wenye matatizo ya afya ya kiakili wanateseka sana zaidi kuliko watu wengine. Kuna haja ya kupaaza mazungumzo kuhusu afya ya kiakili ilenge kuzungumza kuhusu ulemavu wa afya ya kiakili.

Kwa pamoja, ugonjwa wa COVID - 19 umetufanya sisi kuhisi mshtuko mkubwa, kuchanganyikiwa na wasiwasi – haya yote kwa wakati mmoja. Dunia inajipata ikiwa imezidiwa na hili limesababisha dhiki kubwa ya mawazo na kiwewe. Hali ya kupambana na hii dhiki kubwa ya mawazo na kiwewe kumefungua njia mbalimbali tofauti za kuzungumzia afya ya akili kama swala la haki linalostahili kushughulikiwa. Katika



maeneo ya kufanyia kazi ambapo swala la kujadili afya ya kiakili lilikuwa ni mwiko, taasisi nyingi zaidi zinasjipata zikishurutishwa kushughulikia swala la afya ya kiakili na ustawi wa wafanyi kazi wao ili waweze kupata usaidizi kamili. Wafadhili nao pia wamejikuta wakiunga mkono maswala yanayogusia afya ya kiakili kwa washirika wanaowafadhili ili kuhakikisha wanapata msaada unaofaa wanapopambana na ongezeko la visa vya COVID-19. Hili, hata hivyo, litahitaji kufanywa kwa kushaurianana na watetezi wa ulemavu wa kiakili ili kuhakikisha ya kwamba mafunzo yanayopatikana baada ya miaka kadhaa yanaweza kutiliwa maanani.

Baadhi ya maswala jamii yanayozungumziwa na jamii kuhusu afya ya akili sasa yanaweza kutoa chimbuko lake kutoka kwa kipindi kilicholitangulia janga hili. Kama ilivyo hali ya COVID – 19 ni kuwa watu wote waliishia kutumia mitandao ya kijamii. Hili limeonyesha kuwa zawadi na shida kwa wakati mmoja. Shida hivi kwa kuwa kuna namna nyingi ya kupata habari potovu na ya uongo na kuzidi kwa kushirikiwa kwa habari kunakofanyika katika mitandao ya kijamii – hali inayowasukuma watu kuishi kwa wasiwasi usioisha - na baraka hivi kwamba kuna watu wengi zaidi wanaozifungua roho zao kuhusu maswala ya maana kwenye majukwaa haya. Tofauti na hapo awali, watu wengi zaidi wanazungumzia wazi



## Uthabiti wa Afya ya Kiakili katika kipindi cha COVID-19

maswala ya afya ya kiakili kwenye mitandao ya kijamii, wakishiriki wazi hisia zao na namna ya kukabiliana nazo. Hali hii kweli imepiga hatua ndefu katika kupunguza kabisa unyanyapaa kuhusu afya ya kiakili, huku ikileta kwa ujumla kukubalika na jamii kwa ulemavu wa afya ya kiakili na kutambulika ya kwamba hili ni swala zito linalohitaji kutiliwa makini.

Watu wanapozidi kupata ufunguzi wa kufichua na kujadili maswala ya afya ya kiakili, wanaanza kuwa katika hali ya kupungua kwa wasiwasi kuhusu unyanyapaa na fedheha zinazohusishwa na hali hii. Hii ni nafasi ambayo kwa sasa haitumiwi kikamilifu kwani mijadala mingi inalenga jinsi mkurupuko wa COVID – 19 umeathiri afya ya kiakili. Njia moja ya kueleza nguvu katika nafasi hii inaweza kuwa kuunda nafasi muhimu pale ambapo wale ambao tayari wameathirika na ulemavu wa afya ya kiakili wanaweza kuzungumzia mikakati yao ya kukabiliana na hali hii, na mbinu za kuhakikisha ukakamavu wao. Itakuwa nafasi iliyopotea ikiwa ulimwengu hautakubali kuchukua ulemavu wa kiakili kama suala la haki na kuliangazia katika nafasi maalum kama fursa muhimu iliyosababishwa na janga hili.

Kutokana na maoni haya, jukwaa la Feminist Republik, kama tu taasisi zingine nyingi na watu wengi, limekuwa likifanya kazi pamoja na watetezi wa ulemavu wa afya ya kiakili kutetezea hadharani mikakati ya kujitunza kibinafsi na utunzaji wa pamoja. Mikakati hii inawasaidia watu wengi kujenga uthabiti wa kiakili na kimwili kwa vikundi na hata watu binafsi. Kuna kutiana moyo kulikoenea ili kukumbuka kuhusu mwili na akili na ushawishi wa kuingiana na wengine, wawe wanaharakati walio na msimamo ulio sawa, familia na hata jamii kwa jumla kwa faida ya afya yetu ya kiakili.

Swala la utunzaji wa pamoja linawiana kwa akribu sana kutoka kwa haki za ulemavu ambazo hujiondoa kutoka katika "kujitunza mwenyewe" na badala yake kuhimiza kuhusishwa kwa watu na jamii kwa jumla katika kushughulikia na kusaidia katika ulemavu wa afya ya kiakili. Basi ni muhimu kufungua wazi bila kuchelewa nafasi ili kujadili masaula ya ulemavu wa kiakili kwa upana kama swala la haki linalohitaji kushughulikiwa kwa pamoja katika mikakati ya kusaidia na kutunza walioadhirika. COVID - 19 imetutunuku na wakati na utulivu ambao umetupatia nafasi ya kutekeleza utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa pamoja, na inatumainiwa ya kwmba baada ya kipindi cha mkurupuko wa COVID – 19, tutasalia na utajiri wa mazowea na mifumo ya utunzaji na ambayo tutaendelea kutumia. Wengi wanatumai ya kuwa janga hili limekuwa kama baraka iliyofichika inayotushauri kuanza upya kutafakari na kutukumbusha kuhusu umuhimu wa kuipa afya ya kiakili kipaumbele.

Janga hili limetutunuku nafasi ya kufahamu na kuelewa kikamilifu afya ya kiakili, kwanza kama aina ya ulemavu na pia kama hali ambayo inaweza kumfika mtu yeyote. Inatumainiwa kuwa baada ya kipindi cha mkurupuko




wa COVID - 19, kiwango hiki cha kukubalika kitabadilisha mawazo yanayohusishwa na ulemavu wa kiakili na kuleta mabadiliko imara yatakayoonyesha ulemavu wa kiakili ukiwa kama swala la haki. Wafadhili pia wanahimizwa kuliangalia suala la ulemavu wa kiakili sio tu kama matokea ya janga la COVID - 19 lakini kama swala la haki linalohitaji kutambuliwa na kuungwa mkono.


Picha ni aina ya uponyaji kwangu mimi

# Mafunzo na Chembe za Busara katika kipindi cha COVID – 19

NA EASTER OKECH



*"Ukosefu wa uwekezaji katika huduma bora za SRHR umeathiri sana upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana wakati wa kipindi hiki cha COVID-19"*

Janga la corona liliongeza ukosefu wa usawa ambao wanawake and wasichana kutoka jamii za wanyonge na za wale wenye ulemavu hupitia. Kazi ambayo shirika la Kenya Female Advisory Organisation (KEFEADO) linafanya miongoni mwa wanawake na wasichana katika tasnia ya uvuvi na wasichana wanaoishi kwa ulemavu katika taasisi za elimu linaonyesha kuwa serikali ya Kenya mnamo kipindi hiki haikujipanga kushughulikia masuala wanayopitia wanawake na wasichana walio na aina mbalimbali za ulemavu. Tuna stakabadhi za kuonyesha kwamba katika kipindi hiki wasichana watano wanaoishi na ulemavu wa kiakili waliokuwa nje ya shule walilengwa katika kaunti tofauti ambazo ni Kisumu, Homa Bay na Siaya, na kudhalilishwa kingono. Nyumba za usala ambazo zingewahifadhi kuwasaidia zilikuwa adimu kwa sababu ya kukosa raslimali watu ama wafanyakazi waliohitimu kushirikiana kikamilifu na hawa wasichana. Mojawapo ya kesi hizi kule katika eneo la Seme katika Kaunti ya Kisumu ni ile ya msichana aliyekuwa akitafuta pakiti ya sodo ambazo zilikuwa zinatolewa bure na mjumbe wa bunge la kaunti katika kituo kilichokuwa mbali na nyumbani kwao. Msichana huyu anayeishi na ulemavu wa kiakili alibakwa na mwendeshaji wa pikipiki na sasa hivi yu mja mzito. Msichana huyu aliwekwa katika hali hatari hii na serikali ambayo ilipokuwa ikifunga shule ilionekana kusahau kuwa vitambaa vya sodo vinavyopeanwa bure shuleni ni bidhaa ya muhimu sana kwa wasichana wengi mno kutoka kwenye familia maskini sana maeneo ya vijijini, pembezoni mwa miji na hata mijini.

Tatizo hili la kiafya kwa bahati mbaya limesababisha ongezeko la unyanyasaji wa kijinsia. Mojawapo ya vikwazo vilivyopitiwa ni pamoja na ukosefu wa njia sikivu za rufaa zenye kuwashughulikia walemavu zinazozuia utoaji wa huduma bora kwa wale walio na ulemavu nchini Kenya. Kukosekana kwa uwekezaji katkika huduma bora za haki za afya ya kijinsia na kingono,

almaarufu SRHR, kumeathiri sana upatikanaji wa haki za wanawake na wasichana katika msimu huu wa COVID - 19. Pamoja na hali kuwa nyingi za zahanati za afya kutofanya kazi kikamilifu, ubora wa huduma ulidorora. Vituo vya habari vya msingi vinastahili kupewa heko kwa kuangazia habari hii kutoka kwa jamii na pia tunawashukuru wafanyikazi wa sekta ya afya waliojizatiti kushughulikia kesi za dharura hata usiku wa manane wakati watu hawangeruhusiwa kutoka nje hadharani kwa sababu ya vizuizi vya kafiu. Lakini, hata hivyo, ukosefu wa huduma bora za haki za afya ya uzazi kwa vijana wanaobalehe kwenye vituo vyetu vya afya unasababisha kuwepo kwa habari potovu na kwa hiyo wasichana wengi wanaobalehe wanaoapitia kipindi cha mtafaruku wa kihisia na wanawake wenye umri mdogo, hasa wale walio na ulemavu wa kimwili, wa kusikia na kuona, wanajipata wakiwa wanakejeliwa na wahudumu wa afya wakitafuta haki ya huduma bora za afya zilizowekwa kwenye Katiba ya Kenya ya 2010.

Janga hili limedhihirisha wazi mapungufu yaliyoko katika sekta ya afya nchini Kenya na ni lazima tuchukue hatua kwa pamoja ili kuhakikisha ya kuwa huduma muhimu kama vile kukinga na kusimamia GBV, ikiwa ni pamoja na misaada ya ushauri nasaha na SRHR hazitupiliwi kwenye safu ya nyuma kabisa katika sekta ya afya. Jitihada yetu ni kuhakikisha ya kuwa haki za afya ya kiuzazi kwa watu wote zinapewa kipaumbele. Ni kuhakikisha kuwa jamii zimeunda asasi za kuhakikisha kuwa kitovu na mfumo wa matawi katika utoaji wa huduma za afya zinatilia maanani maswala ya jinsia, utofauti wetu, na hata ulemavu. Maswala muhimu ambayo lazima yaangaziwe ni: vituo vya utoaji wa huduma lazima vihakikishe kuwa huduma za afya ni suala la utunzaji wa afya la msingi katika kushughulikia afya bora na kuwa SRHR na GBV zinahusishwa kwa pamoja katika hatua hii ya utunzaji, na isiwe kama swala la kiafya ya kutibu. Hii inalinda kupatikana kwa urahisi kwa huduma katika pande zilizo karibu na wanaohitaji kuhudumiwa na kuhakikisha huduma bora zinaweza kupatikana.

KEFEADO inashirikiana na wasichana na wanawake wenye umri mdogo kwa kupitia michezo na huandaa mikutano kwenye nafasi tunazochezea. Kwa wanawake na wasichana walio na ulemavu, shirika hili linawashirikisha wakiwa kama wanawake mabingwa wa haki za ulemavu na huwasidia wanawake wakiwa kwenye vikundi vyao vya walemavu kujishirikisha kwenye nafasi walizonazo. Mipango ya vikundi hivi ilistahili kulengwa maalum zaidi kwani ubaguzi wa mara mbili kwenye masuala ya SRHR na hata GBV ulikuwa umebainika. KEFEADO inafanya kazi pamoja na mabingwa hawa kubuni mijadala ambayo inawahusisha watu wenye ulemavu mbalimbali tofauti na inatekelezwa na wanawake na wasichana wenye ulemavu. Changamoto iliyoko ni kwamba kuna ukosefu wa uwekezaji katika masuala ya ujumuishaji wa walemavu na washiriki mbalimbali na kufanya kazi ya kufuata nafasi ambapo utunzaji wa kibinafsi unaweza kutekelezwa na ambazo zinaitikia mahitaji ya wanawake na wasichana walio na ulemavu mbalimbali tofauti pamoja na kuwashirikisha watunzaji wao.

KEFEADO pia inapinga itifaki za COVID – 19 ambazo hazizingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu katika baadhi ya hatua. Kwa mfano, ni changamoto kwa wanawake wanaotumia viti vya ulemavu vya magurudumu wanaotakikana kusafisha mikono sanasana kwenye maeneo yaliyotengwa ya kujisafishia ya jamii ambayo hayakuundwa kwa kuzingatia mahitaji yanayoambatana na hali yao. Ni vipi ambavyo itifaki hizi zinashughulikia mahitaji yao na kutoa michakato mbadala kwa wao kuweza kushiriki na kuhusika kwa kikamilifu? Hili limesababisha kuhakikisha kwamba wanawake wengi hawahusiki kwenye mipango mbalimbali, na kwa hivyo kuwaacha wakiwa kwenye mstari wa nyuma maishani.

*"Ni muhimu pia kutambua kuwa kama watetezi wa haki za wanawake na jamii, lazima tukae chonjo kwa ukweli kwamba ugonjwa wa COVID-19 utakuwa nasi kwa muda mrefu lakini hiyo haimaanishi kuwa masuala ya GBV na SRHR yamerudishwa kwenye maeneo ya nyuma bila uwekezaji. Kufanya kosa hili kunaweza kutengua kazi nyingi ambazo tumefanya hadi sasa katika harakati zetu za kutafuta haki za mwili na uwakala kwa watu wote. Nafasi hii lazima ilindwe.*

*Nani yuko tayari kupambana? Mimi niko tayari. Je, wewe? "*



# /Xore /hom sa| Fungua Roho Yako: Mila na Tiba katika Haki ya Ulemavu -

NA FLORENCE /KHAXAS



# Kugundua tena uponyaji wa jadi kwetu sisi wenyewe, uponyaji wa harakati



Historia ya asili ya uponyaji wa jadi imeshirikiwa kupitia ndoto, maono, na maneno ya hekima na mama zetu wa Kiafrika na mama za mama zao. Wanawake wa Kiafrika hawawezi kutengwa na mazungumzo ya uponyaji wa jadi kwani kila wakati wamekuwa katikati kwenye masuala ya kiroho ya Waafrika. Hali ya kiroho ya Kiafrika inaungana na ufeministi wa Kiafrika kwa sababu yote mawili hutoa nguvu, kusudi, na upendo.



**Xore /hom sa| weka nafsi huru**

Tunafungua roho zetu tunapoachilia kuhukumu na kuziamnini sana nafsi zetu na badala yake kuungana na udhaifu wetu ambao unafungua milango ya ubunifu. Kutumia sanaa ya ubunifu kama muziki, densi, uchoraji, na uandishi ni aina ya uhuru wa roho na uponyaji. Tunapofikia kujikubali kikamilifu kwa jinsi tulivyo — safari na uzoefu tulionao, maumivu yetu, na raha zetu — tunaunda nafasi ya udhaifu wetu kutufariji. Kukaa na hatari hii katika utulivu wa kimya ni kushikilia nafasi kwa sisi wenyewe na harakati zetu. Na nafasi inakuja uwezo wa kusamehe. Msamaha kama ibada ni ya kibinafsi kama tu ilivyo ya kisiasa. Tunarudisha nguvu zetu kwa kujisamehe na kuachilia hali ambazo zimesababisha ukosefu mkubwa wa haki katika maisha yetu.

Msamaha kama kitendo cha uponyaji wa jadi hufanyika wakati tunaandika au kwa njia nyinginezo tunatoa vitu ambavyo sio vizuri kwetu, vitu ambavyo tunashikilia sana moyoni mwetu. Kwa kuzikomboa roho zetu kutoka kwenye kiwewe, sio tu tunaponya kizazi chetu, tunaponya pia majeraha ya kizazi waliyopata wazee wetu.

Tunapumua, tunaweka huru roho zetu, kwani tunatambua sisi ni zaidi ya mwili ambao tunaishi ndani. Wimbo ambao unanong'oneza kwa upepo unataka tujitenge na faraja zetu na ubinafsi wetu.

**Jiwachilie mwili wako, mawazo yako, sauti hizo, hofu hizo, kuona kwako, uwezo wako, jina lako, nchi yako. Usiwe chochote na pia uwe kila kitu yoke kwa wakati mmoja. Kuwa asiyeonekana. Uwe na ukaribishe hiyo roho. Roho haihisi maumivu.**

Haki za watu wenye ulemavu huambatana na kanuni hizi za uponyaji wa jadi pia. Tunapoingia kwenye nguvu ya mawazo na ubunifu, tunaunda kujulikana, uponyaji, na mabadiliko makubwa ya mazoea ya uponyaji yaliyopo kuwa yale ambayo ni ya jumla, ya kujumuisha, na ya kushiriki. Kwa vizazi vingi, eneo la uponyaji wa jadi humu barani Afrika limeyachukulia magonjwa ya kiakili kama ulemavu na kuyaunda kwa mitazamo hasi. Mila ya kitamaduni ya Kiafrika imekuwa wenye madhara katika ufafanuzi wao mdogo wa ulemavu kama matokeo ya uchawi au kumilkiwa na mapepo mabaya. Katika tamaduni nyingi za Kiafrika, ulemavu pia umeonekana kama laana au matokeo harsi ya karma ya zamani. Walakini, harakati ya Kiafrika ya leo ya haki ya walemavu, ikizingiatia mielekeo yake inayotegemea haki, inavunja imani hizo zenye kudhuru na zenye mipaka kupitia mipango ya kukuza uelewa. Kwa wengi, uponyaji wa jadi bado ni njia ya kawaida na inayopatikana zaidi ya huduma ya afya. Kama matokeo, ufahamu wetu wa ulemavu unabadilisha mazoea ya matibabu ya Kiagharibi, pia kuna nafasi ya mazoea ya matibabu ya kijadi na ya kitamaduni kukuzwa.

Haki ya uponyaji hutengeneza ushirikiano wa nguvu kati ya harakati za uponyaji za jadi na harakati za haki katika ulemavu, na kwa kufanya hivyo, huunda nafasi ya mpangilio wa kuzingatia anuai ya masuala katika kuendesha harakati za kifeministi kwa njia ya muungano na muingiliano.

Kuandaa mpangilio wa kifeministikwa kuzingatia muingiliano ndiko kunileta hapa, kwa haki ya ulemavu. Haki ya uponyaji iliiachilia roho yangu na nikawa mwenye kujitambua kuhusu ulimwengu tunaoishi ndani, na kuelewa mazoea ya kila siku ya nguvu. Imenielekeza kuuliza maswali: Je! Usawa rasmi ni nini ukilinganishwa na hali halisi ya maisha yetu? Nani ana nguvu?

Tunafikiria upya jinsi tunavyojipanga kama wanaharakati wa kifeministi. Mitazamo ya kifeministi na yenye makutano inaamsha uharaka wa ndani kwa ndani kufikiria tena mitazamo yetu kuhusu ujumuishaji, utofauti, na uwakilishi. Tunahitaji kuunda majukwaa ya uponyaji kupitia kazi yetu ya haki ya uponyaji kwa Watu Wanaoishi na Ulemavu (PLWD) kudai sauti zao, maoni yao, na uongozi wao. Kwa kukubali utofauti wa vidonda [na uthabiti] ambao tunabeba, tunafanya kazi kuelekea muda uliopo ambayo kuna ujumuishaji zaidi.



Nimekuwa nikifikiria sana juu ya njia ya kuaminika ya kipekee sahihi itakuwa nini ili kusimulia hadithi yangu ambayo ni sehemu ya hadithi za womn wasionna umri mkubwa na ambao wametengwa na kudhulumiwa. Tafakari hii ya ukuaji harakati ya makutano ya masuala ya kifeministi imejengwa kutoka mahali panapoongea ukweli kwa nafsi. Mawazo haya hukuza nguvu kutoka kwa uzoefu wetu wa pamoja wa upendo, kuvunjika moyo, kuishi, furaha, raha, hasira kuu, na usumbufu. Kila moja ya uzoefu huu hatimaye hutumikia kusudi la kutupa nguvu ya kujieleza. Unaturuhusu kutumia ubunifu kuhoji dhana za kuishi katika taasisi tofauti za vurugu ambazo womn wasio na umri mkubwa wenye ulemavu wanazunguka, kwa kutaja jina la vurugu hizo na kwa kuzungumza ndani ya maeneo yenye yenye kubadilika kwa urahisi ambamo upangaji wa kifeministi hufanyika.

**Mafunzo na Tiba**

COVID-19 imetengeneza nafasi kwa njia mpya za kujenga ustawi wa pamoja. Imetufundisha juu ya hitaji la haraka la majibu yanayotokana na jamii na imeunda ufafanuzi juu ya upendeleo, nguvu, na ufikiaji. Wanawake, wasichana, watu wenye ulemavu, WAVIU, wafanyikazi ya ngono, jamii za asili, wasagaji, na watu ambao wamebadili jinsia zao wamekuwa kwenye ukingo wa ukandamizaji na COVID-19 ilitupa changamoto kutafakari tena afya na ustawi na pia ujumuishaji wa kiuchumi. Tumelazimika kukabili jinsi ukweli huu mpya unavyoathiri uponyaji wetu wa pamoja na nguvu.

Kwa mtazamo huu, tunapojifunza njia mpya za kuandaa bila kuacha nafasi zetu za kimaeneo, haki ya ulemavu inatufundisha kuthamini miili yote na uwezo wao anuwai. Na kuna kujifunza mengi ambako bado kunahitaji kufanyika. Somo hapa ni kuwa na ufahamu wa ulimwengu tunamoishi, kupingana kwa nguvu na upendeleo, na uwezekano wa nguvu ya mabadiliko tunaposimama katika mshikamano kutekeleza utunzaji wa pamoja.

Wanawake ambao ni Watetezi wa Haki za Binadamu wa Kiafrika (AWHRD) wanaweza kuingiza uponyaji wa jadi maishani mwao kwa kuingiza ulaji wa mimea na dawa za mitishamba katika mitindo yao ya maisha inapowezekana, na kukagua matibabu anuwai ya nguvu, na pia kupumzika. Mapumziko ni aina ya upinzani na uthabiti katika jamii ambayo inasisitiza kwamba tunapaswa kufanya kazi kila wakati. Mapumziko husaidia miili yetu kujipigania wenyewe na wengine tunaposimama dhidi ya mfumo dume. Urafiki na udada pia ni muhimu tu kama njia zingine. Tunahitaji kusherehekeana, kuhalalisha kila mmoja, na kuonyesha upendo na kukubalika. Tunahitaji kubadilisha mashirika yetu na kuingiza mazoea kamili ya ushiriki wa uponyaji wa jadi na maarifa katika harakati zetu ili kutanguliza afya na ustawi wetu.

***Haki ya ulemavu inatufundisha kuthamini miili yote na uwezo wao anuwai. Na kuna mafunzo mengi sana ya kupatikana.***

**Nilipokuwa mtoto mdogo, nilikuwa nachukia picha...**
**Picha zilikuwa zinaonyesha mguu wangu bandia wa kulia ambao ulionekana kuwa mdogo kuliko mguu wangu wa kushoto...**
**Picha zingeonyesha jinsi ambavyo nilikuwa siwezi kusimama wala kusawazisha ...**
**Picha zingeonyesha jinsi ambavyo singeweza kuinuka kwa kuiweka miguu yangu pamoja ...**
**Picha zilikuwa zinaonyesha kasoro zangu zote...**



# /Xore /hom sa| Fungua Roho Yako: Mila na Tiba katika Haki ya Ulemavu

## Mila

Ninataka kuzungumza juu ya mchakato wangu wa uponyaji wa jadi katika safari yangu ya kuacha kuvuta sigara. Kama watetezi wa haki za binadamu, wakati mwingine tunajikuta tunajiingiza katika tabia mbaya za kukabiliana na shughuli zetu kama vile kunywa pombe na kuvuta sigara, kushughulikia athari za kihemko na za mwili za kazi tunayofanya. Miaka michache iliyopita, nilijichunguza sana na ilinisababisha kuuliza, "Je! Jukumu langu ni nini kama mtetezi wa haki za binadamu ikiwa siwezi kujitetea na mwili ambao unaniunga mkono kwa yote hayo?"

Kuunda nafasi shirikishi za uponyaji wa kifeministi kunahitaji kila mtu kuchukua umiliki wa mchakato wao wa uponyaji wake mwenyewe binafsi na safari. Tunachukua jukumu kwa kuwajibika kwa mchakato wetu wa uponyaji na tunafanya hivyo kwa kutafuta na kuingiza mazoea ya uponyaji wa jadi ulio kamilifu na / au shirikishi.

Kwa mfano, muziki unaendelea kuchukua jukumu kubwa katika kufikiria tena kiroho, Ubuntu na udada.

Kuingiza mila kadhaa pia inaweza kusaidia kupata faraja. Kama kushiriki katika nyimbo za mababu za kiroho (haswa ndani ya udada) na upigaji ngoma wa Kiafrika au umoja wa kupiga makofi kwa mikono mpaka iweze kusikika kama wimbo. Kuwasha mishumaa pia ni njia nzuri ya kuingiza mila ya uponyaji katika maisha yako.

Chaguo jingine linaloweza kupatikana na kwa wakati unaofaa ni ibada inayoonyeshwa katika kunawa mikono, kuosha ili kuondoa maumivu, kufahamu ukweli wetu mpya kama vile wa COVID-19, na umuhimu wa kunawa mikono yetu kama njia ya uponyaji na kujikinga na virusi.

Kwa kutazama tena, ninatambua jinsi tabia zenye madhara zinavyowawekea mipaka watetezi wenzangu wa haki za binadamu. Hii pia imenisababisha kuamua kwamba ikiwa ninataka kufanya utunzaji wa jamii ni lazima nifahamu athari za kuvuta moshi wa unaotokana na uvutaji wa sigara wa watu wengine. Kufanya kazi katika maeneo ambayo uvutaji sigara na watetezi wa haki za binadamu huchukuliwa kama kawaida, kumenifanya nitambue kuwa kuacha kuvuta sigara ili kulinda jamii yangu ndivyo uwajibikaji unavyoonekana pia... Kutunza jamii yangu kunamaanisha kutetea haki zetu na afya.

Mbali na mazoea haya ya nje, uponyaji wa jadi kwangu unamaanisha kitendo cha kujiandikia barua kuomba msamaha kwa mikakati ya kukabiliana na hatari ambayo nilikuwa nayo na kuweka nia kwa kutafakari mazingira mazuri ambapo ninajipa kipaumbele kwa kuongoza mtindo mzuri wa maisha kama haki za binadamu mlinzi.

Nilijipa ruhusa ya kulia na kuweka nia. Nilichagua uhuru na uthabiti kuliko hofu. Nilijizunguka kwa mawe ya kioo, nikawasha mishumaa, na nikachoma busara karibu nami. Nilikuwa na mazungumzo ya uaminifu na mimi mwenyewe juu ya maadili yangu na niliunda maadili mapya yenye kuzingatia afya. Kuunganisha na babu zangu kupitia mila hii, msaada wao ulinipa ujasiri wa kuingia katika nguvu yangu ya ndani kupinga tabia mbaya.

*Kuchanganya baadhi ya mila pia kunaweza kuwa mfumo wa kuzaliwa upya. Kama kushiriki katika ngonjera za mababu za kiroho (ikiwezekana haswa ndani ya udada) na upigaji ngoma wa Kiafrika au umoja wa kupiga makofi kwa mikono mpaka sauti iunde utungo. Kuwasha mishumaa pia ni njia nzuri ya kuingiza mila za uponyaji katika maisha yako.*

Nia ni zana yenye nguvu ya ibada ya kuponya miili yetu. Imani ndani yetu ina nguvu vile vile. Kujikomboa kutoka kwa ulevi hufungua mioyo yetu kuwa wanaharakati zaidi wa ufahamu ambao huweka kipaumbele katika utunzaji mkali na wa jumla.

Kama wanawake ambao ni Watetezi wa Haki za Binadamu wa Kiafrika, tunahitaji kujipa kipaumbele sisi wenyewe na ustawi wetu. Tunahitaji kuzungumza na sisi wenyewe. Jibu liko ndani yetu kila wakati. Kuunda mila yetu wenyewe kila siku, hutulinda na kutuweka msingi. Inaunda usawa na inatufundisha kujipenda kidogo zaidi kila siku. Kuunda wakati peke yake kwa mila ya uponyaji hutufundisha upweke; njia za kutafuta amani mbele yetu wenyewe. Afya ya kiakili ni muhimu. Haki ya ulemavu inatufundisha kuwa wema kwa miili yetu na kujali athari za maamuzi yetu kwa wengine.

Uhuru wa mwili na ulindwaji kiadilifu ni haki zetu za asili. Kuandika juu ya ukweli wetu wa kuishi kutaunda ushahidi wa kushikilia serikali zetu kuwajibika kulinda uhuru wetu wa mwili na uadilifu. Kuandika kuhusu ukiukaji ambao tunaupata kutoka kwa tamaduni yetu na kutoka kwa serikali yetu ni uponyaji wa haki. Uhuru wa mwili na uadilifu wa watu wenye ulemavu barani Afrika hauwezi kujadiliwa. Tunahitaji kuendelea kufunua kanuni na tamaduni ambazo tunajifunza kutegemea, na jinsi zinavyoathiri haki za watu wenye ulemavu.





# Uhatarishi Mara Tatu Zaidi: Changamoto Wanazokumbana Nazo Wanawake Wenye Ulemavu Katika Nyakati za COVID-19 -

NA AGNES CHINDIMBA

Nchini Zimbambwe, watu wanaoishi na ulemavu wanatambulika kama "zvirema" neno la kudhalilisha la lugha ya Kishona. Tamshi hili la kimatusi linatumika kusindilia na kukuza mawazo ya kibaguzi kibinafsi na ya umma kwa ujumla dhidi ya watu wenye ulemavu. Tabia hizi pia hazijaachana na imani potofu na ambazo baadhi wamezishikilia kwa dhati ya kwamba mtu mwenye ulemavu ni ushahidi kwamba familia ina laana, imejihusisha na ushirikina ama matendo ya kishetani. Ambayo haya yote yanaweza kuleta matokeo ya kuchukuliwa kama waliokumbwa na mapepo mabaya na kudharauliwa kwa wanawake wenye ulemavu.

Katika nchi ambayo imekuwa ikikumbana na kuangamia kiuchumi kwa zaidi ya mwongo mmoja, wanawake wenye ulemavu wamesalia wakihangaika wenyewe katika ngazi za chini kabisa kwenyemadaraja yaliyopo ya kiuchumi. Katika maeneo ya mijini wanaepukwa. Na katika maeneo ya vijijini wanashushwa hadhi na kuchukuliwa kama omba omba. Kama kwamba hali hiyo mbaya haikuwa ya kutosha mkurupuko wa gonjwa la COVID-19 mnamo mwaka wa 2019 umelifanya tatizo hilo kuwa kubwa zaidi. Mkusanyiko wa masuala ya ulemavu, COVID-19, jinsia, kijamii na kiuchumi, kiwango cha elimu, asili ya mtu na dini vyote vimechukua nafasi katika kukuza changamoto wanazokumbana nazo wanawake wanaoishi na ulemavu nchini Zimbambwe. Athari za muingiliano huu zimedhihirika wazi katika kuongezeka kwa unyanyasaji wa kijinsia hapa Zimbabwe.

Kulingana na ripoti ya mwaka wa 2021 kutoka shirika la Deaf Women Included (DWI), programu za uzuiaji na majibu yamepuuza mahitaji, vipaumbele na maslahi ya wanawake wenye ulemavu. Kwa mfano, ripoti hii ilidai ya kwamba kusitishwa kwa shughuli za kawaida ili kuzuia kusambaa kwa COVID-19 kulipelekea wanawake wenye ulemavu kuwa kataika hali hatarishi zaidi ya kuathirika na unyanyasaji wa kijinsia kuliko hapo awali. Ripoti hiyo inadai ya kwamba kwa sababu ya kusisitizwa kwa kuangazia nguvu zote kulenga huduma za kiafya zilizopelekwa katika kupambana na janga la COVID-19, wanawake wenye ulemavu hawakuweza kupata huduma zingine

# Uhatarishi Mara Tatu Zaidi: Changamoto Wanazokumbana Nazo Wanawake Wenye Ulemavu Katika Nyakati za COVID-19

za kiafya. Kwa mfano huduma za uzazi wa mpango zilipanda gharama mwaka 2020 na wanawake hawakuweza kuzipata huduma hizo katika vituo vya afya vya serikali vya karibu ambavyo labda vilikuwa vimefungwa ama havikuwa na huduma ya uzazi wa mpango.

Hii imeleta matokeo mabaya na kusababisha kesi za unyanyasaji wa kijinsia kuongezeka kwa wanawake wenye ulemavu. Mwanamke mmoja alisema "Nilienda kwenye kituo cha afya kutafuta vidonge vya uzazi wa mpango na nilipata changamoto kupita vizuizi vya polisi sababu walitaka kuona vibali. Lakini nilifanikiwa kufika kliniki ila kuishia kuambiwa hakuna vidonge na niliambiwa nikanunue kwenye duka la dawa. Nilipofika duka la dawa vidonge vilikuwa vinauzwa kwa Dola 1 ya Marekani ambayo sikuweza kuimudu. Nilipofika nyumbani mume wangu alitaka tushiriki tendo la ndoa na nilikataa kwa sababu sikutaka kupata uja uzito. Yalitokea majibizano makubwa nyumbani na mume wangu alinipiga vibaya sana, lakini sikuweza kufanya chochote."

Usitishwaji wa shughuli ulileta ugumu kwa wanawake wenye ulemavu kupata huduma za unyanyasaji wa kijinsia. Upatikanaji wa ushauri nasaha mtandaoni haujumuishi watu wote kama inavyoonekana, kwa mara nyingi kama ilivyo kawaida, wanawake wenye ulemavu huwa pia wametengwa kiuchumi na wengi wao hawana vifaa vya kisasa vya kama vile simu ya mkononi ya kisasa ama hata data za intaneti zinazohitajika. Kwa womn wenye ulemavu ambao wanaweza kumudu gharama za simu na data, wanaweza kupata huduma kutoka kwa watoa huduma za ushauri nasaha mtandaoni ila ambazo hazijumuishi matumizi ya lugha za ishara, jambo linalowafanya wanawake wenye ulwamavu wa kusikia kuwa na ugumu wa kupata huduma hizo.

Upatikanaji wa bidhaa za sodo pia imekuwa changamoto kubwa kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu kiasi ya kwamba wengi imebidi watumie njia zisizo salama kiafya kama vile kinyesi cha ng'ombe kunyonya hedhi yao. Wanawake ambao kwa kawaida walitegemea kujihimiza wenyewe na ujasiriamali wao wenyewe ili kijikimu kimaisha na kupata mahitaji muhimu walisukumwa kwenye umasikini baada ya masoko yasiyo rasmi kufungwa. Nchini Zimbabwe, wengi amabo kabla ya janga hili kutokea walikuwa wakifanya biashara za uchuuzi, biashara za kuvuka mipaka ya nchi waliathirika baada ya kutolewa uamuzi wa mipaka kufungwa ili kulidhibiti janga hilo.

Janga hili pia limezidisha kina cha changamoto ambazo watu wenye ulemavu wanapitia katika kupata taarifa. Vyombo vya habari vimekuwa vikitoa ujumbe na taarifa tele kuhusu COVID-19. Cha kusikitisha, taarifa hizo hazijatolewa kwa kutumia mifumo jumuishi; hakuna lugha ya ishara, hakuna nukta nundu, hakuna nakala za sauti za lugha asilia na bila shaka hakuna chapisho zenye maandishi makubwa kuzingatia utofauti miongoni mwa wanawake wenye ulemavu. Hali hii imewaweka hatarini wanawake wenye ulemavu kwa kuwa hawana taarifa na uelewa wa kutosha kwa yanayoendelea katika mazingira yao. Hii inawaweka hatarini kupata maambukizi bila kuwa na taarifa kamili.

Ingawa changamoto hizi inabidi zijadiliwe mara nyingi iwezekanavyo, kuna nafasi pia ya kuandaa maongezi kuhusu nafasi zilizopo tunapoendelea kujiandaa kwa mambo ya siku za baadaye na kujenga jamii zenye zimejihami na nyenzo bora za kupambana na mikurupuko ya majanga yatakayojitokeza kutokana na tuliyojifunza katika janga hili. COVID-19 imeleta nafasi ya utetezi wa mipango ya kimaendeleo iliyo jumuishi tunapoendelea kusukuma zaidi haki kwa wanawake wenye ulemavu. Nyakati ngumu zimefungua milango ya ushirikiano imara na jumuishi, na mashirika kama ya vile vyombo vya Umoja wa Mataifa, vyuo vikuu, vyombo vya habari, mashirika ya utetezi wa haki za wanawake na serikali ili kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma. Zaidi ya yote, hizi changamoto zote, ingawa zinaweza kuepukika, zimewafanya wanawake wenye ulemavu kuungana na kuwa na nguvu zaidi. Tunaunganisha nguvu zetu na kuibua mikakati ya kujumuishwa katika nafasi nyingi mbali mbali baada ya COVID-19.

# Dizeli - na Kiko Enjani

Macho yako yanafunguka kwa mambo manne:
Kuna mngurumo kila mahali,
Umevaa helmeti,
Umefungwa kwa mikanda kwenye kiti,
Na miko yako imeshikilia duara ya kuendesha .

* * *

"Wakiendelea kumgonga huyo mpumbavu, hili gari litalipuka." Ess Tablishment anasema.
"Kwa hivyo, wacha iwe hivyo," Spec Tator anaongezea bila kujali.
Ob Server anakubaliana: "Hawa wajinga wakiacha kujaribu kuliepa hilo shimo; mbio hizo huenda zisiwe na watu wengi sana hivyo."
Ile traki na stadium zimeuzingira ulimwengu. Nje ya hiyo traki kulikuwa na shimo lisilo na mwisho, ndani ambamo wakati mmoja walituma droni. Zilichukua siku tano kushuka hadi mwisho.

* * *

Inua mguu wako kutoka kwenye pedali moja, na hilo gari linajigonga kwako. Ibane sana chini pedali nyingine na unaligonga lilio mbele yako.
Kulipta gari lingine na utapata ishara ya matusi kutoka kwa huyo dereva mwengine.
Gari moja mbele linagongana na linguine. Unapunguza kasi unapoona yote mawili yakilewalewa kutoka traki na kutokomea.
Utasalia kwenye eneo la katikati kuanzia sasa kuendelea.

* * *

"Chungeni Nambari 1 hadi 9!" Server anautangazia uga.
Tablishment anajiuliza kama ni magari mangapi yatawaondokea kwenye traki ili waweze kupita.
Kama ilivyopangwa, madereva elfu moja walishindwa kuyadhibiti magari yao na kutumbukia kwa siku tano: wakienda na wengine wengi pamoja não.
Lazima wapishwe wale wanaostahili zaidi.

* * *

Uliwaona wakiangamia kwenye shimo lisilo na mwisho.
Haikuwa ajali; kuondoka kwao kuliacha njia. Na kwenye njia hiyo kukaja kikundi maalum, kila moja kapakwas rangi nambari yenye herufi moja.
Unakuika muundo na kulifuata Gari nambari 8.
Gari nambari 9 linajaribu kupita, lakini kizuizi kinafungika na kisha kuna mgongano.
Unapuuza moto mkubwa unaowaka kwa sasa mbele yako na kumwangalia kwa mshangao mwenye makosa.

"BILLIONI SABA ANAMUACHA 8 KWENYE VUMBI!"
Gari nambari 5 anakugonga kwa upande, kwa kurudiarudia. Unamwachia akusukume kuelekea pembeni. Ana mashine bora zaidi:
Haiya, huenda hata labda alipitia mafunzo ya mambo haya.
Lakini ukosefu wako wa uzoefu una maana ya kwamba chombo chako huenda wakati mwingine kikashtuka kurudi nyuma.
Wengi kwenye uga wanamaka 5 anapotokomea.
Magari namabri 3 na 4 wameshtuka sana hadi wanakupisha uende.
Mashindano sasa ni kati yenu watatu. Kuondoka kwengine kunatokea mbele ya Gari 1. Wewe hauzingatii kifo; traki imeachwa wazi.
Mbio za kasi zilizo wazi, unanguruma kama mnyama huku ukikihimiza chombo chako kisonge mbele.
"BILLIONI SABA YUKO BEGA KWA BEGA NA KWANZA!"
Ile rangi ya mabatobato inazidi kukukaribia. Sasa umeinama mbele, unanyongwa na mkanda wako wa kiti. Na pale ambapo mbele ya mshindani wako inakuwa nyuma yako, unapiga ukelele wa furaha ukisherehekea kuupita mstari wa kumalizia.
Wa kwanza kabisa kutoka Billions.

* * *

Watu wengu kwenye uga hawajawai kucheka sana hivyo maishani mwao.
"Huyo mpumbavu aliyepitwa alidhani KWELI eti alikuwa anaenda mbio ili kumaliza mashindano. Hauwezi kulibuni hili."

* * *

Unainua mkono mmoja ili kufuta machozi na kukipata kitu kilicho kwenye shingo lako. Ni kidude cha sikio.
"Tafadhali wakati huu nipe jibu," sauti mpya inasikika kwenye kichwa chako.
"Kidude change cha sikio kilidondoka. Je, unaweza kunisikia?"
Ile sauti nyingine inasema kwa mshangao. "Je, unaweza kunisikia MIMI?"
"Ndiyo. Mbona kuna wengi wenu wanaojaribu kusema kwa wakati mmoja?"
Sauti nyingine inachukuwa zamu. "Sisi ni Wahudumu wako ya Kulikagua Gari Unaposimama."
"Nani... wangu?"
"Fuata msitari wa manjano kwenye ramani iliyoko kwenye dashibodi lako."

Wako chap chap. Mara tu unapofika kwenye eneo la Pit, kuna wale tayari wameshayabadhilisha magurudumu yako, wamejaza tena mafuta kwenye gari, wameiinua helmeti yako ili kukurushia maji kwa uso.

* * *

"Kwa hivyo hii ni yangu ..."
"Mzunguko wa 50," wananieleza wakati ambapo nimerudi kwenye traki. "Mashindano haya ni lapu 1000 ndiyo yaishe. Hakuna anayeruhusiwa kuondoka hadi yaishe. Kila kuondoka kunazalisha mwanzo mwingine."
Gari 1 amerejea, anakuning'inizia chambo.
"Usijisumbue. Wako kwenye lapu yao ya 400. Hakuna unavyoweza wewe kuwafikia."
"Kuna haja gani kufanya haya yote basi?"
"Kwa kusema ukweli," kidude cha sikio anakiri, "sisi ....tuliyapata tu haya hapa, na tunafanya tu yale tunayoweza ili kuepuka kuwawa. Tafadhali fanya bidii ufikie muda unaofuata wa kusimama tena."
Baada ya lapu yako ya 60, wewe fanya hivyo.

* * *

Upepo unaleta kibaridi kwenye uso wako helmeti yako unapogonga chini.
Kaa kwenye sehemu yam choro wa msitari mweupe pembezoni mwa traki na unaweza kuliepa shimo lisilo na mwisho. Tembelea upande huo kwa muda mrefu kutosha na utaweza kuingia katika eneo la pit lililo mwisho wa mstari wa manjano kwenye dashibodi lako.
Mtu anakusaidia kujilaza kitandani.

* * *

"Jameni, inaonekana kuna magari mengi yanayosimama. Madereva wanashuka kutoka kwa magari yao. Wanatembea..."
Kila mtu amemuaangazia Tablishment macho kwa mshangao, naye anasema kwa kutojali.
"Iwapo kuna nafasi ya washindi kupita, haijalishi chochote."

* * *

"Wataizunguka hiyo traki milele?" Wewe unauliza.
"Labda."
"Kuna jambo jingine lolote ila mashindano haya?"
"Ndiyo. Na sayari zingine, pia."
"Je, tunaweza kuenda huko?"
"Wakati ambapo tutamkusanya mtu mwengine mmoja zaidi.... bila shaka."

# Mahojiano

## NA ELIZABETH MANG'ENI



**FR: Unaonekana ukiwa mrembo, kubadilika kwako kulitoka wapi? Namaanisha, ni wakati upi uliamua kufikiria upya kuhusu ubinafsi wako na nini kilisababisha?**
Nilihusika kwenye ajali mbaya ya mauti barabarani katika mwaka wa 1994 na hii ikasababisha kupoteza mguu wangu wa kulia. Tangu siku hiyo, nimelazimika kutumia mguu wa kubandika ili niweze kutembea na kufanya shughuli zangu za kila siku. Nilipokuwa nakua, nilikumbana na ubaguzi kutoka kwa jamii, na hili lilisababisha athari hasi kwangu licha ya kutiwa moyo na familia yangu. Ilipunguza namna nilivyojihisi kuheshimika na hii ikawa ni kikwazo kwa maendeleo yangu.

Nilipokuwa katika mwaka wangu wa kwanza wa chuo kikuu, nilisoma nakala iliyoandikwa kuhusu Frida Bedwei; mhandisi wa programu aliyesifika sana kutoka nchi ya Ghana na ambaye maisha yake na mafanikio yake hayawezi kufikiriwa. Haikuwa kazi yake ya uhandisi wa programu ulionishangaza sana, bali ni hali yake aliyokuwemo. Bedwei aligundulika kuwa na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo akiwa na umri wa mwaka mmoja. Ugonjwa wa kupooza kwa ubongo ni ugonjwa usiopona wala kutibika wa neva na unaathiri kabisa utendakazi wa mwili, mkao wa mwili pamoja na kuathiri ushirikiano wa misuli. Mtu aliye na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo kuishia kuwa mhandisi wa programu za kompyuta ilikuwa jambo jipya kwangu. Farida alibuni namna ya kuushinda ulemavu wake na leo yeye anachukuliwa kama mmoja wa wanawake wenye ushawishi zaidi katika teknolojia ya kifedha barani Afrika. Alithibitisha kuwa ulemavu haumaanishi ni unyonge. Kwa kweli, ni msukumo upi zaidi nilihitaji wakati huo? Tangu wakati huo, nilikumbatia ulemavu wangu na sijawahi kuangalia nyuma. Hiyo ndiyo ilikuwa hatua yangu ya kubadilika.

**FR: Je, sasa una mtazamo tofauti kujihusu na kuhusu mwili wako?**
Iwapo ungeniuliza swali hili miaka saba iliyopita, ningekupa jibu bila tashwishi kuwa ulemavu wangu ni dosari. Lakini leo, kwa kweli sidhani ulemavu huu ni dosari. Mguu wangu wa kubandika hunifanya nione maisha kutoka kwa mtazamo tofauti sana. Ninaweza kuwaonyesha wanaopambana kuwa ni sawa kuwa tufauti. Ninaamini kuwa Mungu alichukua kitu kutoka kwangu na kunifidia na kitu kingine kama malipo.

FR: Ni wapi unaitoa nguvu kwa njia unazopitia maishani leo? Chanzo chako cha uponyaji ni kipi?
Mungu: ninashuhudia kuwa maombi hutimizwa. Familia: msaada kutoka kwa wazazi na wanuna wangu hunipa motisha kila siku. Rafiki zangu wa dhati wanaonifanya niwe kiumbe bora kwangu na mwishowe, kupata kufikia uzoefu kutoka kwa watu wengine ambao wana ulemavu wa kukatwa mguu kama mimi.

**FR: Je, unahisi kuwa picha zina namna ya kuponya nafsi ya mtu? Je, picha zako zimetoa aina yoyote ya uponyaji? Kama jibu ni ndiyo, ni aina zipi hizo?**
Nilikuwa ninachukia picha hapo mbeleni. Ningepigwa picha, ningehakikisha hazionyeshi ulemavu wangu kwa sababu picha hizo zingeonyesha mguu wangu wa kulia ambao ni wa kubandika na ambão ungeonekana mdogo kuliko mguu wa kushoto. Zingeonyesha namna ambavyo singesimama tisti wala sawasawa. Picha zilionyesha kasoro zangu zote.

Leo hii, nimejifunza kuzipenda picha kwani picha ni njia moja ya uponyaji. Nimejifunza kuthamini wanawake ambaye nimeibuka kuwa na jumbe pamoja na uzoefu ninaoshiriki kwa kupitia picha zangu. Kila siku, ninatumai ya kwamba picha zangu zinahamasisha wengine waweze kuthamini kasoro zao na kuzionyesha kwa madaha kwani hakuna binadamu yeyote yule aliye kamili.



**FR: Je, uponyaji unaokunekania vipi katika wakati huu? Ni kwa kule kuzipiga na kuzitazama zile picha? Ni namna unavyosimama ili kupigwa picha? Je, ni kwa kushiriki picha zako na watu wengine kwenye mitandao ya kijamii?**
Uponyaji ni wakati ninaposhiriki picha zangu na uzoefu wangu. Uponyaji ni wakati ambapo watu wanaathiriwa kutoa maoni kuhusu picha na pia wanajihusha na picha hizi. Hili linawatia moyo kwani wanaona msichana mrembo aliye na tabasamu nzuri na ndoto kubwa za siku za usoni zitakazokuwa bora.

**FR: Ni ujumbe upi wa uponyaji ungependa kuwaambia wanawake walio na ulemavu na wanaopambana na masuala ya kukubalika?**
Kuwa kama wewe mwenyewe. Maisha yako ni yako wewe binafsi. Hauna chochote cha kuthibitisha kwa watu kwa sababu ya shinikizo hili litakulemea. Si lazima ujaribu kujitosheleza hata usipofaa kwa madhumuni ya kutaka kujikubali na kukubalika.

Kuwa tofauti kuna wakati wake wa fahari. Kwa mfano, ukiwa wewe ni vanila, hakuna yeyote anayetambua lakini unapobadilika kuwa chokoleti watu hupata hamu ya kukujua. Wewe ni hiyo chokoleti. Kuwepo kwako kwenye ulimwengu huu siyo kosa. Yeyote anayekuwa katili kwako kwa sababu ya ulemavu wako hastahili awe anapata muda au fikra yako hata kidogo kabisa. Jitokeze uwe mtetezi wako binafsi badala ya kujililia tu ndani ya nyumba. Wewe ndiye uliye kwenye usukani wa maisha yako. Tupilia mbali haya zako na hofu za unyanyapaa.

## Sababu Zangu Kupigania Ulimwengu Usiokuwa na Kaasumba ya Kujiweza

NA FRANÇOISE DOGOMANGUE

Jina langu ni Françoise Dogomangue kutoka katika mji wa Dapaong, ambao uko katika eneo la Kaskazini mwa nchi ya Togo. Mimi ni mwanawake wa umri wa miaka 41 na ambaye ninaishi na ulemavu.

Nilizaliwa katika familia iliyokuwa na baba mmoja na mama mmoja ila Watoto 8 wasichana wanne na wavulana pia wanne, nikiwa ni mimi tum toto wa kipekee katika familia hiyo mwenye ulemavu. Nikiwa bado mchanga, nilipohitimu miaka minane, nilipooza kwenye sehemu ya chini ya miguu yangu. Hali hii ilifanya kuwa vigumu sana mimi kutoka nyumbani kwetu na raslimali si haba ilihitajika ili kuhakikisha nimepelekwa shuleni kupata masomo.

Kuhudhuria shule haikuwa kazi rahisi! Waliokuwa wanafunzi wenza kwenye darasa langu kila mara walinizomea kwa sababu ya mwenendo ewangu kwa miguu ambayo haikuwa inatoshana. Nikiwa naelekea shuleni kila mara, ilikuwa ni kawaida kuanguka anagalau mara mbili kabla ya kufika darasani. Licha ya vizuizi hivinilijikakamua na kuwa mwenye nguvu na hatimaye nikaweza kuhitimu na kisawe cha kiwango cha juu cha shule ya upili katika masomo ya Sanaa na pia nikasomea stashahada ambayo iliniwezesha kuhitimu na kuwa Katibu Mtendaji, huku hili likiniwezesha kujiunga na ulimwengu wa walioajriwa kama mwalimu wa shule ya msingi na pia ya chekechea.

Kwa sasa mimi ni mama wa watoto watatu wazuri na werevu; hata hivyo uzoefu wanguwa ubaguzi umeendelea kueneeza wingu lake jeusi katika Maisha yangu ambayo ambayo bila hili yangekuwa ni yenye ufanisi mkubwa.  Nimeweza kupitia matukio ya kibaguzi kutoka kwqa mashemeji zangu ambao hawajaficha hisia zao ya kwamba hawajanikubali kama mmoja katika familia yao. Walimsihi mume wangu asinioe kwa sababu ya ulemavu wang una hata kwa wakati mwinhgine waliweza kuzua vurugu ya kimwili! Mapenzi na kujitolea ambako mume wang una mimi tulishiriki mwanzo wa uhusiano wetu yalinitia nguvu na tukaendelea na Maisha yetu pamoja; hatimaye mshemeji zangu walisalimu amri na kuturuhusu mimi na mume wangu kufunga ndoa.

Hata hivyo, kutokubalika huko kuliweza, baada ya muda, kuthibitisha kuwa jambo kubwa sana ambalo halikuwa rahisi kushinda. Kwa kipindi, tamko "Familia yangu walikuwa wameipinga ndoa yetu" lilitokea mara kwa mara katika mijadala yetu. Hili lilielekeza kuwepo kwa unyanyasaji wa maneno, na hatimaye kukatokea sasa kushambuliwa kimwili. Nimekuwa mwathirika wa unyanyasaji wa nyumbani. Niligeukiwa kikatili na yule yule mtu ambaye hapo mwanzo alikuwa ameshiriki na mimi kujitolea kwake kunipenda, kunisaidia na kunilinda dhidi ya ubaguzi, mimi niliumizwa na kupata mvunjiko kwenye mguu wangu wa kulia ambao ulihitaji upasuaji wa haraka. Hili jeraha, tokeo la vurugu za mume wangu. Kuongezea hali mbovu zaidi, kupata utunzaji wa kimatibabu kaka mwathiriwa wa unyanyasaji wa nyumbani ilikuwa ni changamoto kwa sababu ya ukosefu wa miundo msingi ya kimatibabu.

Upasuaji huo haungeweza kukamilishwa katika mji wa Dapaong, ambako mimi ninaishi, na ilibidi nihamishwe hadi katika hospitali ya chuo kikuu katika mji mkuu, almaarufu Centre Hospitalier et Universitaire (CHU) Campus jijini Lomé ambako nilikaa hospitalini kwa kipindi cha miezi minne. Niliporudi mjini Dapaong, kwa sababu za kuhofia kwamba unyanyasaji na vurugu hizi huenda zikasababisha mimi kupoteza Maisha yangu, nilijiondoa kutoka nyumbani kwa mume wang una kukodi chumba kimoja mahali ambapo kwa sasa naishi na watoto wangu.

Katika Nyanja za kijamii, ninaendelea kupitia uzoefu wa kila siku wa kukatisha tamaa wa kujaribu kuendesha maisha katika ulimwengu uliojaa kasumba dhidi ya walio na ulemavu, kama mwanawake na pia kama mama ambaye mara kwa mara hana budi kukutana na na kushiriki nafasi Pamoja na wanawake wengine ambao hawaishi na ulemavu wa kimwili. Kuzungumza kujieleza na kuweza kueleweka kunaweza kuwa na changamoto pale ambapo jamii hizi hazichukui hatua ya kuzingatia mitazamo ya watu wanaoishi na ulemavu. Kwa makundi haya ya wanawake, kuiweka hali hii dhahiri, yule ,mwanamke mwenye ulemavu hana nafasi miongoni mwa wanawake ambao hawana dosari za

kimwili.

Ni kwa sababu ya uzoefu huu uliojitokeza mara nyingi ndiyo nimebadilika polepole na kuibuka kuwa mtetezi. Nimeamua kuvivunja vizuizi hivi kwa kuzungumza kuhusu ulemavu wangu ili kuwahimiza na kuwatia moyo dada zangu ambao wanaishi na ukatili kama huu kila siku maishani mwao. Ninawahamasisha na kuwajulisha kuhusu ukweli uliopo ya kwamba wasijiruhusu kufikia kiwanga ambapo watavunjika mioyo. Ninafanya utuetezi wa kutaka kupata ulimwengu ambamo womn wenye aina mbalimbali za ulemavu wana uhuru wa kuweza kujitegemea wenyewe kiuchumi na kwamba wanaweza kupata misaada wanayostahili. Hii ndiyo kazi ambayo asasi ya REFED inanuia kufanya.

Ndiyo! Jukumu linalotimizwa na REFED kama shirika ambalo linapigania haki za womn kuishi maisha yaliyo huru kutokana na ubaguzi ni jambo ambalo limeniwezesha kuwa huyu womn ambaye kwa sasa amepata mafanikio makubwa.

Mabali na shirika la REFED, tuko na shirika lingine la watu wenye ulemavu linalojulikana kama Association of Motivated People Living with Disabilities of Tône (APHMOTO), ambamo mimi ni mmoja wa wanachama wanaotenda kazi, na ni shirika ambalo limefanya kazi kubwa ya kujaribu kuhakikisha ya kwamba watu wanaishi na aina mbalimbali za ulemavu wamehusishwa katika jamii kwa usaidizi bila kuchoka kutoka kwa kwa shirika la muungano wa mashirika ya walemavu nchini Togo, almaarufu Togolese Federation of Associations of People Living with Disabilities (FETAPH). Mashirika haya yanalenga kuhakikisha ya kwamba kuna ulimwengu bora Zaidi kwa walemavu usiokuwa na ubaguzi.

Mimi huandaa mafunzo kuhusu maendeleo ya kibinafsi, miradi ya ujasiria mali kama vile utengenezaji wa sabuni, kemikali za kutoa rangi, vifaa vya urembo vilivyoundwa kwa vitambaa vya Kiafrika, na vifaa vya kurembesha maeneo, na kadhalika.

Mimi ndiye mwenyekiti wa kundi la wanawake wenye ulemavu. Mimi huwa nawahimiza dada zangu kufanya mazoezi ya uponyaji na utunzaji wa kimageuzi. Na katika baadhi ya siku, muonekano wa mazoezi yangu ya utunzaji wa kimageuzi ni kuwashawishi dada zangu kuendelea kutabasamu na mimi kuwaandalia shughuli za burudani ili kuwapa faragha.

Hivi leo, mimi niko na ujasiri kwangu mwenyewe binafsi na kwa anuai ya uwezo wangu, jambo ambalo linanipatia nafasi ya kuwa mfano wa kuigwa na wanawake wengine wenye ulemavu. Bado ninapambana kila siku kuweza kukimu mahitaji yang una yale ya watoto wangu katika ulimwemngu uliojaa kasumba ya kuzingatia zaidi watu wasio na ulemavu, ila ninaendelea kuwahimiza wanawake wengine wenye ulemavu wasife moyo kwenye vita hivi. Kulizungumzia suala hili ni kupona na kujiwezesha kukubali kusahau majeraha yanayosababishwa na ubaguzi, kulizungumzia suala hili ni kuwa na athari kwa jamii, kulizungmzia suala hili ni kukua.

Katika kuuandika ushuhuda huu, mimi ninajiweka huru na ningependa sana iwapo hadithi hii itarekebisha anuwai ya udhalimu mwingi sana ambao womn wenye ulemavu kote ulimwenguni wanapitia huku wakinyamaza wakiwa hawana uwezo wa kuyaelezea.



# Shairi la Mwanamke Mwafrika na Watetezi wa Haki za Kibinadamu za wenye Jinsia Tata

NA BEAUTY BOOIS

Hisani yako, nguvu zako, na ako ari kupambania usawa,
Kupambana dhidi ya mfumo - dume na kuelekezea mwisho wa dhiki ya ulimwengu,
Ni hali sawa na roho iliyotakaswa.
Kwa hiyo, usiwahi kuogopa kuzungumza kwa uwazi na kuelezea haki yako ya uhuru.

Zile nguvu na baraka za wahenga alfu moja zinatiririka kwenye mishipa yako,
Kwa hivyo, wewe paa juu ya kiwewe chako, jitikise uwe huru kutokana na ufungwa huu na uiondolee minyororo ubongo wako,
Kukataa kupokea wala kuhifadi hali ilivyo, kwa sababu unajua haki zako na unakataa kuathirkia na tatizo hili.

Wacha wimbo wa mawimbi ya gharibiny ya bahari, unapambana na kupigana na kufanya kazi kuhifadhi
Ulimwengu kutokana na wehu wa wapendao hali yao, wandani wao na uume wa kuudhi.
Ujasiri unatiririka kwenye mishipanyako, bila chochote cha kupoteza ila nyororo zetu,
Kwa hiyo, unakataa kuzuiliwa na bunduki zao, korokoro za jela wala mabomu ya vitoa machozi.
Unasimama imara katika nguvu zako, huku ukiuwasha mtindo,
Huku ukikataa kuruhusu chuki zao kukuangamiza,
Kwa sababu ni upendo, uhuru na amani zinazokupa nguvu.

Kwa hiyo, unainuka na kuipaaza sauti yako, ukiwaacha bila chaguo ila kusikia mngurumo wako wa simba,
Huku ukikuwa, ukipaa, na kukwea,
Huko nje, mbali na njozi za ajabu za mababu zako, kwa sababu,
Wewe ndiye tumaini na ndoto ya mtumwa, anayeamka kutoka uzingizini kudai haki zako na huru.

Kwa sababu muda baada ya muda unaandamana mitaani
Ukiimba nyimbo za uhuru huku ngumi zikiwa hewani
Huku ukipambania uhuruna kila kitu unachikijali
Huku ukiimba madai yako ya kukupa uhuru,
Bila kuwapa nafasi ya kupumua hadi waone
Ya kwamba umekataa kuishi katika ulimwengu usiokuwa na usawa na uhuru,
Na kule kujawa na raha kamilifu ya haki yetu ya maisha,
uhuru kutokana na utumwa, ile haki ya faragha,
Ile haki ya uhuru, ulinzi, usawa na hadhi.

# Haki ya kupata Fursa Sawa kwa Wanawake Wenye Ulemavu

NA MICHELE SOJIP

"Wasifu wako unavutia, na maelezo yako yanaendana na kazi yetu, lakini kwa bahati mbaya tunasikitika kusema kwamba huwezi kupata nafasi hii ya kazi. Mazingira yetu ya kazi hayako rafiki kwako na hatuna fedha za kutosha kuweka mazingira rafiki kwako ili ufanye kazi bila kupata shida." Sentensi hizo mbili hunifanya nisike kama dunia yangu imefika mwisho. Sikuwa nimewahi kupitia ukandamizaji kwa sababu ya ulemavu wangu lakini maneno haya yalikuwa kama bomu kwangu. Je, ulemavu wa kushindwa kutembea ndio uma athari kama hii? Na nitakuwa nikihukumiwa kwa sababu tu natumia kiti cha kutembelea? Na ulemavu huu utaninyima haki zangu zote ikiwemo haki ya kupata kazi, hata ingawa katiba ya nchi ya Kameruni imeweka sheria kuu inayosema kwamba kila mtu ana haki ya kufanya kazi ?

Sitakuwa muongo nikisema watu wengi wenye ulemavu wamepitia ukandamizaji. Ingawa kufikia sasa takwimu rasmi hazijulikani, kuna idadi kubwa ya watu Kameruni wenye ulemavu wa viungo, kusikia, kuona, kuhisi, kiakili, maumbile au ulemavu wa aina nyingine. Ili kuboresha hali zao za maisha, sheria namba 2010/002 ya Aprili 13, 2010, ya kulinda na kukuza watu wenye ulemavu ilipitishwa.

Hata hivyo ilichukua miaka nane tena, hadi Julai 26, 2018 kuanza kufanya kazi. Ijapokuwa kuna maboresho yalianza kuonekana miaka miwili iliyopita, lakini bado kuna pengo kubwa kati ya sheria iliyotungwa na utekelezaji wake. Kushindwa kufika mahakamani ama kupata huduma za kiserikali kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu ya walemavu, kumlipa mkalimani kwa gharama za mtu binafsi katika maswala ya kimahakama, kunyimwa nafasi ya kujiunga na shule kwa sababu ya ulemavu, kukosa nafasi ya kazi japokuwa uma vigezo vyote kwa sababu ya kuwa mlemavu, kutokufaidika na nyumba za gharama nafuu za serikali, upungufu wa bidhaa za kila siku zenye maandishi ya nukta nundu kwa watu wasioona. Sheria ambazo zimepitishwa lakini hazifanyiwi kazi ila zinaonekana tu kwenye makaratasi ni nyingi. Vipi kuhusu ubakaji kwa wasichana wenye matatizo ya kiakili? Kunufaika na hali yao ya kutojielewa? Kesi za Kutendewa vibaya? Kimwili, Kiakili au kuwanyanyasa kifedha? Kuwanyanyapaa na kuwatenga?

Kuna waathirika wengi sana walionyamaza na kuishia kujitenga na jamii, na kujiona watu wasio na msaada, na wanapitia kila aina ya ukandamizaji. Kuishi katika jamii ambayo inafungia macho unyanyasaji, kuumizwa kwa womn na wasichana wenye ulemavu kunamaanisha kwamba sio wengi walikubaliana na hali yao ya ulemavu na kuweza kujisimamia. Dhana potofu ya ''kutokuwa kawaida'' kwa walemavu inaendelea kukithiri. Kupata haki sawa, kutendewa kama wengine na kupata nafasi sawa licha ya kwamba haitoi tu heshima kama

# Haki ya kupata Fursa Sawa kwa Wanawake Wenye Ulemavu

mwanadamu na haki iliyowekwa kisheria. Inaelezewa kwamba lazima usikilizwe na, licha ya yote, uelewe, hivyo kumaanisha mtu anatakiwa ajue haki ambazo anazidai. Amri iliyowekwa katika sheria ya mwaka 2010 iko wazi katika pointi moja, kipengele cha 2 kinasema ''Kipengele hichi kinahusu watu wenye ulemavu ambao wanavyo vitambulisho vya kitaifa vya walemavu na ambao wako hatarini kuwa na ulemavu angalau kwa 50%."

Kupambana kwetu sio tu kwa njia za kukosoa. Inatakiwa tudai vile ambavyo tunatakiwa tupewe, lakini ni muhimu kufanya kazi kwa pamoja. Kama watu wenye ulemavu wanafanya kazi kwa pamoja vitu kama kutengwa, kutokuwa na thamani, kunyanyaswa na kila aina ya mateso na ukandamizaji wanaopitia vitapotea. Umoja huu unatakiwa uenee katika bara zima, ijapokuwa baadhi ya nchi wamepiga hatua kubwa sana, hasa katika miundombinu ya usafiri na maeneo ya umma.

Kubadilishana uzoefu pia ni muhimu. Jinsi gani hatua hizo zilifikiwa katika nchi hizo na kitu gani kinachohitajika kifanyike nchi nyingine pia, na jinsi gani vinaweza kuigwa, huku kukiwa na hali ya kuangalia uhalisia na muktadha wa kila nchi?

Mwisho, Ni muhimu kutambua pengo lililopo katika upande wa sheria kama sheria ya Kameruni ambayo inalinda shule, wataalamu, wasimamizi wa vyuo vikuu, waajiriwa na wakurugenzi ambao wanabagua watu wenye ulemavu kupata masomo na ubaguzi wakati wa mchakato wa kujiunga na shule ama katika ujira.





Leo nimejifunza kupenda picha kwa sababu ni aina fulani ya uponyaji. Nimejifunza kumthamini mwanamke ambaye nimegeuka na kuwa pamoja na ujumbe na uzoefu ninaoshiriki kupitia picha zangu. Kila siku, natumai ya kwamba picha zangu zinawahamasisha wengine kuzikubali kasoro zao na kuzionyesha kwa madaha kwa sababu hakuna mwanadamu aliye mkamilifu.

# Hebu Tuzungumze Kuhusu Ngono, Kipenzi




Na Makgosi Letimile

Mnamo mwaka wa 2016, baada ya kuishi miaka 33 kama mwanamke asiyekuwa na ulemavu, niliamka nikiwa nimelazwa hospitalini siku moja na nikatangaziwa kwamba nimepata ulemavu ambao nitaishi nao kipindi chote kilichobaki cha maisha yangu, sikujua cha kutarajia ila nilikuwa na dhana ya kwamba ya kwamba halitakuwa jambo kubwa sana kuishi kama mwanamke mwenye ulemavu, kisha nikatoka hospitalini na kwa mara moja nikagundua ya kwamba dunia hii ilikuwa sio mahali ambapo ningeweza kufika kila nilipotaka. Sikuwa tayari kwa namna ambavyo hali hii ingebadilisha uzoefu wangu wa ulimwengu na bila shaka sikudhani ya kwamba mabadiliko haya yangekuwa na athari za kujumuisha masuwala ya mahusiano ya kimapenzi na hata yale ya ngono pia.

Niliingia kwenye mtandao wa Twitter ili kulalamikia jinsi ambavyo kulikuwa na upweke mkubwa katika ulemavu na mtu ambaye hata hatukuwa tunafahamiana akajibu kwa mara moja, "Lakini mbona mtu yeyote yule atake kuwa na wewe? Wewe ni mlemavu." Jibu hili limenasa kwa hakika ukosefu wa habari na hata pia madhara ya kasumba za wanaojiweza, ukiwa huu ni mtazamo ambao watu wengi sana ulimwenguni huuchukulia kama ni wa kawaida. Kama mwanamke mwenye umri wa kwenye miaka yake ya 30, akiwa sasa anakuwa kwa ndani yake mwenyewe na ujinsia yake kama mtumizi wa hivi punde wa kochi la walemavu, niliamuwa kuibadilisha mitazamo iliyokithiri. Nilanza kufanya mapitio ya vifaa bandia vya kuchezea ngono kwa wanawake wenye ulemavu. Kama dunia ilikuwa na ujasiri wa kututangaza kwamba hatuna manufaa, kwa kufanya hili ningekuwa ninachangia mapambano ya kusema kwamba sisi bado tuna maana. Hii ndiyo

kwa sababu Wheelsntoys iliundwa, kuhakikisha ya kwamba wanawake wenye ulemavu wanapata raha na kuweza kujitunza kibinafsi, na kwamba haya yanapata nafasi muhimu katika mijadala kuhusu haki za binadamu na haki. Kama mfanyi kazi ya ngono mwenye ulemavu, masuala yangu ya ngono ni muhimu na yasichukuliwe kama mawazo ya baadaye.

Ngono ni kitu ninachopenda sana kuzungumzia, kushiriki mimi mwenyewe na hata na watu wengine, ila kwa idhini yao, kwa kweli. Ninapenda kuwazungumzia na watu kuhusu ngono. Ninapenda kujua ni nini huwafanya kupata raha ya dhati. Huwa nasema sio bahati au kutokusudia kabisa eti kwamba mimi hutumia wakati wangu mwingi kuhubiri juu ya ngono kwa watu wenye ulemavu, haswa wanawake wenye walemavu kwa sababu ule uwepo tu wa wanawake wenye ulemavu tayari ni uzoefu ambao kwa mara nyingi huwa ni wa kutengwa na tena ni wa upweke mkubwa ambao unatuondoa utu. Watu wasio na ulemavu ni wepesi kutukumbusha kuwa ulemavu wetu sio shida wanayotaka kushughulikia ikiwa wanaweza kuepukana na majukumu kama hayo.

Nataka ulimwengu ukumbuke kila wakati kwamba wanawake walemavu pia wanastahili kuwa sehemu ya mijadala kuhusu ujinsia. Ni sehemu ya kile uzoefu wa mwanadamu unahusu. Nyimbo na fasihi isiyo na mwisho imejitolea kuijadili mada hiyo. Hadithi na sumulizi za ngano zinashindana katika kuunda uelewa wetu wa mapenzi na hamu. Siasa za kuheshimika na ulimwengu wa mfumo dume unataka kuweka yake madai juu ya ufahamu wetu, na uhusiano na, ujinsia wetu. Ninakutana na haya yote kama mfanyakazi wa ngono mwenye ulemavu anayejitambulisha mwenyewe kibinafsi. Ile haya ambayo tunahisi wakati tunapoanza kufanya mazungumzo juu ya ngono, mara nyingi inachangiwa kuzidishwa na aibu ambayo wengi wetu tumefundishwa kuwa nayo kuhusu miili yetu na hamu tunazozihisi. Kwa kuacha mawazo haya ya kujichukia mwenyewe na kutoa aibu zetu, tunachukua udhibiti wa miili yetu na raha.

Sijawahi kuacha nipitwe na fursa yoyote ya kuzungumza kuhusu jinsi ambavyo Wheelsntoys ilivyoanza. Jibu langu huwa ni kubwa na madhubuti kila wakati, "Kwa sababu mambo ya ngono ya walemavu ni muhimu." Tuko hapa. Sisi ni walemavu na sisi ni viumbe vya ngono. Mimi huwa kila mara kwenye Instagramu na Twitter nazungumza juu ya ngono, nacheka juu ya ngono, na ninakuwa pale kuhusu ngono. Ninapendekeza ujiunge nami haswa ikiwa wewe ni mlemavu na hauna uhakika juu ya maisha ya ngono yenye kutosheleza. Tunaweza kujifunza pamoja



## Kuimulika Ruzuku ya Haki za Walemavu almaarufu Disability Rights Fund (DRF) - Esther Kyozira, Afisa wa Programu

**Feminist Republik (FR): Disability Rights Fund ni Ruzuku inayoanza ya kipekee na isiyo ya kawaida katika ufadhili wake wa haki za walemavu, uanaharakati, na programu. Je, ni mitazamo ipi na uelewa upi wa kina uliushawishi mfuko huu katika kutanguliza kwake kwa watu na wanawake wenye ulemavu?**

**Esther Kyozira (EK):** Nadhani swali hilo linafupishwa zaidi na kauli mbiu ya harakati: hakuna chochote kutuhusu bila sisi kuhusishwa. Wakati Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu almaarufu Convention on the Rights of Persons with Disabilities ulipounda mfumo wa sheria kwa kikundi kikubwa zaidi cha watu walio wachache duniani kushiriki katika kufanya maamuzi, asasi ya Disability Rights Fund ilizaliwa ili kuzifadhili juhudi hizo na iliundwa kupitia ushirikiano kati ya wanaharakati wa walemavu na wafadhili. Wakati wafadhili wengi niliowasiliana nao kwa miaka mingi huongea juu ya haki za binadamu na usawa huku wakishikilia kwa nguvu uwezo na mikanda inayodhibiti mikoba ya pesa, utoaji wa ruzuku katika DRF unategemea mtindo shirikishi ambao unaegemeza utoaji wa maamuzi kwenye mikono ya watu wenye ulemavu wenyewe.

Tunashukuru kutambuliwa kwa mfuko wa Disability Rights Fund kama mfano wa ubunifu. Tunalotaka tu ni kwamba utoaji shirikishi wa ruzuku, unaojumuisha, na wenye kukutanisha usingeonekana kuwa wa kipekee ila ndiyo ingekuwa kama sheria ya kawaida! Ingawa harakati za walemavu ulimwenguni zina nguvu za watu bilioni moja, ni asilimia 3 tu ya ufadhili wa haki za binadamu duniani na ufadhili wa maendeleo ya kimataifa ndio huenda kwa watu wenye ulemavu. Jambo la kuongezea ukosefu huo wa na usawa hata zaidi ni ukweli kwamba ni 1.5% tu ya ufadhili wa haki za wanawake na wasichana huwalenga wanawake na wasichana wenye ulemavu, ingawa katika idadi yetu sisi kuna ni mmoja wetu baina ya kila wanawake watano. Hii, licha ya ukweli kwamba wanawake wenye ulemavu wanapata hatari kubwa zaidi za vurugu, umaskini, kutengwa kiuchumi, na aina zingine za ubaguzi. DRF imejitolea kusaidia juhudi za wanawake wenye ulemavu kutetea haki zao. Tunafanya hivyo kwa kutumia lensi ya kijinsia ya muingiliano kutoa ruzuku, kwa kuwafikia wanawake na wasichana wenye ulemavu kutoka kwa jamii zilizotengwa zaidi na wale walio na tambulisho zisizo za walio wengi na ujinsia (kama makabila madogo, wakimbizi, au watu wa LGBTQI), kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote anayeachwa nyuma.

Kama vile ambavyo DRF imekuwa na kushikilia nafasi ya mfadhili mkubwa zaidi kuliko wengine wote wa wanawake wenye ulemavu kote ulimwenguni miaka inavyoendelea kupita, ndiyo jinsi ambavyo pia harakati ya nchini Uganda imeendelea kukuwa kwa idadi, ufikiaji na anuai. Awamu ya hivi karibuni zaidi ya utoaji wa ruzuku nchini Uganda ilikuwa na matokeo ya kuwa yenye idadi ya juu zaidi kuwai kutokea ya maombi kwa ujumla na haswa kutoka kwa mashirika ya wanawake wenye ulemavu. Waruzuku wa DRF wanaowakilisha haswa makundi yaliyotengwa, kama vile wanawake wenye ulemavu wa kisaikolojia na watu wa LGBTQ wenye ulemavu, yanazidi kudhihirika wazi na pia yanaendelea kujijengea uwezo wa kujihusisha katika utetezi wa haki.

**FR: Je, ni msaada na mshikamano wa aina gani ndio Mfuko huu unatoa kwa wanawake wenye ulemavu katika kipindi hiki cha janga la COVID-19?**

**EK:** Kabla ya janga hili, DRF ilikuwa inafadhili mashirika ya wanawake wenye ulemavu ili kuchangia juhudi bunifu za kumaliza ukatili wa kingono na kijinsia (SGBV), kufanya utetezi wa sera, sheria na bajeti ili kukuza haki zao za afya ya kijinsia na uzazi, na kujenga harakati za asasi za kawaida za haki za wanawake ambazo ni jumuishi zaidi ili kuhusika katika utaoaji wa maamuzi ambayo yanahusu maisha yao. Mashirika ya womn na wasichana ambayo hupokea ruzuku za DRF yameendelea siyo tu na juhudi zao za kutetea haki zao mnmo mwaka uliopita, wanaongoza katika njia hii. Juhudi hizi zimeweza kujumuisha:

- Kuunda mikataba ya maelewano (MOU) na polisi wa kitaifa na wa mitaa ili kuhakikisha njia zinazopatikana za kuripoti, upatikanaji wa haki, na huduma zinazojumuisha kwa waathirika wenye ulemavu
- Kubadilisha mitandao ya usaidizi wa rika kuweza kupatikana kwenye mazingira ya mikondoni
- Kuongeza uelewa juu ya UWAKI unaowakumba wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kisaikolojia na ulemavu wa kiakili wanaoishi katika taasisi mbalimbali
- Kushiriki katika Mkutano wa Usawa wa Vizazi na mashauriano ya Beijing + 25
- Kushirikiana na mashirika ya kawaida ya haki za wanawake ili kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana wote
- Kuwashirikisha washiriki katika wavuti wa webina za mazungumzo ya mkondoni kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na kingono almaarufu SGBV, na haki za afya ya kijinsia na kizazi – almaarufu SRHR
- Kushiriki katika hafla za utetezi wa kiwango cha juu (COSP, CSW, n.k.)
- Kutetea mipango ya kujumuisha jamii na migao ya bajeti ya kutosha
- Kuchukua majukumu ya ushauri katika mikutano ya kawaida ya kifeministi, kama vile mipango ya uangalizi – almaarufu the Spotlight Initiatives;

## Kuimulika Ruzuku ya Haki za Walemavu almaarufu Disability Rights Fund (DRF) - Esther Kyozira, Afisa wa Programu

• Kutoa taarifa kwa CEDAW, na vile vile kujumuisha sauti za WGWD katika kuripoti kwa CRPD
• Kuendelea na utetezi unaoendelea kwa kushirikiana na vikundi vya haki za wanawake, kama vile kupitisha kwa sheria inayosubiriwa ya VAWG nchini Indonesia (bila vifungu vya kibaguzi kwenye Kifungu cha 104)
• Kuhakikisha kuwa serikali na watendaji wa kibinadamu wanapeana kipaumbele kwa upatikanaji wa SRHR katika majibu ya janga
• Kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu wanaopitia SGBV

**FR: Je, fursa gani ambazo Ufadhili huu unaoziona zilizopangiwa hapo mbeleni ambazo zitahakikisha kwamba wanawake wenye ulemavu wamepata usaidizi wa kutosha kutoka kwa wafadhili na jamii kwa ujumla?**

**EK:**
• Ulengwaji wa kimakusudi na uhamasishaji wa wanawake wenye ulemavu.
• Utetezi wa kimkakati ili kupambana na kasumba na unyanyapaa dhidi ya wanawake wenye ulemavu.
• Kukuza upatikanaji wa huduma zenye usawa kwa wanawake wenye ulemavu bila ubaguzi
• Usawazishaji wa fursa kwa wanawake wote bila kuzingatia ulemavu ambao mtu anao
• Kuthamini utofauti na haki kwa kila mtu kwa misingi ya usawa

**FR: Je! Unaweza kutuelezea kwa ufupi juu ya mawazo uliyo nayo ya 'kuhamasisha' maswala ya haki ya ulemavu katika harakati pana ya wanawake?**

**EK**:
• Kukuza uhamasishaji juu ya haki za wanawake wenye ulemavu kwa harakati pana ya wanawake
• Kuwawezesha wanawake wenye ulemavu kuweza kupeana changamoto kwa wanawake wengine katika harakati pana za wanawake
• Kujenga umoja na mashirika ya wanawake wenye ulemavu na mashirika ya kawaida ya wanawake
• Jitihada za makusudi zilizoanzishwa na wafadhili kuwa na miongozo ya ufadhili inayojumuisha ambayo inalenga wanawake wenye ulemavu.
• Kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa asasi kuu na mashirika ya wanawake wenye ulemavu kusaidia kupatikana kwa maeneo bora na uwezo mwingine wowote unaohitajika na vikundi vyote kuthamini mahitaji na haki na utofauti katika ubinadamu.

**FR: Je! Ni maneno gani ya kutia moyo unayoweza kushiriki na wafadhili wengine ambao wamekaa kwenye uzio na hawajafikiria juu ya wanawake wenye ulemavu wala kutoa kipaumbele kufadhili kazi na uanaharakati wa wanawake wenye ulemavu?**

**EK:** Wafadhili wengine wanahitaji kutambua ubaguzi mara mbili unaowakumba wanawake wenye ulemavu. Kwanza, kama wanawake, na pia kama wanawake mwenye ulemavu. Vikwazo vya kijamii ambavyo vinazuia ushiriki wao wa kikamilifu, ule unyanyapaa wa kuishi na ulemavu, mapungufu ya kimazingira ambayo yanazuia ufikiaji, na usambazaji wa habari jumuishi yote kwa makusudi huwaacha wanawake wenye ulemavu wakisalia kwenye orodha inayojumuisha vikundi vilivyotengwa zaidi katika maendeleo na jamii. Wanawake wenye ulemavu mara nyingi hutengwa bila kupewa nafasi ya kushiriki katika kufanya maamuzi na maendeleo kwa kisingizio kuwa ni vigumu sana kuwafikia, ni ghali sana kwa watu mipango ya kawaida, na kwamba mahitaji yao yamejaa matatizo mengi magumu. Mashirika yao yamehesabiwa kama yaliyo na hatari kubwa kwa sababu mara nyingi wao huwa hawana hamasisho kuhusu mifumo ya kisasa ya mashirika katika kiutawala, kifedha, na uwezo wa usimamizi – yote ambayo huhitajika na wafadhili. Wafadhili wanahitaji kuwa na ujasiri wa kukumbana na hatari hizi ili kuwapa wanawake wenye ulemavu fursa ya kudhihirisha uwezo wao kamili kwa kuwapa misaada ya kifedha na ujengaji wa uwezo unaohitajika. Kwa mfano, katika DRF, kupitia mfuko wa kujenga uwezo almaarufu Uganda Capacity Fund, tunayatambua mashirika yanayoibuka na ambayo hayana mifumo na sera na tunawasaidia kukua hadi kiwango kinachowawezesha kushindana na wengine katika kupata ufadhili wa kawaida. Hii imechangia kupata mashirika zaidi ya wanawake katika uwanja wa utetezi ambapo wafadhili wengine wanawapata. Ikiwa wafadhili wanaogopa hatari zinazohusika, wanaweza kuanza kwa ruzuku ndogondogo na kuendelea kuongezea wakiyajenga mashirika haya.

Kabla ya kutostahilisha shirika la wanawake wenye ulemavu, wafadhili wanapaswa kuuliza: Je! Kuna hatari gani fiche ya KUKOSA kulifadhili shirika hili la womn wenye ulemavu? Utastaajabishwa na kile uwekezaji mdogo unaweza kufanya mara tu utakapotumika kufanya kazi na wanawake wenye ulemavu.



# Maana ya Haki za Walemavu Kwangu Mimi

NA STELLA NKHONYA

Haki ya kifeministi kwa walemavu inamaanisha kuwa kuna nafasi ambapo wanawake na wasichana wenye ulemavu wanahesabiwa na kujumuishwa katika nyanja zote za maisha. Nafasi ambayo hakuna mtu anayeachwa nyuma katika ajenda ya maendeleo ya nchi.

Wanawake na wasichana wengi wenye ulemavu wa afya ya kiakili wanakabiliwa na ubaguzi katika nafasi zao za familia. Wanatendewa vibaya au kunyanyaswa, hata kama wangali watoto na hubaki katika hali ya kuweka unyanyapaa ndani ya roho zao. Ukosefu huu wa usalama au nafasi salama ndani ya familia zao na jamii, kati ya watu wanaowategemea kupata rasilimali na usalama, kunaweza kuchangia kupungua kwa uwezo wa kukabiliana na mafadhaiko baadaye maishani.

Kupitia vikao vya ushauri, kazi ninayoifanya inakusudia kupunguza visa vya kujitoa uhai wenyewe miongoni mwa waathirika wa unyanyasaji. Pia kuna programu katika shirika letu zinazoruhusu wanawake na wasichana wenye ulemavu kuzungumza waziwazi wanapokuwa hatarini. Tuna afisa wa ulinzi anayepokea ujumbe kutoka kwa watoa taarifa katika jamii. Anawaunganisha waathirika na wadau husika ili waweze kupata haki ya msingi.

Kama sehemu ya njia yetu ya kusema na kutenda, katika jamii tunayofanya kazi nayo, tumeunda vikundi vya wanawake na wasichana wenye ulemavu ambao hukutana mara mbili kwa wiki. Katika mikutano hii, wanajadili maswala ya afya ya kiakili. Kwa kuongezea, tunazidisha kuzingatia ustawi kwa, kama vile, kushiriki matendo na mazoezi kadhaa ambayo yanaweza kusaidia kupunguza mafadhaiko. Mikutano hii pia inajumuisha mazungumzo kuhusu maswala ya shughuli za kuleta mapato.

Kuzungumza juu ya ujinsia kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu inachukuliwa kama mwiko. Hata katika sekta ya afya, watoa huduma wana mtazamo hasi ambao unakatisha tamaa wanawake na wasichana wenye ulemavu kutembelea vituo hivyo. Mila na tamaduni zenye madhara na zilizopitwa na wakati zinakuza imani kwamba wanawake na wasichana wenye ulemavu hawana uwezo wa kufanya mapenzi. Mtu mwenye ulemavu akiwa mja mzito, mara nyingi huulizwa maswali yanayodhalilisha kama, "Nani aliyekufanyia hivi?". Kwa hivyo, kuondoa wakala wao kabisa.

Katika muktadha wa nchi ya Malawi, Afya na Haki za Kijinsia na Uzazi (SRHR) kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu hazieleweki kwa sababu wanaonekana kuwa hawana uwezo wa kujiamulia na kukubali vitendo vya ngono. Kwa kushangaza, na katika hali ya kusikitisha, wanawake na wasichana wenye ulemavu wakati mwingine huchukuliwa kama vifaa vya ngono katika tamaduni zingine ambapo wanaume walio na VVU na UKIMWI huwabaka ili 'kusafishwa' kondoa virusi hivyo. Dhana hizi potofu, pamoja na ukosefu wa elimu ya ngono, zinaweza kuwafanya wanawake na wasichana wenye ulemavu kuwa katika hali hatarishi zaidi na hawawezi kufanya maamuzi sahihi juu ya ujinsia wao.

Zaidi ya haya, COVID-19 imeongeza zaidi shida zilizopo, kwani watu wengi wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na mimi, wameshindwa kupata huduma muhimu. Sababu nyingi tofauti zimepelekea kuwepo kwa hali hii, ikiwa ni pamoja na umbali, ukosefu wa vifaa vya kinga ya kibinafsi (PPE), na kanuni za kudumisha umbali wa kijamii ambazo huwazuia watu wenye ulemavu ambao hawawezi kusafiri peke yao kutoka kupata huduma zinazopatikana mbali nao. Ukosefu wa upatikanaji wa habari pia ilikuwa sababu inayochangia, kwani watu hawakuweza kujua ni wapi wangepata msaada kutoka kwa wadau, serikali, au njia zingine zinazopatikana.

Iwapo COVID-19 imetufundisha chochote, ni kwamba kuna haja ya kutetea maendeleo ya sera ambayo inazingatia walemavu, ili ufikiaji ujengwe katika njia ya maendeleo ya jamii yetu. Tunahitaji pia kutetea uwakilishi bora na wa maana zaidi wa wanawake na wasichana wenye ulemavu, ili tuweze kutumia majukwaa yaliyopo kukuza sauti za watu walio katika mazingira hatarishi zaidi katika jamii.

Funzo jingine kutoka kwa COVID-19 ni umuhimu wa kujitunza mwenyewe kibinafsi na kukuza ujasiri, kwa namna zote mbili kama wanaharakati na pia kama wanadamu. Ingawa kuna Mashirika mengi ya Kiraia (AZAKI) nchini Malawi ambayo tunaweza kushirikiana nayo, mengi ni ya kutumia mwingiliano ulioko mkondoni, na kwa hivyo haufikiwi na watu wengi. Hili ni jambo ambalo linahitaji kubadilika.

Kwa mimi mwenyewe, ninahakikisha kuwa nina wakati wa kupumzika. Ninahakikisha kuwa ninapeana kipaumbele wakati na watu ambao wanaweza kunishikilia nafasi salama. Kwa uthabiti wa muda mrefu na msaada (kwangu mwenyewe na kwa wengine), pia ninahakikisha kuwa mimi ni sehemu ya nafasi za maendeleo na mikutano katika jamii yangu.


# Ishara Zinapozungumza Kwa Sauti ya Juu Zaidi Kuliko Maneno!!!

**Mimi si mlemavu, nipo wa karibu na ninajiweza,
Neno muhimu ni kwamba ninaweza,
Ingawa watu wengi zaidi wangependelea kuweka lebo.
Mimi kuwa kiziwi siyo kwamba sina uwezo
Mimi ni kiziwi ila mikono yangu huongea.
Kutumia ishara yangu naweza kufika vilele vya juu zaidi.
Ulimwengu ninaoujua nitaubadilsiha,
Plastiki hadi karatasi ninaweza kubadilisha,
Ingawa mimi ni kiziwi lakini ulimwengu utanisikiza,
Na niutunze na hadhi yangu kiziwi,
Na kwa hivyo, unanikumbatia kwa hiari,
Ninapoendelea kujifunza kukubali udhaifu wangu mwenyewe.**

**Mikono yangu ni ya kusudi nyingi,
Tofauti kabisa na muonekano wa juu juu,
Inafunga na kukunja na kukata na kutawala,
Ndiyo sauti yangu na chombo changu.
Sina uwezo wa kuisikia dunia, ila naiona kwa uwazi kama mchana,
Binti kiziwi mwenye mfuko na pia njia,
Njia ya kuyabadilisha maisha yangu na yako,
Na hata huenda akauondolea Ulimwengu vidonda vyake vya plastiki.
Sina suluhu kwa matatizo yote,
Ila najua ya kwamba sharti nianze,
Na licha ya lolote litakalotokea,
Utaona mfuko wa karatasi na tabasamu kwenye moyo wangu.**

**Ni heri lugha zetu ziunganishe,
Pamoja tunaweza kuvishinda vita hivi.
Ni heri tuibadilishe na kuondoa hii mifuko ya plastiki,
Saidia na Kuunga mkono mifuko ya karatasi ya Teki,
Ingawa njia inaonekana kuwa yenye giza totoro,
Katika nchi ya Uhabeshi tunaweza kuwa na athari si haba.
Ni fursa yetu kuchukuwa nafasi ya kuwa watangulizi.
Kwa viziwi, tafadhalini, naomba mnipe sikio.
Nafasi ambayo lazima tuione,
Kwetu sisi ajira hizi huwa zina umuhimu mkubwa.
Kwa pamoja wacha tuwe ndio mwangaza,
Siku zetu za usoni zinaweza kuwa zenye mafanikio.**

**Limetungwa kwa upendo na Familia ya Teki**



> LICHA YA SISI KUTENGWA KUTOKA KWENYE PROGRAMU MUHIMU KATIKA HUDUMA ZA AFYA ZINAZOZINGATIA VIJANA, TUNACHUKUA HATAMU YA KUTWAA MAMBO MIKONONI MWETU ILI KUYASHUGHULIKIA MAPUNGUFU HAYA.

# AFYA YA KINGONO NA UZAZI NI ZAIDI YA MAWAZO YA BAADAYE KATIKA AFYA YA UMMA

– NA FATIMA KALIMA

Afya ya uzazi na ya kijinsia ina maana ya kwamba watu wana maisha ya ngono yenye uwajibikaji, yenye kuridhisha, na salama na kwamba wana uwezo wa kufanya hivyo. Hapa Malawi, afya ya uzazi haifikiwi, haswa kwa watu wenye ulemavu. Sababu kuu ni kwamba wafanyikazi wa afya mara nyingi hawajui changamoto halisi ni nini kwa sababu hawafanyi juhudi ya kuwafikia wahusika. Kwa muktadha, nchini Malawi, tuna mashirika mengi yasiyo ya kiserikali ambayo yanatekeleza mipango ya huduma za afya rafiki kwa vijana. Lakini vijana wenye ulemavu mara nyingi hutengwa kwenye miradi hii. Kama matokeo, mahitaji ya afya ya kijinsia ya watu wenye ulemavu bado hayajatimizwa. Mahitaji haya yanaweza kuanzia upatikanaji wa habari hadi utoaji wa huduma za kliniki na vituo vya afya ambavyo ni rafiki kwa walemavu, ambapo bila huduma kama hizi watu wenye ulemavu hawawezi kupata huduma za afya ya kijinsia na uzazi kwa urahisi.

Licha ya kutengwa na programu muhimu kwenye huduma za afya zinazozingatia vijana, tunachukua mambo mikononi mwetu kushughulikia mapungufu haya. Kwa mfano, tulifanya mafunzo yaliyolengwa kwa wanawake wenye umri mdogo na mbao wana ulemavu ambapo habari juu ya afya ya uzazi na ngono ilifanywa kupatikana katika mifumo ya aina nyingi ili kuhakikisha hakuna mtu aliyeachwa nyuma. Tunatumia pia programu za redio kwa ufikiaji wa jamii ili kuzungumza juu ya afya na haki za ngono na uzazi, almaarufu Sexual and Reproductive Health Rights (SRHR).

Tunazingatia viwango vya kuelewa kuwa kuna maoni kadhaa yaliyo potofu kuhusu kuishi na ulemavu na afya na haki ya ngono na uzazi, mengine ambayo yanashirikiwa na watu wenye ulemavu wenyewe. Katika visa vingine, dhana hizi potofu zinahusiana na habari potofu juu ya ngono au wasiwasi wa kimsingi kuhusu VVU na UKIMWI na maambukizo ya zinaa. Yote haya yamefungamana na kuwepo kwa elimu ya ngono yenye matatizo na / au elimu ya ngono ambayo haizingatii mahitaji ya watu wanaoishi na ulemavu.


Kazi ambayo shirika letu linafanya katika kuziba pengo hili haswa ni muhimu sana kwa sababu wanawake na wasichana wana hatari ya unyanyasaji wa kijinsia. Tunataka kuonyesha njia ambazo elimu duni kuhusu haki za ngono inaweza kuongezea hatari hii zaidi au kuwatenga watu walio katika mazingira hatarishi. Wakati ambapo wasichana na wanawake wenye ulemavu wananyanyaswa na walezi wao au wale wenye uhusiano wa karibu nao, shirika letu linatumia elimu ya SRHR kuwapa waathirika habari kuhusu rasilimali wanazoweza kupata.

Kuwasili kwa janga la COVID-19 kulimaanisha kuwa watu wenye ulemavu wamepata na kushuhudia changamoto zinazozidi kuwa ngumu, haswa wanawake wenye umri wa chini wenye ulemavu. Kuongezeka kwa msukumo kwenye mfumo wa huduma ya afya kulimaanisha kuwa uwezo wa hospitali na kliniki kutoa huduma za afya ulizidi kupunguka. Athari za hali hii kwa wanawake aliye na ulemavu imekuwa ni ukosefu wa upatikanaji wa habari na huduma ambazo tayari hata awali wamekuwa na wakati mgumu wa kuzipata kwa sababu hawajawekwa kwenye nafasi ya kipaumbele na kuzingatiwa kwenye programu zilizoundwa kushughulikia mapungufu ya afya ya umma. Kwa mfano, ikiwa wanawake aliye na ulemavu alijitahidi kupata vituo vyenye ujumuishaji ambavyo vinatoa huduma za uzazi wa mpango au utoaji mimba salama, shida hii ilizidishwa na janga hili na kuongezea zaidi, alikuwa kwenye hatari ya kupuuzwa kama shida kubwa wasiyotaka kuishughulikia.

Nchini Malawi, watu huwa wanafikiria kuwa ulemavu ni mzigo kwa familia, na, wakati mwingine, wanahusisha ulemavu na uchawi. Yote haya yanaweza kuchangia mtazamo wa jumla ambao unawapelekea watu kuzingatia haki za walemavu kwa kutumia mfumo wa hisani akilini mwao. Imani ya msingi hapa ikiwa ni kwamba watu wenye ulemavu wanahitaji msaada ili kuishi katika jamii, badala ya kujitolea kuifanya jamii kwa ujumla iwe jumuishi zaidi.

Mtazamo huu uliokita mizizi na tabia ya kuchukulia haki za walemavu na haki kama mawazo ya baadaye, ina maana kwamba hakuna njia maalum au zilizodhihirika kuwa ni muhimu sana ambazo serikali imetumia kujibu mahitaji ya jamii ya walemavu wakati huu wa janga la COVID-19. Serikali ya Malawi, kama serikali nyingi ulimwenguni, imeshindwa kutoa miundo mbinu ya usalama kwa mamilioni ya watu ambao wanakabiliwa na mazingira magumu hatarishi ambayo hayajawahi kutokea awali.

Jibu langu la kibinafsi kwa hali hii limekuwa kuona ulemavu wangu kama nafasi ambayo inaniruhusu kuwasiliana na jamii yangu na kuwasaidia kuelewa ni nini jinsi ambavyo taswira ya haki za walemavu na haki inaweza kuonekana. Ulemavu wangu ni jukwaa ambalo ninaweza kutumia kuwahamasisha wenzangu wenye ulemavu kutetea haki zao za kuishi maisha kamili na, jambo la muhimu, huduma za afya ya ngono ambazo zinawaweka katika nafasi ya kipaumbele.



## ULEMAVU WA KUONA

Akili zangu zimeamka katika ulimwengu ambao watu wanaweza kuona tu kwa mwili. Macho yangu hata hivyo ni kupitia hisia zangu, mguso, harufu na sauti. Ni zawadi yangu sio maumivu yangu. Mimi ni hai na ninaweza kuona wazi.

Miseda_Art

# Fumbo la Haki za Walemavu

NA ZANELE MBUGUA

**Wiki ya Uhamasishaji wa Usiwi - upofu 21 - 27 Juni: Kuna ukosefu mkubwa wa ufahamu wa wale walio na usiwi - upofu, watu ambao ulemavu wa kusikia na pia kuona. Wakati wa janga la Covid-19 ambapo watu wanashauriwa kukaa nyumbani, kufanya kazi kwa mbali na kudumisha umbali wa kijamii, huku wapendwa, wapenzi na waajiriwa wenza na marafiki wanapounganishwa kwa jumbe za maandishi, simu za video, barua pepe na mitandao ya kijamii; ulimwengu kwa wale wenye ulemavu na haswa upofu wa viziwi unazidi kuwa wa kutenga.**

**1.Je, jukwaa la Feminist Republik lilizundua lini toleo la kwanza la jarida la Dzuwa?**

**2.Katika kipindi cha Covid-19, ni nini ambacho Tariro anakielezea kama "zawadi na pia uchungu" kwa wakati mmoja?**

**3.Ni makundi mangapi ya womn wenye ulemavu ambayo shirika la UAF – Afrika liliwasaidia wakati wa kilele cha Covid-19 mnamo mwaka wa 2020? Kutoka kwenye nchi zipi?**

**4.Taja mila tatu ambazo Florence /Khaxas anazielezea katika Fungua Roho Yako: Mila na Tiba katika Haki za Ulemavu?**

**5.Je! Jina la kitabu kilichotajwa na Minna Salami ni nini?**

# MAONI KUTOKA KWA TOLEO LETU LA KWANZA LA DZUWA




"Formidable! Merci pour ce partage pour nous les francophones il y a des difficultés de pleine participation et d'accès à toutes le informations. Mais nous sommes engagées pour l'atteinte des objectifs nobles de Feminist Republik. Ensemble nous bâtirons un monde meilleur pour tous, mais surtout pour les femmes.Merci bien." – Florence Ouattarra

Translation:
"Ajabu! Asante sana kwa kushiriki kwetu sisi wa kutumia lugha ya Kifaransa kuna ugumu wa kushiriki kikamilifu na kupata taarifa zote.
Lakini tumejitolea ili kufanikisha malengo ya kibusara ya Feminist Republik
Kwa pamoja tutaunda ulimwengu ulio bora kwa kila mtu, lakini haswa kwa wanawake.
Asante."

"Ajabu kabisa! Asante kwa kushiriki! Heshima za kutosha!!!!" – eloise Burke (Aliyechangia uandishi wa Dzuwa)

**Naipenda hii" – Vuyela K Lindiwe (kupitia Facebook)**

"Nina furaha iliyoje ya kwamba nilishiriki kwenye kampeni hii ya kupendeza sana, asante sana kwa ushirikiano mwingi zaidi wa maana katika siku zijazo" – Elizabeth Maryann



# UKURASA WA WALIOCHANGIA



**Agness Chindimba** ni Msomi aliyefadhiliwa kupitia wakfu wa Mandela Washington (2016) kwa viongozi wa Kiafrika wenye umri mdogo, mwanaharakati wa haki za walemavu na vile vile mwanaharakati wa haki za wanawake. Agnes ni mfeministi na ana shauku kubwa kuhusu masuala ambayo yanawaathiri wasichana na wanawake wenye ulemavu. Amehitimu na shahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Afrika kupitia udhamini wa Umoja wa Afrika.

**Twitter :** @deafwomenzim
**Facebook :** https://www.facebook.com/deafwomenincluded
**Tovuti :** https://www.deafwomenincluded.org/




**Amisa Rashid** ni mwanasaikolojia mshauri nasaha na pia mpatanishi ambaye umaarufu wake ni kwa kujenga amani na uponyaji wa kiwewe. Yeye ni Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Wakfu wa Nivishe ambayo lengo lake kuu ni kujenga udhabiti wa jamii kupitia programu zilizoshawishika na kiwewe ili kufikia amani na uwiano wa kijamii kayika jamii yake kwa kuunda nafasi salama na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waathiriwa wa ukatili. Huku akiwa mtu binafsi anayethamini ujumuishaji ametanguliza Nivishe katika utoaji wa huduma za Afya ya Kiakili kupitia lugha ya ishara. Shauku yake kuu na kuchangamkia kwake katika kazi za jamii zilimfanya kuibuka wa pili mnamo mwaka wa 2019 katika tuzo muhimu ya kila mwaka ya Wanubi Afrika Mashariki almaarufu EANA – East Africa Nubian Awards. Yeye ni mshauri mtaalamu katika baadhi ya asasi kama Kamilimu, Akilidada and Akirachix ambazo huwasaidia vijana kutoka kila maeneo na asili nchini Kenya, haswa womn wenye umri mdogo katika STEM – masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na isibati.

**Barua Pepe:**amisarashid@gmail.com

**Agnes Hausiku** amefanya kazi kwenye mashirika kama vile la Namibian Association for Differently Abled Women na kwa sasa anasomea kazi ya jamii. Agnes kwa sasa ameajiriwa katika Wizara ya Migodi na Nishati katika mji wa Windhoek kama afisa wa utawalal katika idara ya ununuzi. Kujitolea kwake kwa kazi anayofanya nje ya ofisi yake ni thibitisho tosha ya kwamba yeye ni mtetezi shupavu wa haki za walemavu na uwezeshaji wa wanawake. Anafanya kazi na Kamati ya Kitaifa ya Olimpiki za Walemavu kwa programu ambazo zinazingatia masuala ya wanawake kwenye uongozi wa spoti n ani mmoja wa wanachama wa kilabu cha Wheel-Ability sports club jijini Windhoek, ambapo miongoni mwa shughuli zingine yeye hucheza mpira wa vikapu.



**Beauty Boois** ni mfeministi wa makutano mwenye jinsiatata. Yeye ni mwanasaikolojia mshauri nasaha, mtunzi, mwandishi wa kujitegemea na mwalimu wa yoga. Beauty pia ni mwanaharakati mkali wa haki za afya ya kijinsia na uzazi ikijumuisha uchanya wa ngono. Utunzi wake wa maandishi umechapishwa mara nyingi sana katika gazeti la Namibia, Sister Namibia, African Feminism, Monochrome Magazine, gazeti la the Namibian Sun na jarida la Elephant Journal. Utunzi wake wa riwaya ya kwanza yenye jina, Namgu's Escape Theory ilichapishwa na wachapishaji wa chou kikuu cha Namibia - University of Namibia Press mnamo mwaka wa 2020.





**Easter Okech** ni Mfeministi wa Kiafrika ambaye ni bingwa wa upangaji wa kifeministi unaozingatia makutano na vizazi. Hii inampa nafasi ya kushauri katika shule na katika ngazi ya jamii kupitia vikundi na nafasi mbalimbali. Ushiriki wake unasukuma njia inayotegemea haki za binadamu ambayo sio ya kimapokeo na kwa hivyo inasukuma dhidi ya kanuni za mfumo dume ambazo zinazuia ushiriki wa maana wa wanawake na wasichana katika ngazi ya jamii. Easter pia anaunda ajenda ya kisiasa kama mkufunzi wa wanawake katika siasa ili kuhakikisha utetezi wa bajeti una washirika wa kushinikiza ajenda ya jinsia katika serikali za ugatuzi na kitaifa. Kama mshauri, anaamini kuwa upangaji wa kifeministi ni muhimu kuhakikisha harakati thabiti ambazo zitahakikisha usawa na usawia katika ngazi zote.

**Elizabeth Mang'eni** ni Afisa Biashara Mwandamizi katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Maendeleo ya Ujasirialmali nchini Kenya, na ni mmoja wa waanzilishi wa mpango wa You4She Initiative. Amejitolea katika kazi yake kuwawezesha wanawake na wasichana wenye ulemavu kwas kukuza ujasiriamali mdogo mdogo wa mitaani, mafunzo jumuishi ya ujuzi wa kazi, na programu zinazowaelimisha watu wenye ulemavu kuhusu usimamizi wa biashara na kuweka akiba. Ana shauku juu ya Ujasiriamali kwa sababu inampa fursa ya kujaribu hatari ya kujisukuma zaidi ya uwezo wake kuona maendeleo na mabadiliko ambayo ana ari ya kuona katika jamii yake. Elizabeth ni mmoja wa wanafunzi wa zamani walionufaika na masomo jumuishi ya kitaalamu ya uajiri wa walemavu Marekani mwaka wa 2019 - US Professional Fellow Program on Inclusive Disability Employment, na pia 2018 Australian Award African Fellowship Program, na pia ya uongozi wa barubaru almaarufu Young Africa Leadership Initiative - 2017 Mandela Washington Fellowship. Kujiunga kwake kwenye ufadhili huu wa masomo umemwezesha kuipanua kazi yake kuhusu uajiri jumuishi na msaada wa afya ya uzazi kwa womn wa umri mdogo wenye ulemavu.



**Elizabeth Namaholela** Namwandi nimsimamizi wa kujitolea katika Shirikisho la Kitaifa la Watu Wenye Ulemavu nchini Namibia - National Federation of Person with Disabilities in Namibia (NFPDN) na pia katika shirika la uzeruzeru the National Albinism Association Trust (NAAT). Yeye ni womn mwenye umri wa miaka 30 mwenye ualbino, aliyezaliwa katika maeneo ya kaskazini mwa Namibia katika Kijiji kinachoitwa Omundjalala wilaya ya Ombalantu, eneo la Omusati. Kubuni mashairi na hotuba za motisha kwa watu wenye ulemavu kama njia ya kuwatia moyo ndiyo burudani lake. Anaamini ya kwamba ulemavu wetu sio kutoweza kwetu.
**Barua pepe:** namwandielly@gmail.com





**Ekaete Judith Umoh** ambaye hivi karibuni alijiunga na halmashauri ya shirika la Urgent Action Fund-Afrika ni mtetezi wa haki za walemavu ulimwenguni na mtaalamu wa maendeleo jumuishi mwenye uchambuzi wa kijuzi wa masuala yanayohusiana na jinsia, ulemavu na maendeleo jumuishi. Yeye ni mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa FACICP Disability Plus, shirika ambalo linakuza ujumuishaji wa walemavu katika juhudi zote za jinsia na maendeleo. Ekaete ni mwanzilishi wa THE PURPLE CORNER ... nafasi salama ambapo mtazamo wa kifeministi na unganishi unatumika kushughulikia unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana wenye ulemavu. Yeye kwa sasa anahudumu kama Katibu wa shirika la African Disability Forum- ADF; Naibu wa Mwenyekiti wa muungano wa mashirika ya walemavu ya Africa Magharibi almaarufu - West African Federation of the Disabled-WAFOD;(Jinsia na Haki za Binadamu), Mwenyekiti; muungano wa Disabled People's International-DPI Eneo la Afrika. Kati ya mwaka 2012 na 2016 alikuwa Naibu wa Mwenyekiti, shirika la urekebishaji, Rehabilitation International-RI kwa Eneo la Afrika.

**Faith Njahîra** ni mwanamke wa Kiafrika mwenye ulemavu na anayetumia kiti cha magurudumu ambaye ambaye anaugua kuzorota kwa misuli na aliyejitolea kufanya utafiti na kazi ya jamii akiongozwa na maadili ya haki ya ulemavu, ufeministi na upinzani wa kasumba ya kujiweza. Faith amekuwa msomi wa kujitegemea na mshauri katika masuala ya ulemavu, ujinsia, afya na elimu akifanya kazi na mitazamo ya ukutanishaji kwa miaka miwili iliyopita. Alianzisha shirika la wenye kuathirika na kuzorota kwa misuli Muscular Dystrophy Society Kenya mnamo mwaka wa 2013 kama jukwaa la kuwasaidia wenye tatizo la kuzorota kwa misuli na wapendwa wao. Yeye ni mhusika mkuu na mtayarishaji mwenza wa "For All the Brilliant Conversations", filamu kuhusu urafiki, uponyaji na kupambana na kiwewe. Kwa sasa hivi amejisajili kwa masomo ya shahada ya Uzamifu katika Kituo cha Haki za Binadamu almaarufu Centre for Human Rights katika Chuo kikuu cha Pretoria. Katika kazi yake yote anajitahidi kuhakikisha ya kuwa ulimwengu hauna raha ya kufikiri kwamba ulemavu na utofauti haupo. Muziki, asili, joto la jua na muda anapokuwa na wapendwa wake ndo vitu vinavyomletea furaha.
**Barua pepe:** njahirafw@gmail.com
**Tovuti viungo:**
https://www.linkedin.com/mwlite/in/faith-njahira-68ab5b83





**Fatima Kalima** ndiye mwanzilishi mwenza wa shirika la vijana wenye ulemavu nchini Malawi. Hivi sasa ndiye mratibu wa mipango katika Jukwaa la Maendeleo ya Vijana wenye Ulemavu, almaarufu Forum for the Development of Youth with Disabilities (FDYD). Fatima amefanya kazi bila kuchoka nchini Malawi katika miaka iliyopita ili kuboresha maisha ya vijana wa Malawi wenye ulemavu kupitia kushiriki kikamilifu katika uundaji na utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya vijana wenye ulemavu. Fatima pia hushauri vijana walemavu wa shule za upili na yeye pia hujitolea katika kufundisha watoto walemavu na vijana katika kituo cha masomo cha jamii. Fatima anaamini katika kukuza maisha ya wasichana walemavu kwa kuwahimiza kwenda shule na kuzungumza wakati wanapokumbana na changamoto na unyanyasaji.

**Florence Flora /Khaxas** ni mwandishi wa kifeministi wa Namibia, tabibu na mtetezi wa haki za binadamu wanawake. Uanaharakati wake unazingatia haki ya ulemavu, wasichana wanaotazama kubalehe na uongozi wa wanawake wwnye umri mdogo na kujulikana, wanawake wa kiasili na wa vijijini, harakati za LBTQ, VVU / Ukimwi, Afya ya kiakili, uzuiaji wa ukatili dhidi ya wanawake na wasichana - VAWG na haki ya Uchumi kwa wanawake. Florence ni mkurugenzi mtendaji wa Y - Fem Namibia Trust na pia anahudumu katika bodi na kamati mbali mbali za mashirika yasiyo ya kiserikali - NGO. Katika wakati wake asipokuwa akifanya kazi, anapenda kutazama ndege, uendeshaji wa baiskeli wa milimani na anayetaka kuwa mkulima wa muda ili kukuza usalama wa chakula na uthabiti wa uchumi kwa wanawake wenye ngozi nyeusi. Anawashauri pia wanaharakati wachanga wa kifeministi kuwa viongozi wakali wa kifeministi ambao wanabadilisha kutokuwepo kwa usawa wa nguvu, kubadilisha sera zenye madhara na kuimarisha mwonekano wa vikundi vilivyotengwa kupitia usemi wa ubunifu. Florence anaendeleza maandishi ya ubunifu miongoni mwa jamii za asili na zilizotengwa huko nchini Namibia.





**Kiko Enjani** kwa wakati mooja alitengengeza ngoma akitumia ndoo ya plastiki iliyovunjika. Kulifuatia msururu wa matukio ambao uliishia mtoto huyo mpiga ngoma wa miaka 9 kupelekwa uhamishoni katika maktaba iliyokuwa karibu. Baada ya kusoma kila kitu kilichokuwa kwenye sehemu ya hadithi za kubuni za kisayansi na ndoto, Kiko alihamia nchi mbalimbali akiandanaman na wazazi wake hadi walipokuja kutulia kwa makao ya kudumu mjini Nairobi, Kenya. Amejaribu bahati yake katika kubuni michezo ya kumpyuta, uingizaji wa data na utayarishaji wa muziki huku akiwa anasomea kozi nyingi za kubuni.



**Liz Ombati** ni mtetezi wa haki za watu wenye ulemavu. Utetezi wake unakuja kupitia uzoefu wake wa hali halisia mwenyewe na hali ya afya ya akili. Alianza kuandika kutoka umri mdogo sana, kwani ndiyo njia bora ambayo angeweza kuelezea ambayo yalikuwa yamesalia bila kutamkwa. Kuandikia kwake ni aina ya tiba. Liz anatumia uandishi kuchochea mabadiliko; kuvuta umakini kwa kutengwa, na kuangazia udhalimu unaomzunguka. Anaandika juu ya hasira iliyokithiri ndani yake na kustahirika kwa kutoweza kuufanya ulimwengu kuwa bora kwa kila mtu. Anaandika kujipata wakati ana maumivu na uchungu mwingi kwa sababu ya ndoto ambazo hazijatimizwa. Walakini, yeye pia anaandika kuelezea urembo na matumaini yanayomzingira. Sasa, ambayo ni kilele cha miaka mingi iliyopita. Liz anaandika juu ya mapenzi na hamu; kuhusu uponyaji. Anaandika juu ya kesho mpya na matumaini mapya. Kuhusu machweo na mawio. Anaandika juu ya ahadi ya ulimwengu wenye usawa. Ulimwengu salama kwetu sisi sote. Ulimwengu ambao unatutosha sisi sote; kushiriki katika ajabu na uzuri wake.

**Makgosi Letimile** ni mfanyi kazi ya ngono mwenye ulemavu, mwenye kuchangia uandishi kwenye majarida na mama ambaye anishi katika mji wa Cape Town, Afrika Kusini. Mpate katika Instagramu: Wheelsntoys ambapo anauza midoli ya kukodisha kwa sababu ya ukosefu wa ajira uliosababishwa na COVID-19.






**Melissa Wainaina** ni mfeministi wa Kiafrika mwenye jinsia kinzani anayeishi nchini Kenya. Anahusika kikamilifu katika nafasi za kifeministi za Kiafrika ambazo zinaendeleza ulinzi na usalama kamilifu, utunzaji wa pamoja na ustawi, uponyaji haki kwa wanawake na watu wasioambatana na jinsia yoyote, na vile vile mipango ya nyaraka zinazochochewa na ufeministi. Ana uzoefu zaidi ya miaka 13 katika sekta isiyo ya faida baada ya kufanya kazi tangu mwaka wa 2006 haswa akizingatia ujinsia, jinsia na haki za kijinsia. Melissa ana uzoefu mkubwa katika kuimarisha uwezo wa mbinu zaidi zenye msingi wa haki katika kazi ya mabadiliko ya kijamii ya kimageuzi. Kazi ya Melissa imehusisha kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia ambao unaathiri wanawake waliotengwa na watu wabadili jinsia. Amechangia kupanua mazungumzo hapa katika eneo la Afrika Mashariki kuhusu uponyaji wa haki. Anachunguza utumiaji wa sanaa kwa hali chanya ya mwili, kujieleza binafsi, upinzani na utunzaji wa kibinafsi na wa pamoja. Kama msanii yeye mwenyewe, anafurahia uandishi wa ubunifu, ushairi, kubuni mapambo ya mwili, ufundi na upigaji picha. Ameandika juzuu za kijinsia na ubunifu kwa kutumia majina ya ya kujibandika ya kisanii kama vile Sikiliza na Kamanzi Wainaina. Melissa anahudumu katika Bodi ya Women Spaces Africa, shirika la kijamii ambalo linakuza haki za afya ya kijinsia na uzazi kwa wasichana na wanawake wenye umri mdogo wenye ulemavu nchini Kenya.



**Michèle SOJIP** ni mwanamke wa umri mdogo ambaye aliupata ulemavu wa kupooza miguu na mikono kufuatia ajali ya barabarani ambamo alihusika miaka nane iliyopita. Michèle SOJIP aliamua kutumia hali yake ya kupungukiwa kwa uwezo wa kusonga kusaidia kuufanya ulemavu uwe kama jambo la kawaida. Alibuni ukurasa wa Facebook unaoitwa "Michèle SOJIP—Parlons de Tout" na yeye pia ni mwanzilishi na mwenyekiti wa shirika la "Handicapés et Fiers" ambalo lina kauli kuu zikiwa ni pamoja na kutambua mchango wa watu wenye ulemavu, kuzisaidia familia na haswa wasichana wenye umri mdogo na ambao wana ulemavu, na kukuza haki za watu wenye ulemavu, haswa haki ya kupata elimu. Kama matokeo ya hayo, mradi wa "My Books" ulianzishwa mnamo mwaka wa 2019 na unalenga kutoa vitabu vya kusoma kwa watoto wenye ulemavu au wale waliozaliwa na wazazi wenye ulemavu. Michèle SOJIP alihitimu na Shahada ya Uzamili kwenye somo la kuendesha kesi za kibiashara na Usuluhishi almaarufu Commercial Litigation and Arbitration kutoka katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika ya Kati, huku historia yake ya masomo ikimruhusu kufanya kazi ambayo inahusu kuendelea kuunda jamii jumuishi ambayo inasisitiza kufanyiwa haki na fursa saw ana haki. Akiwa na matumaini na huku amedhamiria, amekubali sentensi "Kila maisha inafaa kuishi" kama kauli mbiu.

**Miseda_Art/ Marylyne Jan Akinyi Miseda** ni msanii wa miaka 26 wa sanaa ya kuonekana ambaye ni mwanzilishi Miseda_Art na pia mwanzilishi mwenza wa shirika la Strokes of Magic. Biashara hii ya Marylyne Jan Akinyi Miseda ilianzishwa mnamo mwezi wa Januari 2021. Miseda_Art inazingatia mtindo wa sanaa "surrealism", sanaa dhahania, Sanaa elezi na sanaa kwenye nguo. Strokes of Magic ni darasa la sanaa la watoto ambalo linaongozwa kitaalamu.

**Barua pepe:**
janmarylyne@gmail.com Miseda_Art Instagram: miseda_art
**Miseda_Art kiungo cha IG :**
https://www.instagram.com/miseda_art/
**Kiungo cha Strokes of Magic art :**
https://www.instagram.com/strokes_ofmagic/?hl=en





**Namafu Amutse** ni msanii wa taaluma anuwai wa Namibia ambaye amejikita kwenyebaadhi ya aina za sanaa kama vile utengenezaji wa filamu, upigaji picha, usimamizi wa kuongoza na kuandika na hufanya kazi kama mpiga picha wa kujitegemea na mkurugenzi wa ubunifu. Hivi sasa anasoma kuelekea Shahada ya Heshima ya Elimu katika Kiingereza na Kijerumani katika Chuo Kikuu cha Namibia. Kazi yake inachochewa na utamaduni wa Kusini mwa Afrika, ufeministi na kuangazia siku zijazo kwa waafrika, kwa lengo la kuzingatia mitazamo kuwa na kipaumbele cha maswala ya watu weusi. Mnamo Oktoba wa 2020 alikuwa na maonyesho yake ya kwanza alipokuwa msanii peke yake yenye jina la "Macho Mkali ndani ya Afrofuturism," na mnamo Novemba mwaka huo huo kazi yake iliyoitwa 'Chrysalis' iliangaziwa katika toleo la nne la Doek, jarida la fasihi la Namibia, ambapo moja ya picha zake ilitumika kupamba jalada la jarida. Unaweza kumtazama kwenye
**Instagram** @namafu na uone kazi zaidi na nakala kwenye wavuti wake wa
**Linktree**: www.linktr.ee/namafu
**Baruapepe**: namafu.amutse@gmail.com



**Ndapwa Alweendo** amehitimu na shahada ya uzamili (MSocSci) katika Masomo ya Siasa na Masuasla ya Kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha Rhodes. Kwa sasa anafanya kazi kama mwandishi wa kujitegemea, mhariri na mratibu wa miradi wa shirika la Sister Namibia. dhamira yake ni pamoja nahistoria ya Namibia ya kifeministi ambayo kwa mara nyingi huwa imefinyiliwa, dhana muhimu ya masuala ya rangi ya Ngozi, na afya ya kiakili ya umma.

**Palesa Deejay Manaleng** alisomea uandishi wa Habari katika Tshwane University of Technology. Wakati akiendelea na masomo, alikuwa aliweza kupata nafasi ya kuhudumu kama mwandishi wa habari mwanafunzi katika shirika la Witbank News. Aliyafanyia mafunzo yake ya kazi katika jarida la the Citizen Newspaper mnamo mwaka wa 2011, kisha akafanya kazi kama mhariri mdogo katika jarida hilo la the Citizen Newspaper (2011-2013). Alijiuzulu na kuenda kuhudumu kama mwajiriwa mwanafunzi katika shirika la Wits Justice Project (2013-2014) na Clickmaths kama mwenye kutafsiri Isibati katika lugha ya Kizulu. Alifanya kazi katika shirika la eNCA (2014) kama mwandishi mdogo wa mkondoni, na akakaa kipindi kilichosalia cha 2014 hospitalini akisubiri kupona baada ya ajali ya baisikeli iliyomwacha akiwa amepooza. Mara tu alipotoka hospitalini alifanya kazi katika shirika la Global Girl Media kama mkufunzi wa uandishi wa Habari, huku akifanyia kazi Wits Vuvuzela kama mwalimu wa Kisotho (2015). Pia aliliwakilisha taifa la Afrika Kusini katika mashindano ya Kombe la Dunia ya uendeshaji wa baiskeli kwa walemavu mara 3 na amekuwa bingwa wa kitaifa kwa miaka 6 sasa. Tangu alipohusika katika ajali ameweza kushiriki katika zaidi ya mashindano 30 ikiwa fupi zaidi kuwa kilomita 46 na masafa marefu zaidi yakiwa kilomita 111. Kwa sasa yeye ni mwandishi wa habari mkondoni kwa jarida la EyeWitness News, mwanariadha wa kutumia kiti cha magurudumu na mwendeshaji baisikeli mwenye ulemavu.
**Blogi:** https://beyondaccessibility.wordpress.com






**Stella Nkhonya Chisangwala** aliugua ugonjwa wa kupooza wa polio akiwa na umri wa miaka 7. Anatumia magongo na viboko wakati mwingine kiti cha magurudumu. Alipata shahada yake ya kwanza katika masomo ya maendeleo ya jamii licha ya changamoto nyingi. Stella alianzisha shirika la kutetea haki za watu wenye ulemavu (Haki za Binadamu za Wanawake na Wasichana wenye Ulemavu nchini Malawi na ambapo yeye ndiye mratibu wa kitaifa) kuanzilishwa kwa shirika ulikuwa dhidi ya msingi wa uzoefu wa kibinafsi uliopatikana wakati wa ujauzito wa kwanza ambapo ilikuwa changamoto kupata huduma za haki ya afya ya kijinsia na uzazi. Alikabiliwa na unyanyapaa na ubaguzi muda wote katika maisha yake yote hadi alipopata tena nguvu ndani yake kupitia mafunzo kutoka AWDF. Stella ambaye ni mama wa wasichana watatu wa kibaolojia na msichana mmoja aliyelelewa anapenda kuomba, Mungu ndiye nguzo yake ya mafanikio. Stella aliteuliwa kujiunga na Kikundi cha Ushauri cha Jamii na Shirika la wanawake la UN Women na anakaa katika Kamati ya Uendeshaji katika kikundi cha utetezi cha utekelezaji wa UPR. Yeye ni balozi wa wasichana wadogo wenye ulemavu na anapenda kudensi na kuimba.

**Shinaz Ali-Zaids** ni bingwa wa haki za kijamii na mtaalam wa taaluma anuwai akiwasilisha zaidi ya uzoefu wa maendeleo wa miaka 10 unaosaidiwa na maarifa ya kisheria katika maswala ya kisiasa ya Kiafrika, haki ya mazingira na mazingira ya ufadhili. Shinaz ambaye ni Mtunzi wa Utamaduni katika jukwaa la Feminist Republik ana utaalam mkubwa wa utoaji wa ruzuku na uzoefu kwa kuwa amefanya kazi na shirika la UAF-Afrika tangu mwaka wa 2013. Asili yake ya kitaalam na ushiriki wa jamii umesaidia kukuza uanaharakati wake. Shinaz anaamini katika uongozi wa utumishi na anajihusisha na kazi ya jamii wakati wowote anapopata nafasi. Ujuzi wake wa kina juu ya hali halisi ya kuishi kwa wanawake anayejiuta akiishi kando kando ya jamii, haswa katika makazi duni ya mijini, pamoja na shauku yake ya kutumia ukumbi wa uigizaji na densi kama vifaa vya ukarabati na huduma ya pamoja imemwezesha kufanya kazi kote Afrika akijumuika na wanaharakati wasanii katika kuinua njia za haki za kifeministi na za haki za kijamii ili kufikia haki za wanawake za muda mrefu na haki ya kijinsia. Kama mbunifu, Shinaz huona kwamba kufanya mazoezi na kupika kama ni matibabu na anaamini chakula kizuri huponya mwili na roho. Yeye pia ana shauku kuhusu uhuru wa kifedha na ni mjasiriamali hodari. Katika UAF-Afrika, Shinaz imekuwa shupavu katika kutetea haki za jamii zilizotengwa, watetezi wa haki za mazingira na wanaharakati wasanii wa kifeministi. Shinaz yuko kwenye **Instagram**: @nubianqueenbiz_zaids na pia kwenye **LinkedIn**: Shinaz Rehema Ali





**Tariro Tandi** ni mwanasheria wa haki za binadamu na mwanaharakati anayefanya kazi kama Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo na UAF-Afrika. Yeye ni mtetezi wa afya ya kiakili na mwanablogu anayeeneza uelewa juu ya afya ya akili, kushiriki msukumo na ustadi wa kukabiliana, kutafuta njia za kipekee za kuzungumza juu ya mhemko, magonjwa ya akili, afya, ustawi na maisha kwa ujumla. Unaweza kupata maandishi yake kwenye https://tarytells.com/ na anapatikana tarirotandi@gmail.com

**Thato Mphuthi** ni mzungumzaji hodari na mwanaharakati wa sababu zinazozingatia uraia kamili, afya ya kijinsia na uzazi, kazi ya utunzaji bila malipo dhidi ya kazi nzuri, kujitunza na uongozi; kati ya wengine. Yeye ni kiongozi mwenye moyo mkuu na shujaa katika dhamira ya kufanya athari kubwa ulimwenguni. Mbali na sifa zake kadhaa, ni moyo wake na shauku ya kuendesha mabadiliko chanya katika jamii ya ulimwengu ambayo humfanya kuwa nguvu ya kuhamasisha ambayo ni yeye.





**Zanele Mbugua** ni mfeministi na mwanaharakati wa Kiafrika ambaye ana shauku kuhusu utetezi wa haki za womn na wenye jinsia kinzani. Alihitimu na Shahada ya Sanaa katika ulingo wa Saikolojia na Sosholojia kutoka katika Chuo kikuu cha Rhodes (Afrika Kusini) na kwa sasa anasomea shahada ya Uzamili katika ulingo wa Masomo ya Jinsia na Maendeleo katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Zanele ameishi muda mwingi wa maisha yake jijini Johannesburg, Afrika Kusini na aliweza tu kurudi katika nchi yake asilia, Kenya, mnamo mwaka wa 2018. Kwa sasa yeye ndiye Bingwa wa Feminist Republik ambaye ana shauku kuhusu uwezeshaji wa ustawi kamili, utunzaji wa pamoja, na haki ya uponyaji inayojizalisha upya. Unaweza kumpata Zanele kupitia \
**Istagramu:** @zane_ee and
**LinkedIN:** Zanele Mbugua

**Esther Kyozira** Kabla ya hivi karibuni kubadilisha jukumu na kuchukua hatamu ya Afisa Mkuu Mtendaji katika Umoja wa Kitaifa wa Watu Wenye Ulemavu wa Uganda al;maarufu the National Union of Disabled persons of Uganda (NUDIPU), Esther Kyozira alikuwa Afisa Mpango wa Mfuko wa Haki za Walemavu (Disability Rights Fund) na Mfuko wa Utetezi wa Haki za Ulemavu nchini Uganda (the Disability Rights Advocacy Fund in Uganda). Hapo awali, Esther aliongoza mipango huko NUDIPU na kuratibu Mradi wa teknolojia ya juu chini ya Chama cha Kitaifa cha Wasioona cha Uganda, almaarufu Uganda National Association of the Blind. Amefanya kazi pia kushawishi sera na sheria muhimu za kitaifa, kama vile Muswada wa Kitaifa wa Ulemavu nchini Uganda, na amekuwa akifanya kazi kwa karibu na Asasi za walemavu kufuatilia utekelezaji wa malengo ya ruwaza ya kimaendeleo - SDG. Yeye pia anahudumu kama mwakilishi wa wanawake wenye ulemavu kwenye Chama cha Kitaifa cha Mashirika ya Wanawake nchini Uganda na Mwakilishi wa Walemavu kwenye Bodi ya kutoa Fedha za Elimu ya Juu kwa Wanafunzi na hapo awali aliwahi kuwa mwanachama wa Baraza la Kitaifa la Walemavu kama Mwenyekiti wake na Wakfu wa Vipofu wa Uganda. Esther ana shahada ya Uzamili ya Sanaa katika somo la Haki za Binadamu na Shahada ya Sanaa katika Elimu zote zikiwa ni kutoka Chuo Kikuu cha Makerere Kampala na Stashahada ya Sheria kutoka Kituo cha Maendeleo ya Sheria - Uganda.



**ICODZIM** ni shirika ambalo lilianzilishwa na linaongozwa na womn na ni la womn. Shirika hili linatafuta kufikia usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na kuimarisha nafasi yao ya kiuchumi. Hatua za shirika hujaribu kushughulikia kanuni za kijinsia na usawa wa kijinsia mapema katika maisha, kabla ya hali za kasumba za kijinsia kukita mizizi ndani ya womn waliotengwa. Kwa hivyo, ICODZIM inakuza haki za womn kupitia kubuni majukwaa kwa womn ili kupaza sauti zao na kushawishi sera na maamuzi ambayo yanawaathiri ili kuwezesha mabadiliko ya kijamii na kiuchumi katika maisha ya wanawake.

**Barua pepe:** director@icodzimbabwe.org
info@icodzimbabwe.org
**Tovuti:** www.icodzimbabwe.org
**Facebook:** Institute for Community Development in Zimbabwe (ICOD ZIM)
**Twitter:** @icodzimtrust

ICOD ZIMBABWE
EMPOWER • PROMOTE • PROTECT

**Mfuko wa Haki za Ulemavu,** almaarufu The Disability Rights Fund (DRF) ni ushirikiano wa kutoa ruzuku kati ya wafadhili na jamii ya haki za walemavu ulimwenguni ambayo hutoa rasilimali za kifedha na kiufundi kwa mashirika ya watu wenye ulemavu kutetea haki sawa na ushiriki kamili katika jamii. Tangu 2008, DRF na shirika dada, Mfuko wa Utetezi wa Haki za Walemavu - the Disability Rights Advocacy Fund (DRAF), wamefadhili mashirika ya watu wenye ulemavu kote ulimwenguni katika nchi zinazoendelea - haswa barani Afrika, Asia, Visiwa vya Pasifiki, na Karibiani - kushiriki katika uthibitisho, utekelezaji, na ufuatiliaji wa Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu – Convention on the Rights of Persons with Disabilities (CRPD).
**Tovuti:** https://drafund.org/

**Teki** Ni neno la Kiamhariki linalotokana na kitenzi "Metekat", ambalo linamaanisha kuchukua nafasi ya mwengine. Mifuko ya Karatasi ya Teki ni biashara ya kijamii na mazingira iliyoundwa na kwa jamii ya viziwi. Lengo letu ni kuunda ajira endelevu ili kuwawezesha wanawake viziwi wakati wa kujenga nchi ya Ethiopia ambayo haina mifuko ya plastiki Ethiopia. Na unajua nini?... Inafanya kazi. Katika Teki tunawasiliana tu kwa Lugha ya Ishara, kutoka kwa mauzo hadi uzalishaji. Hii ni ya kipekee, na mteja anapoingia kwenye mlango wetu, tunabadilisha hadithi. Ndio ambao hawaelewi chochote sasa. Mara tu tutakapowatoa kutoka kwa eneo lao la ujuzi, umakini wao huongezeka, na tunaweza kuwashawishi waache kutumia mifuko ya plastiki kuanzia sasa hadi milele. Hawatasahau dakika hizo chache kwa maisha yao yote.

**Barua pepe:** reachus@tekipaperbags.com
**Twitta:** @TekiPaperBags
**https://www.tekipaperbags.com**

**Dzuwa ni chapisho huru la uhariri lililoletwa kwako na jarida la the Feminist Republik, ambalo linajulikana kirasmi kama Jukwaa la Wanawake wa Kiafrika ambao ni Watetezi wa Haki za Binadamu, almaarufu The African Women Human Rights Defenders Platform.**

**Limefadhiliwa na shirika la Urgent Action Fund-Afrika kama nafasi iliyojaa usimulizi wa hadithi, kushiriki na kujifunza kuhusu ulinzi kamilifu, uponyaji kamili, ustawi na utunzaji wa kimageuzi unaowalenmg, na unaotolewa na Waafrika wanawake, wabadili jinsia na wasiowiana na jinsia yoyote ambao ni watetezi wa haki za binadamu na jamii zao ili kupata msukumo wa ukwasi wa uthabiti katika harakati zao...**

**Wasiliana nasi kupitia barua pepe: feministrepublik@uaf-africa.org**
**Facebook: The Feminist Republik**
**Instagramu: @feminist_republik**
**Twitta: @feminist_rep**

**DZUWA II Juni 2021**

The Feminist Republik